# Nipashe

Jumatatu Desemba 2, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580090

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Asimulia alivyofukuzwa kazi kwa kukataa rushwa ngono

UKURASA 2




UKURASA 13

# Masharti 9 waangalizi uchaguzi mkuu 2020

UKURASA 2




Baadhi ya makundi ya washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani wakiwa wameshika mabango yaliyoandikwa jumbe mbalimbali wakipita mbele ya mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Ajira, na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyemwakilisha Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, katika kilele cha sherehe hizo kitaifa kwenye Uwanja wa Rock City Mall jijini Mwanza, jana. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE.**

## MAAMBUKIZO YA UKIMWI TISHIO KUBWA KWA VIJANA

UKURASA 3




# Aliyepita bila kupingwa akataliwa na wananchi

**MBUNGE** awatuliza, awaambia... *Endelea ukurasa wa 2*

**MICHEZO** MWAKYEMBE AWALILIA MASHABIKI WA MWAKINYO UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Masharti 9 waangalizi uchaguzi mkuu 2020

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeanza mchakato wa kupata waangalizi wa ndani wa uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka 2020.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwa vyombo vya habari (siyo Nipashe), na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, mwisho wa kupokea maombi hayo ni Januari 31, mwakani.

Waombaji hao wametakiwa kuhakikisha wanakamilisha masharti tisa, ikiwamo ya kuwa na watendaji Watanzania wawili kwa taasisi inayohusisha watendaji wa kimataifa. Pia wanatakiwa kuwa na anwani kamili ya taasisi, mahali/sehemu taasisi inapofanyakazi, shughuli zinazofanywa na taasisi husika kwa mujibu wa hati ya usajili.

Masharti hayo ya NEC pia yanataka sehemu ambazo asasi/taasisi inataka kufanya zoezi hilo pamoja na taarifa zao za idadi ya watu watakaotumika kwenye kazi hiyo.

Vile vile, wametakiwa kutaja majina na namba za simu za viongozi wa asasi/taasisi husika kama yalivyoandikwa katika hati za usajili.

Nec kadhalika inataka kuambatanishwe nakala/kivuli cha hati ya usajili wa taasisi au asasi pamoja na kivuli cha katiba zake.

"Tume baada ya kupokea barua za maombi itazitaarifu taasisi/asasi husika iwapo zimekubaliwa au kukataliwa," ilibainisha. Kwa mujibu wa Katiba, uchaguzi mkuu unafanyika Oktoba 25, kila baada ya miaka mitano kwa ajili ya wananchi kuchagua Rais, wabunge na madiwani.



Wakazi wa mji wa Musoma mkoani Mara wakishangaa maji ya mvua kubwa ilionyesha jana na kusababisha mafuriko maeneo ya Machinjioni na Kariakoo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Asimulia alivyofukuzwa kazi kwa kukataa rushwa ya ngono

Na Elizabeth Zaya

MADHARA yanayowapata baadhi ya wafanyakazi wanawake kazini kwa kuombwa rushwa ya ngono ni pamoja na kunyanyasika au kufukuzwa kazi wanapokataa kutimiza matakwa ya mabosi wao.

Stell Igidio, ni mmoja wa wafanyakazi aliyepitia changamoto hiyo na anasimulia namna alivyofukuzwa kazi baada ya kukataa kushiriki ngono na bosi wake na kukutana na 'vigingi' vya kuombwa rushwa ya ngono akitafuta haki yake ya kurudishwa kazini.

Akihojiwa katika moja ya televisheni zinazoendesha shughuli zake kwa njia ya mtandao, Stella ambaye alitafuta haki yake na kurudishwa kazini baada ya kushinda kesi, alisema alifukuzwa kazi kwa kukataa kusafiri na mkuu wake wa kazi aliyemwomba asafiri naye kwa ajili ya mapumziko ya kimapenzi.

"Bosi wangu aliniita siku moja akaniambia kwamba anataka asafiri na mimi 'weekend' kwenda nje ya mkoa kwenye mapumziko ya kimapenzi na pia kwenda kuitangaza taasisi yake huko, nilishtuka sana na sikukubaliana na suala hilo," alisema Stella.

"Baada ya kukataa, akabadilisha na kusema basi twende weekend iliyokuwa inafuata, pia nikakataa kwa kumwambia nashukuru kwa ofa lakini sitakwenda."

Kitendo cha kukataa mara kadhaa ombi la mkuu wake wa kazi, alisema kilisababisha aanze kufanyiwa visa hadi kufukuzwa kazi.

Hata hivyo, Stella alisema hakukubaliana na hatua ya kufukuzwa kazi kwa kuamini kuwa hakuwa na kosa.

"Niliomba ushauri kwa wanasheria baada ya kufukuzwa ili kufahamu namna ya kupata haki yangu na waliniambia kwamba nianze kwa kukata rufani katika bodi ya kazini kwangu, nilifanya hivyo kwa kumtafuta mwenyekiti wake ambaye naye alinikatisha tamaa baada ya kuniambia ili nishinde natakiwa kuwa karibu naye sana," alisema Stella.

"Alikuwa anataka niwe naye kimapenzi na akinihakikishia kwamba nikikubali kufanya hivyo nitashinda na nitarejeshwa kazini, nilikataa

INAENDELEA UK. 8

## Aliyepita bila kupingwa akataliwa na wananchi

Na Enock Charles

WANANCHI wa Kijiji cha Ng'ombe, wilayani Misungwi mkoani Mwanza, wamemkataa mwenyekiti aliyepita bila kupingwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 24, mwaka huu.

Kiongozi huyo anatuhumiwa kwa rushwa na uchochezi, huku wananchi wakishangazwa na ushindi wake kwa kuwa kwenye kura za maoni ndiye aliyekuwa na kura chache kuliko wagombea wote.

Wananchi hao walitoa dukuduku lao mbele ya Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga, ambaye aliwatuliza kwa kuwaambia kuwa taratibu zilizomwingiza ndizo zitatumika kumwondoa.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara walisema aliyetangazwa kuwa mwenyekiti ambaye alishawaongoza kwa miaka 15, Zakayo Magongo (CCM), hakuchaguliwa na wananchi wa kijiji hicho.

"Amani haipo watu tunatafutana na tanutafutana kwanini kwa sababu watu wameng'ang'ania madarakani pasipo kuchaguliwa hata hapa ukiangalia hakuna hata kiongozi mmoja aliyefika kwenye hiki kikao," alisema mmoja wa wananchi hao.

"Tuliyemchagua (kura za maoni ndani ya CCM) alipata 300, yeye (aliyepita bila kupingwa) alipata 100 na kitu, cha ajabu jina lake yule ambaye hatukumchagua ndiye tumchague awe kiongozi wetu," alisema mwananchi mmoja na kuongeza:

"Ameongoza kwa miaka 15 hawakufanya kitu chochote katika kijiji hiki kwa hiyo hatumtaki kabisa."

Aidha, wananchi hao wamelalamikia kutokusomewa mapato na matumizi katika kijiji chao, pamoja na tabia za rushwa na uchochezi wa migogoro anazodaiwa kuwa nazo kiongozi wao kiasi cha kukosa imani na uongozi wake.

"Tuna tatizo kubwa la kutosomewa mapato na matumizi, sababu hakuna amani kwa vile watu wanang'ang'ania madaraka bila kuchaguliwa," alisema mwananchi mwingine.

"Ndiyo maana tumefika kwako Mbunge, lakini hatujui kama utatusaidia," alisema mwananchi mwingine.

Akijibu hoja ya wananchi hao Mbunge wa Jimbo hilo, Charles Kitwanga, aliwataka wananchi hao kuwa watulivu wakati taratibu zilizomchagua zinafuatwa ili kumwondoa.

"Taratibu zilizompitisha lazima tufuate za kumtoa, na taratibu zenyewe lazima kiti kibaki wazi Mkurugenzi wa Uchaguzi ataitisha tena uchaguzi," alisema Mbunge huyo. Wiki iliyopita, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akizungumza kuhusu matokeo ya uchaguzi nchi nzima, alisema CCM ilipita bila kupingwa kwenye mitaa 316,474, vijiji na vitongoji.

Aidha, Chadema wamepata nafasi 69, ACT-Wazalendo nafasi 12 na Chama cha Wananchi CUF nafasi 8.

Hata hivyo, matokeo haya yalipingwa vikali na vyama vya upinzani kwa madai kuwa havikushiriki uchaguzi huo, hivyo kushangazwa kwa kitendo cha kutangazwa kuwa wameshinda uchaguzi huo katika baadhi ya vitongoji, vijiji na mitaa.

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya makundi ya washiriki wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani wakipita huku wakiwa wameshika mabango yaliyoandikwa jumbe mbalimbali mbele ya mgeni rasmi Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Bunge, Kazi, Ajira, na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, aliyemwakilisha Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, katika kilele cha sherehe hiyo iliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Rock City Mall jijini Mwanza. **PICHA: ELIZABETH FAUSTINE.**

# Vijana waongoza maambukizo VVU

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

KUNDI la vijana hasa wa kike linadaiwa kuongoza kwa kuwa na maambukizo mapya ya virusi vya Ukimwi kwa mujibu wa takwimu za maambukizi ya virusi hivyo kwa mwaka 2016/2017.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Rock City Mall jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema katika maambukizi mapya 72,000 vijana ni asilimia 40 na kati

INAENDELEA UK. 8

## Wazalishaji umeme binafsi wategwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amesema atawachukulia hatua wazalishaji binafsi wa umeme watakaobainika kutoza Sh. 3,500 badala ya Sh. 100 kwa uniti moja.

Dk. Kalemani alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa alipokuwa akizungumza na makandarasi wa miradi ya nishati vijijini, menejimenti ya Tanesco, REA na wazalishaji wa vifaa vya kuunganisha umeme.

Alisema amepokea malalamiko katika Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza kwamba wananchi wanatoza Sh. 3,500 kwa uniti moja wakati bei halali iliyopangwa na serikali ni Sh. 100 kwa uniti.

"Wazalishaji wadogo naomba muache tabia hiyo na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma

za Nishati na Maji (EWURA) nilishawaeleza, bei za wananchi kulipia ziwe zilizopangwa na serikali kama unaona hupati faida acha, kufanya biashara hiyo," alisema Dk. Kalemani.

Alisema katika maeneo ya visiwani kama Ukerewe na Mafia kwa wazalishaji binafsi bei ni moja lazima zilingane hakuna bei tofauti.

"Nikisikia wanaendelea nitamwagiza mkuu wa wilaya awakamatie huko huko una mkataba wa miaka 20 lazima tu utapata faida nataka nijue mkandarasi gani anafanya hivyo tuchukue hatua, nisisikie mtu analalamika kuhusu jambo hilo," alisema Dk. Kalemani.

Alisema kupeleka umeme visiwani makandarasi wamepewa ruzuku ya serikali na baadhi ya wadau wamechangia bei ya kuunganisha umeme nchi nzima, lazima kwa hiyo inatakiwa kulingana yani Sh. 27,000 na hata bili zilingane.

Aliwataka makandarasi kuhakikisha kazi za kusambaza umeme vijijini zinakamilika kama ilivyopangwa kwa kuwa kila mmoja amepewa mkataba wa miezi 24 kumaliza kazi ifipao Juni 2020. Alisema mpaka sasa umeme umshawashwa katika vijiji 8115 nchi nzima kati ya vijiji 12,268.

Alisema lengo ni kuhakikisha ifikapo Desemba 31 mwaka huu vijiji 10,446 vitakuwa vimefikishwa na umeme na kubaki vijiji 1,822.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Dk.Tito Mwinuka, alisema wameendelea kuweka mchango wao kwenye suala la umeme vijijini kwa vijiji vilivyopitiwa na njia za umeme.

Alisema awamu ya kwanza walilenga vijiji 390 ambapo kati ya hivyo, vijiji 163 viko kwenye utekelezaji na vijiji 14 vimeshawashwa umeme.

## Halmashauri 16 zina upungufu wa chakula

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HALMASHAURI 16 nchini zimetajwa kukabiliwa na upungufu wa chakula baada ya kufanyiwa tathmini ya hali ya chakula iliyofanywa na Wizara ya Kilimo na kwamba serikali imejipanga kukabiliana na changamoto hiyo.

Halmashauri hizo ni Kongwa, Mpwapwa, Chwamwino, Bahi, Simanjiro, Longido na Musoma. Nyingine ni Same, Mwanga, Rorya, Manyoni, Kishapu, Shinyanga, Korogwe, Mkinga na Nzega.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu na Menejimenti ya Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Matamwe Said, wakati akifungua mafunzo ya wataalamu wa uchambuzi na tathmini ya usalama wa chakula na lishe nchini (Mchali).

Kanali Said alisema kila mwaka Wizara ya Kilimo imekuwa ikitoa taarifa ya hali na usalama wa chakula nchini na kwa mwaka huu tathmini hiyo awali ilifanywa kwenye halmashauri 46 ambazo zilikuwa na viashiria vya upungufu wa chakula hata hivyo, baada ya mvua kunyesha halmashauri 16 ndio zilionekana bado zina chagamoto ya uhaba wa chakula.

Alivitaja vigezo vilivyotumika katika kufanya tathmini ya hali ya chakula kwa halmashauri hizo 16 zenye changamoto ya chakula ni kuangalia upatikanaji wa chakula, soko na usalama wa chakula .

Mkurugenzi huyo alisema tathmini hiyo ililenga kujua sababu za halmashauri hizo kuwa na upungufu wa chakula ili kuangalia namna ya kukabiliana na changamoto hiyo.

"Miaka 1980 hadi 1984 ndio tulishuhudia upungufu wa chakula nchini, lakini kwa sasa nchi haina njaa isipokuwa yapo maeneo machache kwenye baadhi ya halmashauri nchini zina changamoto kidogo za upungufu wa chakula hata hivyo, kama nchi inafanya mipango na mikakati ya kitaifa ya kukabiliana na hali hiyo," alisema Kanali Said.

Alisema kila mkoa umeweka mikakati yake katika kukabiliana na hali hiyo kwa kuwasaidia wananchi waliokumbwa na upungufu wa chakula ikiwamo kuwauzia kwa bei nafuu na pia ipo mikakati ya kuimarisha maghala ya kitaifa, hivyo mkutano wa wataalamu wa tathmini utasaidia serikali kujua hali na usalama wa chakula.

Naye Kaimu Mkurugenzi Idara ya Usalama wa Chakula na Lishe, Tatu Kayumbu, alisema Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa ( (FAO ) kwa kushirikiana na serikali, limetoa mafunzo hayo kwa wataalamu wa timu ya uchambuzi na tathmini ya usalama wa chakula na lishe hanchini kwa kutumia mfumo wa uainishaji wa madaraja mbalimbali ya usalama na lishe (IPC). Alisema kuwa mafunzo hayo yataendeshwa sambamba na kazi ya uchambuzi na uandaaji wa taarifa ya hali ya chakula na lishe ili nchi iweze kuchukua hatua stahiki kulingana na taarifa hiyo. Aidha, aliwashukuru wawakilishi FAO kwa kuwezesha mafunzo.




# Watendaji wakala maji kuwekwa kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amesema leo atakutana na Watendaji wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kutokana na kutoridhishwa na utendaji kazi uliopo.

Prof. Mbarawa alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akipokea ripoti ya utendaji kazi wa Ruwasa katika Wilaya ya Chamwino.

Alisema kasi ya utendaji kazi iliyopo inaweza kuchelewesha matarajio ya wananchi wa vijijini katika kuondokana na adha ya maji.

"Tangu Ruwasa imeanza kazi Julai mwaka huu, kasi yake ni ndogo na hairidhishi mnachelewesha malipo na kusababisha makandarasi wengi wanaotekeleza miradi wananilalamikia wanapiga simu," alisema.

Hata hivyo, alisema anashangazwa na kucheleweshwa kwa malipo kwa makandarasi wakati wizara ilishatoa fedha hizo kwa ajili ya yao baada ya kukamilisha na kazi.

"Nimepigiwa simu na mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wilayani Longido analalamika kutolipwa fedha kutokana na kazi ambazo ameshatekeleza, wakati anajua fedha zimeshatoa," alisema.

Waziri huyo alisema uongozi wa juu wa wakala huo haumpi shaka isipokuwa kuna viongozi wa kada ya chini wanafanya kazi kwa urasimu na hivyo kukwamisha miradi.

"Jumatatu (Leo) nitakutana na Ruwasa nizungumze nao maana kasi ya utendaji kazi wao hairiridhishi," alisema.

Alisema Ruwasa ilipoanza matarajio ya watu wengi yalikuwa makubwa, lakini kutokana na kasi ndogo ya utendaji wake, inatia shaka yanaweza yasifikiwe.

Alisisitiza kuwa kwa sasa wizara imefuta utaratibu wa kutangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata makandarasi kwa kuwa utaratibu huo unachelewesha miradi na kusababisha gharama kubwa ikilinganishwa na wizara kutumia watalaamu wake.

Alisema wizara itatumia watalaamu wake kutekeleza miradi hiyo na katika uchimbaji visima ambapo watatumia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa

INAENDELEA UK. 8



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kinyerezi JICA, wakipita kwenye daraja lililotengenezwa kwa mbao wakitoka shuleni hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NSSF sasa kufanya tathmini nyumba zake

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limeanza kufanya tathmini ya bei ya upangishaji wa nyumba zake za Toangoma, Mtoni Kijichi na Dugu jijini Dar es Salaam.

Aidha, shirika hilo kwa kushirikiana na wizara, leo litatangaza wataalamu watakaofanya utafiti utakaowezesha NSSF kupanga bei ya nyumba hizo.

Uamuzi huo ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyetaka kufanyia kwa tathmini ya bei halisi ya upangishaji wa nyumba hizo na gharama za ujenzi.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kazi hiyo itakamilika mwishoni mwa mwezi huu, kuhakikisha wateja na shirika wananufaika na uwapo wa raslimali hizo.

"Tulikuwa na ujio wa mheshimiwa Waziri Mkuu akifuatana na mawaziri katika kuangalia miradi ya nyumba tulizozijenga katika maeneo ya Tuangoma, Mtoni Kijichi na Dungu. Lengo la ziara hiyo ilikuwa kuhakikisha kwamba zile nyumba zilizokamilika ziweze ama kuuzwa au kupangishwa kwa wananchi ili kuwafanya wananchi wawe na makazi bora, lakini vile vile kutuwezesha sisi kupata mapato yanayotokana na uwekezaji huu," alisema.

"Lakini kabla ya kuuza au kupangisha kunatakiwa kufanyike tathmini ya kitaalamu kwamba nyumba hizi ziuzwe kwa bei ipi au zipangishwe kwa bei ipi suala hilo tunao wataalamu ndani ya serikali wakiongozwa na mthamini mkuu wa serikali ambao tulielekezwa na Waziri Mkuu, tunashukuru kwamba tumewapata na mara moja wameweza kufika katika eneo hili ili wafanye tathmini hiyo," alisema Erio.

Mthamini Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha, alisema wamefika katika maeneo ya miradi hiyo ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Waziri Mkuu ya kwenda katika maeneo hayo ili kufanya tathmini na kutoa bei ya soko kwa nyumba hizo.

"Kama mlivyosikia tulipokea maelekezo kwamba tuje tufanye ukaguzi na kutoa bei ya soko ya hivi sasa kwa nyumba hizi ambazo bei hizi zitawafanya Watanzania waweze kupanga au kukunua nyumba hizi," alisema Mugasha.

"Leo ni ukaguzi wa awali, tategemea wataalamu watakuja kuchukua taarifa zote na kufanya tathmini, pia tutafanya utafiti kwa sababu vitu hivi vinatofautiana kutokana na mahali, kazi hii tutaifanya kwa uadilifu na tutaikamilisha ndani ya muda mfupi ili Watanzania waje kujipatia nyumba hizi," alisema Mugasha.

# Mkuu wa chuo kortini madai kuomba rushwa

**Na Jumbe Ismailly,** IRAMBA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Singida, imewapandisha kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Iramba watu wawili akiwamo Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC) Msingi kwa tuhuma za kuomba rushwa ya shilingi milioni tano.

Kesi hiyo ambayo ipo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Iramba, Sydney Nindi inawahusisha Mkuu wa FDC Msingi, Elia Wony Jackson Urio na Mhandisi Mshauri, Ahmed Mohamed Ahmed.

Mwendesha Mashtaka wa Takukuru Mkoa wa Singida, Edsoni Mapalala, alidai kwamba Septemba13, mwaka huu walitenda makosa hayo kwenye maeneo ya Manispaa ya Singida, mkoani Singida.

Kwa mujibu wa Mapalala, FDC Msingi ilitangaza zabuni ya kusambaza mbao za kujengea majengo ya chuo hicho, na kwamba mfanyabiashara aliyemtaja kwa jina la Aikande Amani Swai ndiye aliyeshinda zabuni hiyo.

Mapalala hata hivyo alidai kwamba baada ya mfanyabiashara huyo kushinda tenda hiyo ndipo mkuu wa FDC Msingi alipokwenda kwa mfanyabiashara huyo na kumwomba rushwa ya shilingi milioni tano ili aweze kumkabidhi kazi hiyo, vinginevyo kazi hiyo hataweza kuipata.

Mwendesha mashtaka huyo alidai zaidi kuwa baada ya Aikande kugoma kutoa kiasi hicho cha fedha ndipo mkuu wa chuo hicho alitoa kazi ya kusambaza mbao kwa mtu mwingine.

Hata hivyo washtakiwa hao baada ya kusomewa shtaka lao wamekana na wapo nje kwa dhamana ya shilingi milioni tatu kila mmoja hadi Desemba 11, mwaka huu kesi hiyo itakapoanza kusikilizwa kwa uchambuzi wa awali.

# Uvamizi shoroba wapunguza simba

**Na Mwandishi wetu**

ASILIMIA 60 ya simba nchini wanaishi nje ya hifadhi za taifa kutokana na uvamizi wa mapito ya wanyama maarufu kama shoroba na mtawanyiko yanayounganisha maeneo yaliyohifadhiwa.

Taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya 'Be the Pride.com' imeonyesha jinsi simba wanavyoendelea kupungua kwenye maeneo mbalimbali barani Afrika. Mtandao huo kupitia ukurasa wa 'WildAID' umebainisha kuwa ndani ya miaka 20 iliyopita, idadi ya simba wanaoishi porini imeshuka kwa karibu nusu kutokana na vitisho.

Walisema uvamizi wa binadamu kwenye maeneo ya mtawanyiko na mapito ya wanyama kuna watu zaidi ya 350,000, na kwamba kuna ushindani wa rasilimali ardhi na maeneo ambayo ni makazi halisi ya simba.

Walisema mvutano baina ya wanyama na binadamu ni kwenye matumizi ya ardhi, kwa kuwa wanataka kufungua mashamba na wakati huo wanyama wanakwenda kujipatia mahitaji muhimu. Kadhalika, changamoto nyingine ni wanyama na mifugo kugombania malisho ambayo ni chakula cha simba.

"Kitendo hiki huwasukuma wanyama wawindaji kuwa karibu zaidi na wanadamu. Mifugo inapouawa mara nyingi simba huwa ndiyo walengwa wa kwanza wa mauaji ya kulipiza kisasi," ilibainisha sehemu ya taarifa hiyo. Ilieleza kuwa ujangili wa wanyamapori umepungua kwa kiasi kikubwa, na kwamba simba hunaswa na mitego haramu iliyowekwa na majangili kwa ajili ya kupata nyamapori.

Mwaka juzi simba sita wa Hifadhi ya Taifa Serengeti (Senapa), waliuawa kwa kuwekewa sumu kwenye mzoga wa ng'ombe katika eneo la Mugumu, ikiwa ni namna ya kulipiza kisasi baada ya simba kula mzoga.

Kadhalika, fisi walikufa baada ya kula mabaki ya nyama hizo, jambo ambalo liliathiri ustawi wa simba ambao ni kivutio kikubwa cha utalii.



# HALMASHAURI YA MJI KAHAMA

## TANGAZO LA ZABUNI

**Zabuni Na. LGA/155/2019/2020/NC/01 na LGA/155/2019/2020/ W/01**

1. Halmashauri ya Mji Kahama inakaribisha maombi ya Zabuni za huduma ya kuzoa taka ngumu kutoka kwa wazalishaji hadi dampo kuu za Busoka, kukusanya ada ya taka ngumu na pia kuwapata mafundi ujenzi (Local Fundi) kwa kazi mbalimbali za ujenzi katika Halmashauri ya Mji Kahama kutoka kwa Watu binafsi, vikundi au Kampuni zenye kutoa huduma hizo kwa kipindi cha kuanzia January 2020 hadi Juni 20120 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. Vikundi, makampuni au watu binafsi mnakaribishwa kuleta maombi yenu kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka ngumu, kukusanya ada ya taka ngumu na kufanya shughuli za ujenzi (Local Fundi) katika makundi yafuatayo:

**A. ZABUNI YA KUZOA TAKA NGUMU, KUZISAFIRISHA TOKA KWA WAZALISHAJI HADI DAMPO KUU LA BUSOKA NA KUKUSANYA ADA YA TAKA NGUMU. ZABUNI NAMBA LGA/155/2019/2020/NC/O1**

Zabuni hii imegawanyika katika kanda mbalimbali ambazo mwombaji anaweza kuomba kanda moja wapo au kuomba kanda zote au kuomba kanda kulingana na uwezo wake kama ifuatavyo:

| KANDA | SHUGHULI | KATA |
|---|---|---|
| A | Kukusanya taka ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, majengo ya biashara, taasisi mbalimbali na kuzisafirisha moja kwa moja hadi dampo kuu Busoka pamoja na kukusanya ada ya tozo ya taka ngumu | KAGONGWA NA MWENDAKULIMA |
| B | Kukusanya taka ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, majengo ya biashara, taasisi mbalimbali na kuzisafirisha moja kwa moja hadi dampo kuu Busoka pamoja na kukusanya ada ya tozo ya taka ngumu | NYIHOGO, MTAA WA IGALILIMI, KAHAMA MJINI, MAJENGO NA MALUNGA |
| C | Kukusanya taka ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, majengo ya biashara, taasisi mbalimbali na kuzisafirisha moja kwa moja hadi dampo kuu Busoka pamoja na kukusanya ada ya tozo ya taka ngumu Kukusanya taka ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, majengo ya biashara, taasisi mbalimbali na kuzisafirisha moja kwa moja hadi dampo kuu Busoka pamoja na kukusanya ada ya tozo ya taka ngumu | MHONGOLO |
| D | Kukusanya taka ngumu kutoka kwenye makazi ya watu, majengo ya biashara, taasisi mbalimbali na kuzisafirisha hadi kwenye vizimba/ghuba pamoja na kukusanya ada ya tozo ya taka ngumu | NYASUBI NA MTAA WA MBULU MISSION |
| E | Kuzoa taka ngumu kutoka kwenye vizimba/ghuba na kusafirisha hadi dampo kuu Busoka ndani ya Halmashauri ya Mji Kahama. | Kwa kata ambazo zitakosa mzoaji wa taka toka kwa wazalishaji hadi dampo kuu Busoka |

**A. ZABUNI ZA KUWAPATA MAFUNDI UJENZI (LOCAL FUNDI). ZABUNI NAMBA LGA/155/2019/2020/W/O1**

Zabuni hii inahusu kuwapata mafundi ujenzi (local fundi) kwa ajili ya kazi mbalimbali za Halmashauri ya Mji Kahama. Mafundi hawa inatakiwa wawe ni mafundi wa ukweli na siyo dalali

**1. MASHARTI KWA WAOMBAJI**

1. Mwombaji awe na leseni hai kwa biashara husika inayohusika na shughuli za usafi na ukusanyaji wa mapato, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi(TIN), usajili wa kampuni au kikundi, usajili wa VAT kwa wale wanaokidhi matakwa ya kusajiliwa kwenye VAT, Tax clearance, uhalali wa kisheria wa kusaini nyaraka (Power of attorney).Mwombaji aambatanishe vielelezo halali vya kuonyesha umiliki wa kampuni hiyo (Memorandumu na articles of association/extract. Kwa mtu binafsi aonyeshe "affidavit" iliyopitishwa na Mwanasheria. CBO hazihusiki na sharti la leseni. Vikundi vya Kijamii (CBOs) waambatanishe orodha ya viongozi na kikundi na barua za utambulisho toka kata husika. Mwombaji aambatanishe wasifu wa kampuni (Company Profile)

2. Mwombaji kwa upande wa kuzoa taka ngumu toka kwa wazalishaji, kuzisafirisha kwenda dampo kuu la Busoka na kukusanya ada ya tozo za taka ngumu ataje kiwango cha asilimia (%) atakacholipwa na Halmashauri kutoka kwenye makusanyo. Makusanyo yote yote yanatakiwa kuingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri. Wakala atatumia mashine za risiti za kielectroniki (POS) za Halmashauri ya Mji Kahama.Kiwango cha Dhamana ya mkataba (Performance Security) ni makusanyo ya mwezi mmoja yaletwe kwa mfumo wa fedha taslimu "Cash"

3. Maombi yatalipiwa ada ya uzabuni ya **TZS 50,000/=** ambazo hazitarejeshwa, fedha hizi zilipwe ofisi ya Mkurugenzi wa Mji, S.LP 472, Kahama.

4. Mwombaji wa kukusanya taka ngumu anatakiwa awe na magari/trekta yenye uwezo wa kubeba tani 8 au zaidi na yenye uwezo usiopungua mita 9 za ujazo, Awe na wafanyakazi wenye uwezo wa kuhudumia Kaya/Majengo 150 kwa siku.

   Wafanyakazi wote wawe waadilifu na wenye umri zaidi ya miaka 18 na wapewe vifaa vya kazi pamoja na nyenzo za kujikinga (viatu vigumu, kofia ngumu, ovaroli, miwani, gloves na mask) vyote vikiwa na nembo ya Kampuni husika, Awe na ofisi yake inayotambulika katika Mji wa Kahama, Awe tayari kufanya kazi katika mazingira yenye miundombinu hafifu mfano; (barabara mbovu na njia zenye matope), Awe na uwezo wa kufanya kazi kabla ya kuanza kukusanya pesa angalau kwa mwezi mmoja, Awe tayari kulipia ushuru wa dampo kiwango cha 15% ya makusanyo ya ushuru kila mwezi kwa Mkurugenzi wa Mji Kahama, Awasalishe Bank Statement ya miezi 6 ya nyuma,

   Awasilishe kadi za umiliki wa magari na vifaa vingine alivyo navyo, Awe na uwezo wa kuondoa Taka ngumu mara mbili kwa wiki toka kila Kaya au Jengo

   Mwombaji anatakiwa aambatanishe ratiba inayoonyesha mzunguko wa Uzoaji Taka Ngumu (route) kwa kila siku ya kazi. Maeneo yatakayohusika yataambatanishwa katika tariff inayoonyesha gharama kwa kila aina ya jengo mara baada ya Mzabuni kukubaliwa maombi yake.

5. Vitabu vya Zabuni vinapatikana kwenye Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Mji Kahama, S.L.P 472, Kahama kuanzia Saa 1.30 Asubuhi hadi Saa 9.30 Alasiri

6. Maombi yote yajazwe kwa umakini na yaambatane na nakala halisi Moja na nakala iliyorudufiwa (Copy) Moja) na yafungwe vizuri kwa lakiri na juu ya bahasha andika jina la zabuni unayoomba. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 16/12/2019 saa 5.00 asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo na waombaji mnakaribishwa kuhudhuria sherehe za ufunguzi.

**Maombi yote yatumwe kwa:**

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA MJI,**
**S.L.P 472,**
**KAHAMA.**

7. Maombi yatakayochelewa au sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi ambayo hayakufunguliwa kwenye sherehe ya ufunguzi wa maombi , kwa hali yoyote ile hayatapokelewa na hayatakubaliwa kwa tathmini.

**Anderson D. Msumba**
**MKURUGENZI WA MJI**
**KAHAMA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Timuatimua makocha Simba, Yanga chanzo kuvurunda Caf

**HATIMAYE** baada ya tetesi zilizodumu kwa takribani wiki mbili kuhusu kutimuliwa kwa Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, zimetimia mwishoni mwa wiki, kufuatia uongozi wa klabu hiyo kutangaza kuvunja mkataba rasmi na Mbelgiji huyo.

Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, imesitisha mkataba wa kocha huyo ikiwa ni wiki tatu hivi tangu watani zao wa jadi, Yanga walipomtimua Kocha Mkuu, Mkongomani Mwinyi Zahera.

Kocha huyo wa Yanga, alitimuliwa kwa kile kilichoelezwa kuwa ni kutokana na kushindwa kuiunganisha timu hiyo kucheza vizuri jambo lililosababisha kutolewa kwenye michuano ya kimataifa na Pyramids FC ya Misri kwa jumla ya mabao 5-1.

Aidha, uongozi wa Yanga ulifafanua kuwa haukuona sababu kwa Zahera kushindwa kufanya vizuri kwa kuwa idadi kubwa ya wachezaji katika kikosi chake walisajiliwa kutokana na mapendekezo yake.

Zahera aliyerithi mikoba ya Mzambia George Lwandamina msimu uliopita akatimuliwa wakati timu hiyo ikiwa imecheza mechi tatu ikipoteza moja, sare moja na kushinda mchezo mmoja, hivyo timu kukabidhiwa kwa Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwasa.

Kwa upande wa Aussems aliyerithi mikoba hiyo kutoka Mfaransa Pierre Lechantre Julai mwaka jana, ametimuliwa wakati timu hiyo ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, imejikusanyia pointi 25 baada ya kucheza mechi 10, ikishinda nane, sare moja na kupoteza mchezo mmoja.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa, katika taarifa yake ameeleza kuwa uongozi umefikia hatua hiyo ya kumtimua Aussems kutokana na kushindwa kufikia malengo na viwango walivyokubaliana na klabu.

Katika taarifa yake imeeleza zaidi kuwa pamoja na Aussems kupewa ushirikiano hata baada ya kutolewa kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo malengo ilikuwa kufika hatua ya makundi ameendelea kusimamia bila kujali malengo ya Simba.

Malengo akiyataja kuwa ni kujenga timu yenye ari na mafanikio, nidhamu na ushindani kwenye mashindano ya ndani na nje ya nchi.

Kwa ujumla hatuwezi kupinga uamuzi uliofikiwa na Simba kama ambavyo pia tulishaeleza wakati Yanga ilipomtimua Zahera, kwa kuwa makocha hao wameshindwa kufikia malengo ya waajiri wao kama kweli yalikuwapo katika mikataba yao.

Lakini kinachotusikitisha na kutufanya kuamini itazichukua muda mrefu klabu hizi mbili kuweza kufikia malengo yao kwenye michuano ya kimataifa, ni kutokana na tabia ya timuatimua hii ambapo makocha huwa hawamalizi zaidi ya msimu mmoja.


Tulitarajia kama ambavyo inaelezwa Zahera alipewa nafasi ya kupendekeza wachezaji wakusajiliwa na hata Aussems ambaye inadaiwa alitoa mapendekezo lakini hayakuzingatiwa kama alivyohitaji, wangedumu na klabu hizo kwa angalau misimu miwili ama mitatu.

Tunatambua ili kuweza kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika ni pamoja na kocha kupata muda wa kutosha kuzifahamu mbinu, ugumu na hata fitina zilizopo kwenye mashindano hayo.

Lakini sasa, muda si mrefu klabu hizo zitatangaza makocha wapya na wanaweza wasiwe wameshawahi kuziongoza timu kwenye michuano hiyo Caf, lakini huenda wasipate hata nafasi ya kufanya usajili wanaoutaka.

Hivyo, ni wazi wakiingia katika michuano hiyo watakuwa wanaanza upya, huku wakihitaji muda zaidi kuvisuka vikosi vyao, jambo litakalozifanya kila msimu kuwa wasindikizaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kipa Zanzibar Queens asilie, atakuwa imara

Na Adam Fungamwango

**TUKIO** la golikipa wa Timu ya Soka ya Wanawake ya Zanzibar Queens, Hajra Abdallah, kuangua kilio baada ya kufungwa mabao 7-0 dhidi ya Tanzania Bara katika mechi ya mashindano ya Kombe la Chalenji, yaliyomalizika hivi karibuni, lilisikitisha wengi waliokuwa wakiangalia pambano hilo.

Ilikuwa ni mechi ya Kundi B ya michuano hiyo iliyoanza Novemba 16 hadi 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini Dar es Salaam na kikosi cha Kenya kutwaa ubingwa, uliokuwa unashikiliwa na wenyeji, Kilimanjaro Queens ya Tanzania Bara.

Kabla ya hapo Zanzibar ilikuwa imeshapoteza mechi mbili, dhidi ya Burundi na Sudan Kusini ambazo zote walikula mabao 5-0 kila mechi.

Wakati wenzake wameshikana mikono na ndugu zao wa Bara wakizunguka kuonyesha ishara ya upendo kwa kuwa wote ni ndugu moja, Hajra yeye alikuwa akibembelezwa na baadhi ya watu waliokuwa kwenye benchi ya ufundi la timu yake.

Golikipa huyo alilia kwa uchungu na kwa hisia kubwa. Wengine wanasema alikuwa analia kwa sababu aliona kama amewafungisha wenzake. Baadhi wanasema huenda wenzake walimlaumu kwa kufungwa magoli mepesi ndiyo maana amechukia na kulia.

Ukweli ni kwamba Hajra alikuwa akilia kwa sababu ni mshindani wa kweli. Kufungwa kwake ilikuwa ni kitu kilichomuumiza sana. Kwa nini afungwe? Alikuwa pia na uzalendo na Zanzibar.

Mchezaji mzuri mara nyingi ni yule ambayo anachukia kupoteza mechi.

Tatizo lilikuwa moja tu, uwezo. Hakuwa na uwezo wa kuzuia mashuti makali ya yaliyopigwa na Asha Rashid, Philomena Kizima, Donesia Minja na wengineo.

Si kwa sababu hana uwezo wa kukaa golini na kudaka, la hasha. Kwanza kabisa matatizo yanaanzia kwenye maandalizi ya timu yenyewe ya Zanzibar ambayo yalikuwa ya zimamoto, nadhani na pia kiuchumi haikuwa sawa.

Pili ni kwamba ukimwangalia Hajra ni mmoja wa wachezaji mwenye umri mdogo kwenye michuano hiyo.

Ukitafuta wachezaji watano kwenye michuano hiyo wenye umri mdogo, miongoni mwao atakuwa ni kipa huyo wa Zanzibar aliyedaka mechi hiyo dhidi ya Tanzania Bara.

Kwa maana hiyo umbile lake la kitoto, ndilo kwa kiasi kikubwa lilimfanya afungwe magoli yale.

Pamoja na kufungwa magoli yote hayo, lakini bado kuna wakati Hajra alikuwa akidaka mipira vizuri, kupangua, kupanga mabeki vizuri kwenye faulo na kuwafokea pale wanapojisahau, tofauti na umri wake pamoja na wenzake.

Kitu kingine kwa Hajra ni kwamba anaonekana anapenda kucheza. Anaupenda mchezo wenyewe na anafurahia kucheza.

Benchi la ufundi la Zanzibar Queens bado lina nafasi ya kumwendeleza kwa kumtunza golikipa huyo kwani inaonekana baadaye atakuja kuwa kipa nzuri sana si kwa Zanzibar, bali hata Tanzania yote.

Kitu kizuri kwa Hajra ni kwamba ameuanza mchezo wa soka akiwa na umri mdogo, hivyo baadaye atakuwa na kukomaa akiwa ndani ya soka.

Mara nyingi wacheza soka wanawake huanza mchezo huo wakiwa wakubwa, na hata kuna taarifa kuwa baadhi ya wachezaji wa Zanzibar walichukuliwa kutoka kwenye mchezo wa netiboli na kuletwa kucheza soka.

Yale mashuti aliyokuwa anapigiwa na kina Mwanahamisi Omari kila anapozidi kukua na kucheza soka atayazoea. Baada ya miaka miwili na kuendelea atakuwa mrefu, hivyo hatokuwa na matatizo tena na mipira ya juu.

Ukichanganya na kujituma kwake na kuupenda mchezo wa soka, atapata uzoefu na mafunzo na kuwa kipa mzuri na tegemeo kwa taifa.

Ana uwezo mzuri wa kuruka na hata 'timing', ila makocha itabidi wampe zaidi mazoezi ya mikono ili aweze kudaka bila kutema.

Hajra atakuwa kipa mzuri sana baada ya miaka michache kama ataendelea kucheza soka.

# *Kero usafiri Dar-mikoani*

**Mhariri,**

*MARA zote nimekuwa najiuliza mambo kadhaa katika ustawi wa maisha yetu wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, hasa inayohusu upatikanaji tiketi wa safari kwenda mikoa mingine.*

*Linalohusu wapiga debe wa daladala naliweka kando, katika maana ya kwamba wana 'utaratibu' wao tofauti, ingawa najua fika wanachokifanya si halali.*

*Kuna wanaopiga debe katika stendi kuu ya mabasi wakidai wanawakilisha kampuni na mabasi mbalimbali, kiulizo changu kikubwa ni katika uhalali wa matendo yao, pia namna yanavyoambatana na baadhi ya kero zisizovumilika.*

*Nitatoa mifano kadhaa. Abiria wa daladala anaposhuka katika kitu cha daladala, River Side Ubungo, ambako kuna mabasi yanayotoka Mnazi Mmoja kupitia Buguruni; Temeke, Mbagala, Gongolamboto, Segerea na Tabata wengi hukerwa sana na wapiga debe hao.*

*Pindi wanapomuona tu ana mizigo inayowapa dalili huenda ni abiria anayeelekea safari ya mbali, basi inakuwa shida kubwa hasa kinamama. Wanawavamia, baadhi kupora mizigo mikononi wakijaribu kulamizisha akakate tiketi katika basi analoliwakilisha, pasipo hata kujua anakoelekea.*

*Wengi wanaofanya hayo wanakuwa na nguo zenye nembo za 'mabasi yao' ambayo baadhi yana vituo ya tiketi jirani mahali hapo, japo siwapingi kwa hilo la kuwa na vituo jirani, ni mbinu nzuri za masoko yao na kumpa urahisi.*

*Shida yangu kuu ni namna uwakala huo wa huduma na biashara unavyoendeshwa. Badala ya kusimamia tija, wenyewe unaegemea kero zaidi.*

*Nimetoa mfano wa ushuhuda wa River Side Ubungo, lakini ndicho kinachojiri katika stendi ya mabasi yaendayo Kusini Temeke Mbagala jijini Dar es Salaam na mikoa mingineyo, hata katika mji wetu wa Kibaha.*


*Najua wa kwanza mnaoshughulikia hilo ni Wakala wa Usafiri Barabarani (Latra), pia halmashauri mbalimbali. Tafadhali wajibikeni kutuondolea kero hii.*

**Sixtus Mienda,**
**Mwedapole, Kibaha.**

## WASILIANA NASI:

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz

# Viongozi Yanga wasicheze ngoma ya Simba




**Na Adam Fungamwango**

**UKITAKA** kuharibikiwa na kupata tabu kwenye hii dunia, ishi kwa kumuiga mwenzako, au kuangalia jirani amefanya nini ili na wewe ufanye wakati hauna uwezo huo.

Tabu itakupata hata ukiwa na tabia ya kuishi kusikiliza majirani wanasema nini.

Maisha ya raha ni kuishi vile unavyoona wewe na utakavyo, iwe huna kitu au unacho.

Kwa siku za karibuni klabu ya Simba imekuwa ikionyesha kukamilika kwa viwanja vyao vya Bunju.

Vyombo vya habari na mitandao ya kijamii imekuwa ikionyesha picha za kukamilika kwa viwanja viwili, kimoja cha nyasi asili na kingine cha nyasi bandia, huku kukiwa na taratibu za kuzindua viwanja hivyo.

Wakati Simba wakijiandaa kuzindua uwanja wao, nikaona picha mbalimbali kwenye eneo la Yanga ambalo walipewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, maeneo ya Kigamboni zikionyesha katapila likiwa linang'oa miti.

Siku chache baadaye nikamsikia kiongozi mmoja wa Yanga akisema kuwa wao hawamtegemei mtu mmoja kuwajengea uwanja, ila watajenga kwa nguvu za wanachama wenyewe.

Sina maana kuwa wanachama na mashabiki wa Yanga hawawezi kufanya hivyo, lakini si lazima kwa viongozi wa Yanga kwa sasa kutaka kujibu nini watafanya kama watani zao wa jadi Simba walivyofanya.

Viongozi wa Yanga sasa wanatakiwa waendeshe klabu kwa yale ambayo kwa sasa wanaweza kuyafanya yaliyo ndani ya uwezo wao na si kuonekana kama wanataka kushindana na Simba.

Wanatakiwa wajiepushe zaidi na maswali ya waandishi yanayooenekana kutaka kuwapeleka kwenye ushindani mwingine na si wa soka uwanjani, kwa sababu wanaweza kujibu maswali ambayo hayapo kwenye malengo yao, au yatakuja kuwahukumu baadaye.

Hakuna mtu ambaye hataki maendeleo kama ambayo Simba wameanza kuyaonyesha, lakini wenzao kwa sasa wana mwekezaji, Mohamed Dewji, ambaye anafanya yote hayo, huku Yanga si tu haina mwekezaji, lakini hata haijafikiria kuingia kwenye mfumo wa uwekezaji.

Kwa sasa Yanga haitakiwi kabisa kuonekana inashindana na Simba kwenye miundombinu hasa ya uwanja, bali ijikite kutengeneza timu bora ili iweze kufanya vema na hatimaye kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara na si vinginevyo.

Ukweli upo pale pale kuwa kuna ugumu mkubwa kuwatumia wanachama na mashabiki kujenga uwanja na kama ingekuwa rahisi basi Simba na Yanga ambazo zina umri wa zaidi ya miaka 80 zisingekuwa na matatizo hata na viwanja vya kufanyia mazoezi.

Imepita miaka kadhaa, tangu Simba ilipoanzishwa hadi mwaka huu inapokaribia kuuzindua uwanja wake, ambao utaanza kwa kufanyia mazoezi, huku vizazi na vizazi vimepita ambavyo havijawahi kushuhudia kitu kama hicho cha klabu ikiwa na wanachama na mashabiki hadi alipokuja Mo, hivyo sidhani kama itakuwa rahisi sana kwa wanachama na mashabiki wa Yanga kwa kipindi kifupi tu eti kufanikisha jambo hilo.

Yanga inaweza kupata kiwanja chake cha mazoezi huko mbele ya safari, lakini haitakiwi kutaka kufanya hivyo haraka haraka kwa sababu wanachama na mashabiki wao watachekwa wa wenzao wa Simba, haitaweza.

Yanga kwa sasa inaweza kushindana na Simba na kuishinda ndani ya uwanja, vitu vingine isitake kushindana nayo kwa sababu itakuwa ngumu sana kutokana na mfumo ambayo kwa sasa inao.

Kwa sasa viongozi wa Yanga wanatakiwa kuendesha klabu kwa kufanya vitu ambavyo viko ndani ya uwezo wao tu, lakini kama ikitaka kufanya vinginevyo watajikuta wanafanya vitu vingine ambavyo haviko kwenye mipango na huenda vikawaweka kwenye maswali kutoka kwa wanachama na mashabiki wao.

Wanatakiwa wasajili wachezaji wazuri, wawalipe mishahara na posho, ili timu ifanye vema uwanjani na kwa sasa wasiwaaminishe kuwa wanaweza kufanya vitu ambavyo kwa sasa haviwezekani vinavyoweza kuwachanganya Wanayanga.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Lema ambwaga Selasini Kaskazini

**Na Enock Charles**

MBUNGE wa Arusha Mjini, Godbless Lema (pichani), amemshinda Mbunge wa Rombo, Joseph Selasini katika uchaguzi wa ndani wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kumpata Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

Leama alishinda kwa kupata kura 78 dhidi ya kura 27 alizopata Selasini. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Idara ya Habari ya chama hicho, Tumaini Makene, nafasi ya mwenyekiti wa kanda iligombewa na wabunge hao wawili, huku wakijitokeza watu wanne kwa nafasi ya Makamu

Mwenyekiti ambapo Mbunge wa Viti Maalum, Yosepher Komba, akiibuka mshindi kwa kupata kura 76 akiwabwaga wenzake watatu.

Uchaguzi katika chama hicho kikuu cha upinzani nchini ulianza Novemba 18, mwaka huu baada ya Katibu Mkuu wa chama hicho Taifa, Dk. Vincent Mashinji, kutangaza ratiba rasmi ya kuanza kwa mchakato huo ambao unatarajiwa kukamilika Desemba 18, mwaka huu kwa kumchagua Mwenyekiti wa chama hicho Taifa.

Baadhi ya kanda zimeshakamilisha mchakato wa uchaguzi huo ikiwamo Kanda ya Kusini ambapo Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe

aliangushwa na Suleiman Methew aliyejinyakulia kura 53 dhidi ya kura 31 za Mwambe, huku Salum Barwan akijinyakulia kura 53 na kuwabwaga wenzie watatu katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Kanda hiyo.Katika Kanda ya Pwani, Waziri Mkuu wa zamani, Fredrick Sumaye, alishindwa kutetea kiti chake kwa kupata kura 48 za hapana dhidi ya kura 28, huku Baraka Mwago akishinda nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa kanda hiyo na kuwabwaga wenzie




wanne katika uchaguzi huo.

Uchaguzi huo pia utaendelea kwa kuchagua viongozi katika mabaraza ya chama hicho ambapo katika Baraza la Wanawake (Wawacha), Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, ndiye pekee aliyerejesha fomu za kugombea uenyekiti wa baraza hilo, huku Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, akiwa mgombea pekee aliyejitokeza kugombea nafasi ya ukatibu mkuu wa baraza.

Kwa Upande wa Baraza la Wazee, Mwenyekiti wa baraza hilo, Hashim Juma, ndiye pekee aliyejitokeza, huku pia Mbunge wa Viti Maalum, Susan Lyimo, akijitokeza pekee kuwania nafasi ya makamu mwenyekiti wa baraza hilo.

# Mvua siku 10 mfululizo mikoa 12

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetangaza uwepo wa mvua kwa siku 10 mfululizo kwenye mikoa 12 ya Kanda ya Ziwa, Magharibi na Kaskazini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana jijini Dar es Salaam, kuhusu utabiri wa hali ya hewa hatarishi na athari zinazoweza kutokea, wananchi wa mikoa hiyo wanatakiwa kuchukua tahadhari mapema. Mikao hiyo ni Mwanza, Kagera, Geita, Kigoma, Katavi, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Mara, Tabora, Manyara na Arusha.

Taarifa hiyo ilibanisha kuwa mvua kubwa itanyesha kuanzia Desemba 3 hadi 12 kwenye mikoa hiyo, na wananchi kutakiwa kuwa makini wakati wote.

"Athari zinazoweza kujitokeza ni pamoja na baadhi ya makazi yatazungukwa na maji, ucheleweshwaji wa usafiri, kusimama kwa muda kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi na kijamii," ilifafanua taarifa hiyo.

# Asimulia alivyofukuzwa kazi kwa kukataa rushwa ya ngono

INATOKA UK. 2

kabisaa na ndipo baada ya siku chache nikapewa barua kwamba rufani yangu imetupiliwa mbali."

Pamoja na kikwazo hicho, Stella alisema hakukata tamaa na kuamua kwenda kushtaki katika vyombo mbalimbali ambavyo alikutana na hali hiyo ya kuombwa rushwa.

"Baada ya miaka miwili niliposhindwa kupata haki kote nilikozunguka, ilibidi niende Tume ya Usuluhishi na Maamuzi ambako nashukuru Mungu nilishinda na iliamua nilipwe mishahara ya miezi 12," alisema Stella.

"Nilipotafakari niliona kwamba uamuzi ule haukunisaidia sana kwa sababu haukusema nirudishwe kazini isipokuwa nilipwe mshahara wa miezi 12 tu wakati mpaka uamuzi huo unatolewa tayari nilikuwa nimekaa zaidi ya miaka mitatu nje ya kazi. Sikuridhika, libidi niende Mahakama Kuu divisheni ya kazi."

"Hivi ninavyozungumza mwaka jana mwezi wa nane nilishinda kesi, nililipwa haki zangu zote katika kipindi chote ambacho nilifukuzwa na nimerudishwa kazini."

"Nataka niwaambie wote wanaosumbuliwa na jambo hili kazini, wasikubali kutoa rushwa ya ngono kwa ajili ya kupata jambo fulani au kunyanyaswa, wajenge tabia ya kukimbilia kwenye vyombo vya sheria maana inawezekana kupata haki bila kutoa rushwa.

Hivi karibuni katika Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP-Mtandao, Lilian Liundi, alisema takwimu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) mwaka 2015/2016 zinaonyesha kuwa vitendo vya ukatili wa kingono vinaongezeka kulingana na umri.

Liundi alisema ripoti ya idadi ya watu duniani ya mwaka 2019 inaonyesha kuwa asilimia 35 ya wanawake wote duniani wamekutana na aina mbalimbali za ukatili ikiwamo udhalilishaji wa kingono katika maisha yao.

# Watendaji wakala maji kuwekwa kikaangoni

INATOKA UK. 4

(DDCA) kutekeleza miradi hiyo.

"Wizara haitatumia makandarasi ambao wanadai fedha nyingi na kuchelewesha miradi badala yake tutatumia fedha za ndani na watalaamu wa wizara kuharakisha miradi na kwa gharama nafuu," alisema.

Alisema michakato ya zabuni inachelewesha miradi kwa kuwa kisima kimoja DDCA wanauwezo wa kuchimba kwa siku tatu tofauti na michakato hiyo inayochelewesha huduma kwa wananchi.

Awali, akisoma ripoti ya utekelezaji miradi wilayani Chamwino, Kaimu Meneja wa Ruwasa Chamwino, Christina Msengi, alisema hadi Oktoba mwaka huu, watu 264,484 wanapata majisafi na salama sawa na asilimia 65 ya wakazi wote.

Aidha, alisema katika bajeti ya 2018/19, serikali ilitenga Sh. milioni 350 kwa ajili ya kujichimba visima virefu katika vijijini 14 hadi sasa mkandarasi DDCA ameshalipwa malipo ya awali ya Sh. milioni 175.1 na amechimba visima saba.

Alisema katika bajeti ya mwaka 2019/20, serikali kupitia Ruwasa Chamwino itaanza kukarabati miradi ya maji kupitia Mpango wa Malipo Kutokana na Matokeo (PbR) katika vijiji saba hivi karibuni.

Alibainisha kuwa utaratibu wa manunuzi upo katika hatua ya tathmini ya kupata wazabuni na kusambaza vifaa vya ukarabati wa miradi na itakayogharimu Sh. milioni 82.4.

Alisema watu 16,000 wa vijiji hivyo sawa na asilimia 3.9 ya wananchi wote watapata huduma ya majisafi.

"Pia mpango wa bajeti ya mwaka 2019/20, serikali imetenga Sh. milioni 660 kwa ajili ya kuboresha miradi kwa kununua pampu na mashine na kufunga katika vijiji vinne vya Chikola, Chiwondo, Ilowe na Dabalo na kuchimba visima virefu katika vijiji vya Bwawani, Ikowa, Chibwe na Mlimwa,"

# Vijana waongoza maambukizo VVU

INATOKA UK. 3

ya hao asilimia 80 ni wa kike.

"Takwimu hizi ni dhahiri kuwa kundi la vijana hasa wa kike ndiyo zinaonyesha lipo kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi... miongoni mwa sababu ni pamoja na ngono zembe katika umri mdogo, hali inayosababisha mhusika kuwa na wapenzi wengi, inayojenga hatari ya kupata maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi," alisema Mhagama.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wamejitoa kuelimisha umma hasa kwenye mikusanyiko ili kupunguza maambukizi mapya katika jamii.

Aliwasihi watu wanaoishi na virusi hivyo kuendelea kutumia dawa na wanaume kuacha kuwarubuni vijana wadogo kwa lengo la kufanya nao mapenzi.

Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema wameshusha umri wa vijana kupima maambukizi ya virusi vya Ukimwi bila kupata ridhaa ya mzazi au mlezi kutoka miaka 18 hadi miaka 15 na kuwasihi vijana kupima afya zao ili wapate kufahamu na watakaobainika kuwa na maambukizi kuanza dawa mapema.

Mkurugenzi wa Shirika la Unaids nchini Dk. Leo Zekeng, alisema mpaka sasa watu milioni 32 wamefariki dunia kutokana na ugonjwa wa Ukimwi.

Mwenyekiti wa Baraza la Watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi nchini (Nacopha), Letisia Kapela, alisema ongezeko la maambukizi ya VVU linaongoza kwa vijana walio na umri wa miaka 15 hadi 24 na kutoa tahadhari kwa vijana wanaojirahisisha kwa kinamama kupata urahisi wa maisha.

"Niwaombe acheni michepuko, kwa kuwa bila michepuko maisha hayaendi, tulia na wako tujenge taifa ambalo haina maambukizi," alisema Kapela.

"Kuwaita watu wanaoishi na virusi ya Ukimwi waathirika ni unyanyapaa wa hali ya juu, Ukimwi sio mwisho wa maisha, hakuna sababu ya sisi kujinyanyapaa, kwanza kwa sisi wenyewe na pili jamii, huu ni ugonjwa kama yalivyo magonjwa mengine," alionya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kivulini, Yasin Ally, alisema hofu ya vijana wa sasa sio Ukimwi wala magonjwa ya zinaa bali mimba na ndoa.

Yasin alisema vijana wa kiume wanatumia fursa hiyo kuwahadaa wasichana kwa kuwaahidi ndoa na kuwavalisha pete za mitego ili kufanikisha malengo yao na wengine kuwasababishia kupata maambukizi.

"Wengi wamediriki kujifungia njiti shuleni kwa ajili ya kukwepa mimba kuliko Ukimwi na magonjwa ya zinaa na wengine vijana wa vyuo vikuu kutokana na uhuru walionao hutumia 'boom' (pesa ya kujikimu) kuwarubuni watoto wa watu," alisema Yasin.

Katika takwimu za maambukizi ya virusi vya Ukimwi iliyofanyika mwaka 2016/2017 ilionyesha kuwa Mkoa wa Njombe uliongoza kwa kuwa na asilimia 11.4, ikifuatiwa na Iringa wenye asilimia 11.3, Mbeya asilimia 9.3 Mwanza asilimia 7.2 na Kagera asilimia 6.5.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni 'Jamii ni chachu ya mabadiliko tuunngane kupunguza maambukizi mapya ya VVU'.



Wafanyakazi wa Benki ya Exim tawi la Shinyanga, wakiongozwa na Meneja wa Tawi hilo, Sarah Paul (katikati), wakiwa na walimu pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mapinduzi mkoani humo, baada ya kukabidhi msaada wa taulo za kike kwa wanafunzi hao, mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Benki yasaidia taulo za kike maelfu wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu**

MAELFU ya wanafunzi wa kike wa shule za sekondari na msingi mkoani Shinyanga wamesaidiwa taulo za kike na Benki ya Exim Tanzania.

Benki hiyo imetoa taulo za kike kwa wanafunzi wa kike zaidi ya 2,400 wa shule hizo ambazo ni Shule ya Sekondari ya Kiislamu Istiqaama, Shule ya Msingi Mwenge, Shule ya Msingi Mapinduzi, Shule ya Msingi Jomu, Shule ya Msingi Ibadhi pamoja na Kituo cha Agape Aids Control Programme kilichopo mkoani humo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi msaada huo mwishoni mwa wiki, Meneja wa Benki hiyo tawi la Shinyanga, Sarah Paul, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa mpango wa uwajibikaji kwa jamii wa benki hiyo unafahamika kama Exim Cares.

Alisema benki hiyo imekuja na mpango huo ili kusaidia wanafunzi wa kike kwa kuwapatia hitaji hilo muhimu kiafya sambamba na kutoa elimu kuhusu hedhi salama kwa wanafunzi wa kike pindi wakiwa shuleni.

Kwa mujibu wa Sarah, kupitia mpango huo, benki hiyo inatarajia kutoa misaada mingine kama hiyo kwa shule kadhaa katika mikoa mingine ikiwemo Tabora na Iringa.

"Benki ya Exim inafarijika sana kuwa sehemu ya ajenda muhimu za kijamii na hiyo ni moja ya imani yetu, kwa hiyo tumeamua kuja na mpango wa kusaidia mtoto wa kike na ili kuhakikisha kwamba msaada huu unakuwa na tija zaidi taulo hizi tulizotoa zinaweza kutumika zaidi ya mara moja na itawasaidia zaidi wahusika," alisema.

Kwa mujibu wa ripoti ya Unesco, inakadiriwa kuwa msichana mmoja kati ya kumi katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara anakosa kwenda shule wakati wa mzunguko wa hedhi.

Aidha, katika baadhi ya tamaduni suala la hedhi linapewa tafsiri potofu zaidi na hivyo kuongeza changamoto kwa watoto wa kike na hivyo kuathiri maudhurio yao shuleni na hatimaye kuathiri taaluma zao.

"Benki ya Exim imejitolea kikamilifu kuhakikisha kuwa vijana wa Kitanzania wanapata elimu, licha ya changamoto zinazowakabili na hili tutalifanikisha kwa kuhakikisha tunakuwa sehemu ya kuwasaidia kuzitatua changamoto hizo na utoaji wa taulo hizi ni sehemu ya mkakati wa kukamilisha adhima hiyo," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Istiqaama, Mbaraka Songoro, alisema msaada huo si tu unaonyesha utu bali pia ni unaonyesha heshima kwa watoto wa kike.

"Sisi kama shule tunaona hii kama heshima kubwa kwa wapokeaji wa msaada huu na kwa jamii kwa ujumla. Misaada ya namna hii inaonesha namna watu na taasisi makini kama Benki ya Exim zinavyowachukulia watoto wa kike...tunashukuru sana," alisema.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wanafunzi wenzie, mwanafunzi wa kidato cha tatu, . kutoka Shule ya Sekondari Istiqaama, Fathihiya Faiz, alisema mbali na uhitaji walio nao kwa bidhaa hiyo muhimu pia wamepokea msaada huo kama ishara ya upendo na heshima kutoka kwa benki hiyo hatua ambayo itawafanya wasome wakitambua kuwa zipo taasisi na Watanzania wanaowajali na kutambua changamoto za kijinsia wanazopitia.

"Kwa msaada huu tunaamini hatutakabiliwa tena na magonjwa ambayo yanaweza kutokea kwa ukosefu wa taulo za hedhi. Pia msaada huu utaziba pengo ambalo wazazi wetu hawawezi kuliziba kwa sababu ya changamoto kadhaa zinazowakabili zikiwamo za kiuchumi," alisema.

# Walima tumbaku waipa serikali kazi ya ziada

**Na Beatrice Moses**

SERIKALI imelazimika kufanya kazi ya ziada ya kutafuta soko la tumbaku baada ya wakulima wa zao hilo nchini kuzalisha kilo 69,757,425 katika msimu uliopita, hivyo kuwa zaidi ya lengo la uzalishaji kwa mujibu wa mikataba ambao ilikuwa kilo 57,305,127.

Kutokana na hatua hiyo, serikali imepata kazi ya ziada kuhakikisha inawasaidia wakulima hao kupata soko la kilo 12,452,298 zilizozalishwa nje ya mikataba. Hayo yamebainishwa na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema tumbaku iliyonunuliwa mpaka mwisho wa msimu huo wa mwaka 2018/2019 ndani ya mikataba ni kilo 60,691,972.21 zenye thamani ya dola za Kimarekani 92,927,331.79 sawa na asilimia 105.9 ya lengo.

"Jitihada za Wizara ya Kilimo kushirikiana na Bodi ya Tumbaku zilifanikiwa kushawishi kampuni ya Alliance One na Premium Active kununua tumbaku kilo 6,305,000, kuongeza kilo toka 4,200,000 hadi 7,400,000, mpaka sasa, ununuzi wa tumbaku hiyo iliyozidi malengo ya uzalishaji umefikia kilo 8,107,221 zenye thamani ya Dola za Kimarekani 6,330,174," alisema.

Alisema tumbaku iliyobaki kwa wakulima bila mnunuzi ni kilo 3,345,077 katika mkoa wa Tabora na kiasi kidogo Ushetu Shinyanga, ununuzi umekamilika kwa 100% mkoa wa Mbeya, Songwe, Kigoma,Singida, Iringa, Ruvuma na Katavi," alisema.

Waziri alibainisha kuwa wizara yake imeendelea kuhakikisha tumbaku hiyo inanunuliwa yote toka kwa wakulima, mnamo Novemba 11, 2019 Kampuni mbili ambazo ni Copper Leaf Company na Tombwe Processing toka nchi ya Zambia, zimekubali kununua tumbaku iliyobaki kwa wakulima na tayari wamewasili nchini na wameanza kusaini mikataba kupitia vyama vya msingi vya ushirika. "Kwa hatua hiyo tatizo la uwepo wa tumbaku iliyozalishwa nje ya mkataba msimu huu kwa wakulima wa tumbaku litakuwa limekwisha kabisa. Wananchi waendelee kulima mashamba kwa msimu unaokuja," alisema.

Katika msimu wa kilimo 2019/2020 ambao masoko yake yataanza mwezi Mei 2020, kampuni za ununuzi zilizopo nchini ambazo ni Alliance One Tanzania, Premium Active Tanzania na Japan Tobacco International zimetoa mikataba ya kilo 42,225,985.

"Tayari wakulima wapatao 33,000 wameomba kusajiliwa na Bodi ya Tumbaku kutokana na uzalishaji huo, uzalishaji huo ni mdogo na hivyo unaacha wakulima takribani 16,000 bila kulima tumbaku msimu huu," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na hali hiyo wizara kupitia Bodi ya Tumbaku ilianzisha jitihada za kutafuta masoko mengine ili kuziba pengo la kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco - TLTC ambayo haijatoa makisio ya uzalishaji msimu huu. Alisema kampuni nne mpya tayari zimeonesha nia ya kununua tumbaku ya Tanzania msimu ujao. Kampuni hizo ni Magefa Growers Ltd itanunua kilo 5,500,000 Transafricque kupitia kampuni ya kizawa ya Grand Tobacco Growers Co. Ltd imeomba kununua kilo 9,000,000, Petrobena itanunua kilo 300,000 na Pachtec Ltd imeomba kununua kilo 500,000.

# Asakwa tuhuma kubaka mapacha

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, linaendelea kumsaka Issa Khalid Rashid anayetuhumiwa kuwabaka mapacha wawili wa kike huko Wingwi Wilaya ya Michweni Pemba.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Mohamed Shehan Mohamed, alisema bila ya halali mtuhumiwa huyo aliwabaka ndugu hao mapacha wenye umri wa miaka 17.

Alisema tukio hilo lilitokea kati ya Novemba 10 mwaka huu asubuhi na Novemba 14 asubuhi Wingwi Wilaya ya Micheweni.

Kamanda Shehan alisema baada ya kutenda kosa hilo, mtuhumiwa alikimbia, kuwa Jeshi la Polisi linaendelea kumsaka, na atakapopatikana atafikishwa mahakamani.

"Mtuhumiwa huyu amefanya unyama wa kuwabaka ndugu wawili mapacha, kitu ambacho kinaweza kuwaathirika kisaikolojia na kimwili, hivyo tunaendelea kumtafuta ili afikishwe mahakamani," alisema kamanda huyo.

Aliitaka jamii kuacha kuoneana aibu na kutokuwaficha wahusika yanapotokea matukio ya ukatili ili kufanikiwa kutokomeza vitendo hivyo kwa watoto.

"Uhalifu huu sana hufanywa na ndugu wa karibu na majirani, jambo ambalo linasababisha jamii kuwa na muhali, hivyo tusioneane aibu, vinapotokea vitendo hivyo turipoti kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Aidha, alieleza kuwa, ushirikiano unahitajika zaidi katika kuhakikisha jamii inakuwa mstari wa mbele kutoa ushahidi wanapoitwa kwenye vyombo vya sheria.

"Bila ya ushahidi huwezi tu kumtia hatiani mtuhumiwa, kuna baadhi ya wanajamii wanakuwa wagumu kutoa ushahidi, baadaye wanakaa na kusema hakuna hukumu inayotolewa, hivyo tushirikiane," alieleza kamanda hiyo.

Pia aliitaka jamii kuwa makini kwa watoto wao sambamba na kuwafuatilia nyendo zao, jambo ambalo litasaidia kudhibiti vitendo hivyo.

Kubaka ni kosa kisheria kinyume na kifungu cha 113 (1) (a) cha Sheria ya adhabu, Sheria namba 6 ya mwaka 2018 ya Zanzibar.

## Marufuku uchimbaji wa mchanga Bunju

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imepiga marufuku utupaji wa taka na uchimbaji mchanga kwenye Mto Nyakasangwa uliopo eneo la Bunju jijini Dar es Salaam, kwa kuwa hatua hiyo imechangia uharibifu na uchafuzi wa mazingira.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki katika eneo hilo, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Joseph Malongo akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alipiga marufuku ya shughuli zote hapo ikiwamo utupaji taka na uchimbaji mchanga.

"Shughuli zilizokuwa zikiendelea eneo hili zimechangia uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwani zinakiuka sheria na kanuni za mazingira, hivyo serikali inapiga marufuku shughuli zote ambazo zilikuwa zikifanywa hapa," alisema.

Mhandisi Malongo aliziagiza mamlaka za serikali za mitaa kote nchini kuhakikisha hakuna shughuli zozote za kiuchumi zinazofanywa kwenye vyanzo vya mito ndani ya mita 60 na ambazo hazina kibali kutoka kwa

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). "Naagiza Mamlaka za serikali za mitaa kote nchini kusimamia mazingira kwa mujibu wa sheria na kuwachukulia hatua kali wale wote watakaokiuka kanuni na taratibu zinazongoza katika kusimamia mazingira," alisema Mhandisi Malongo.

Mhandisi Malongo alisema wanazo taarifa za uwapo wa taasisi na watu binafsi ambao wamekuwa wakitupa taka katika eneo hilo la Mto Nyakasangwa, hivyo wamejipanga kuimarisha ulinzi.

"Tunachukua hatua kuanzia sasa ambapo nimemwagiza Mkurugenzi mkuu wa NEMC kuwachukulia hatua mara moja viongozi wa serikali ya mtaa huu wa Boko kwa kufumbia macho uchafuzi uliokuwa unafanywa na pia Jeshi letu la Polisi litaimarisha ulinzi katika eneo hili ili kuzuia uchimbaji wa mchanga na utupaji wa taka eneo hili," alisisitiza.

Kwa upande wake, Dk. Gwamaka alisema baraza lake litaendelea kuchukua hatua kali na za kisheria dhidi ya watu wanaoharibu mazingira ikiwamo utupaji taka kwenye kingo za mito yote nchini.

"Tutaendelea kuchukua hatua kwa watu na taasisi ambazo zimekuwa zikifumbia macho utunzaji wa mazingira kwa kutumia kanuni na sheria zilizopo ili kuyalinda mazingira kwa faida vizazi vijavyo," alisema.

Aidha, Dk. Gwamaka alikemea tabia ya baadhi ya watendaji wa kata, kitongoji na mtaa wasiowaaminifu kushirikiana na watu au taasisi kutupa taka na kuchimba mchanga kwa manufaa yao binafsi.

# Magunia yakwamisha korosho kwenda minadani

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

SERIKALI imeombwa kuingilia kati suala la tatizo la ukosefu wa magunia ya kuhifadhia korosho za wakulima wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Korosho nyingi za wakulima bado zipo majumbani, na zinashindwa kupelekwa katika minada kutokana na tatizo hilo.

Hayo yalisemwa na madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwenye kikao chao kwamba korosho nyingi bado zipo majumbani kwa wakulima, na zimehifadhiwa sakafuni na kwamba zinashindwa kukusanywa na kupelekwa katika minada inayofanyika kutokana na uhaba wa magunia.

Walisema hata idadi ya korosho zilizouzwa kwenye minada na zilizopo kwa wakulima kwa kukosa magunia idadi kubwa zile ambazo zimekwama kwa kukosa magunia ya kuhifadhia.

Musa Msanga, Diwani wa Lulindi, alisema wanaiomba serikali kuingilia kati suala la uhaba wa magunia.

Alisema korosho bado zipo kwa wakulima na wengi wanashindwa kupeleka korosho zao katika minada kwa sababu hawana magunia.

Naye diwani wa Lupaso alisema tatizo hilo la uhaba wa magunia katika chama kikuu cha wakulima Masasi-Masasi (MAMCU) zinaweza kufanya korosho nyingi za wakulima zikabaki bila ya kuuzwa na minada ikawa imefungwa.

Alisema serikali ichukuwe hatua za masukudi kuingilia kati na kutafutia ufumbuzi tatizo hili ambalo limekuwa kero kwa wakulima.

Naye Diwani wa Nangoo, Mohammed Chilumba, alisema kila mwaka tatizo la uhaba wa magunia limekuwa likijitokeza, hivyo kufanya korosho nyingi kushindwa kuingia katika minada mpaka minada inafungwa korosho inakuwa bado zipo kwa wakulima bila kuuzwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Masasi, Juma Satma, alisema inashangaza kuona kila mwaka kunakuwa na tatizo la uhaba wa magunia.

Alisema mkulima mtaji wake ni korosho hivyo anavyoshindwa kuuza korosho zake kwa sababu ya uhaba wa vifungashio vya kuhifadhia korosho zao inashangaza.

"Tunaiomba serikali hasa wizara husika kuingilia kati tatizo hili la magunia kwani wakulima wengi korosho wameziweka majumbani kwao baada ya kukosa magunia ya kuwekea," alisema Satma.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Alfred Francis, alisema alithibitisha kuwa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Mtwara-Masasi (MAMCU) kina uhaba wa magunia. Hata hivyo, Francis alisema tatizo hili bado wanalishughulikia na litakwisha siku chache zijazo.



Meneja Chapa na Mawasiliano wa NBC, David Raymond (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika hafla ya kuchangisha fedha kwa njia ya vichekesho na burudani iitwayo 'Cheka Nisome' iliyodhaminiwa na NBC yenye lengo la kuwasaidia wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na masomo kutokana na kushindwa kumudu gharama za ada. Hafla hiyo ilifanyika chuoni hapo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Hafla hii iliratibiwa na Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DARUSO). **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# 'Watoto wenye ulemavu wasifichwe nyumbani'

**Na Enock Charles**

WAZAZI wametakiwa kutokuwaficha nyumbani watoto wenye ulemavu wa aina mbalimbali bali kuwatafutia msaada wa kuwawezesha kutimiza ndoto zao katika maisha kama watoto wengine wasiokuwa na ulemavu.

Akizungumza katika mahafali ya wanafunzi wa chekechea katika kituo cha Furaha jijini Dar es Salaam juzi, Katibu wa Tawi la Chama cha Wanawake

Wakristo Duniani (YWCA) la jijini Dar es Salaam, Monica Kimaro, alisema ni makosa kwa wazazi waliojifungua watoto wenye ulemavu kuwaficha majumbani kwa kuwa upo uwezekano wa kuwasaidia na kufanikisha malengo yao katika maisha.

"Watoto wenye ulemavu wana malengo na matarajio katika maisha kama ilivyo kwa watoto wengine kuna watoto walioletwa hapa wenye ulemavu

miaka mingi leo ni mawaziri, wengine wakuu wa wilaya na viongozi wengine wakubwa tu serikalini," alisema Kimaro.

Akizungumzia kuhusu mikakati ya kukiendeleza kituo hicho amesema mpaka sasa ipo mikakati ya kufungua matawi ya kituo hicho nchi nzima ili kuwasaidia watoto wenye ulemavu katika maeneo mbalimbali nchini.

"Tuna fund rising ambayo ni ya dunia nzima na mwezi uliopita tulikuwa nchini Northerland ambao wameahidi kutusaidia kujenga kituo cha watoto wenye ulemavu wa akili na viungo ambacho kitachukua watoto takriban 200 na tumeshanunua shamba eneo la kiluvya ambapo kutajengwa kituo Hicho," alisema.

Mwanachama mkongwe wa tawi hilo, Doroth Steven, alisema tangu kuanza kwa tawi la chama hicho jijini Dar es Salaam miaka zaidi ya hamsini iliyopita limekuwa msaada na kimbilio kwa watu wenye ulemavu na kuwaomba wazazi wenye watoto walio na ulemavu wa aina mbalimbali

kuwapeleka kituo hapo ili wapatiwe malezi bora ya kimwili na kiroho.

"Kituo hiki kwa Tanzania kimeanza mwaka 1959 na tawi hili ni tawi mama ingawa tawi la kwanza lilianzishwa Kilimanjaro na la pili likawa hapa na haya ni mahafali ya 58 na tatizo kubwa tulililoliona ni kuwa jamii yetu inaficha watoto wenye ulemavu na sisi tulianzisha kituo hiki ili kiwe msaada kwa watoto wenye ulemavu," alisema Doroth.

Mwanachama huyo aliomba serikali kwa kushirikiana na wadau kuongeza vituo vingi zaidi ili kuwasiadia watoto wengi walio na ulemavu pamoja na kusaidia katika kuhamasisha jamii kutokuwaficha ndani watoto wenye ulemavu kutokana na mila na desturi potofu.

# DC atoa onyo kwa wapambe wa wagombea

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Zephania Chaula, amewapa onyo wapambe wa wagombea udiwani na ubunge kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanaoanza kampeni kabla ya muda na kuwa na makundi.

Alisema atayasambaratisha au kukata majina yote ya wagombea wanaoanza kampeni hizo.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye Kata ya Naisinyai, wakati wa kuapishwa kwa wajumbe wa serikali za vijiji na wenyeviti wa vijiji na vitongoji.

Alisema akigundua majina ya watu wanaoanza upambe wa kupigia kampeni wagombea wa udiwani au ubunge kwenye uchaguzi wa mwakani atawaita kwenye kamati ya usalama ya wilaya.

“Nina kamati yangu ya wilaya ya kuangalia ulinzi na usalama sasa tukisikia unasababisha chokochoko kwenye wilaya yetu tutakuita ujieleze kwa nini unarudisha maendeleo nyuma sababu ya minyukano,” alionya Chaula.

Alisema mwaka huu wamewasambaratisha wote waliokuwa na makundi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kupitia CCM na ndivyo watakavyofanya kwa wagombea udiwani na ubunge.

“Mtu anaona njia pekee ya kupata udiwani au ubunge kwenye uchaguzi mkuu mwakani ni kuunda makundi, tunachotaka sisi ni kuwa na mgombea wetu ambaye ni CCM, mambo ya mgombea yanakuja baadaye,” alisema Chaula. Alisema wanaoanza kuunda makundi hivi sasa kwenye CCM wanawaharibia wagombea wao kwa kuwa majina yao yatakatwa kama walivyoyakata kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa.

Diwani wa Kata ya Naisinyai, Kilemp Ole Kinoka alipongeza jitihada za uongozi thabiti unaofanywa na mkuu huyo wa wilaya, katika kusimamia wananchi.

Kinoka alisema wanatambua kazi ya uongozi ni ngumu na inahitajika ushupavu, lakini mkuu huyo wa wilaya amesimama kidete katika uongozi wa eneo hilo la Simanjiro.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Naisinyai, Merika Makeseni aliwashukuru wananchi wa kijiji hicho kwa kumpa heshima kubwa ya yeye kuwa kiongozi wao.

“Tangu kwenye kura za maoni ya CCM hakukuwa na mgombea ambaye alichukua fomu ya kugombea nafasi hiyo hivyo anatoa ahadi ya utumishi uliotukuka ili kulipia hayo,” alisema Makeseni.

Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, Taiko Laizer, aliwashukuru wananchi wa eneo hilo kwa ushirikiano mkubwa waliompatia kwenye kipindi cha uongozi wake hadi kufikia hatua hiyo.



Askofu wa Kanisa la Roho Mtakatifu wa Kanda ya Kaskazini, Boaz Ambonya (katikati), akizungumza baada ya kusimikwa kushika nafasi hiyo Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# Familia ya bilionea Msuya kutafuta suluhu nje mahakama

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

FAMILIA mbili za marehemu bilionea Erasto Msuya mwishoni mwa wiki zilifika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ili kuondoa kesi ya mirathi kutafuta suluhu nje ya mahakama ya mgogoro wa mali uliodumu kwa miaka takribani sita tangu kifo chake.

Upande wa baba wa marehemu ukiongozwa na mama wa marehemu, Ndeshu Msuya na upande wa mke ukiongozwa na Steven Mbazi, umefika mahakamani hapo na kushindwa kuondoa kesi hiyo, kutokana na Jaji kutokuwapo na kupanga kuisikiliza Desemba 13, mwaka huu.

Maazimio hayo yanakuja baada ya Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro kukaa katika kikao cha pamoja kuomba familia hiyo kuondoa kesi mahakamani ili wayamalize nje ya mahakama.

Mama wa marehemu, baada ya kuahirishwa kesi hiyo, alisema hawapo tayari kuondoa kesi mahakamani hapo, bali kinachofanyika ni kusimamisha kesi kwa muda ili kufanya mazungumzo nje ya mahakama. Alisema hakubaliani na mali za marehemu mtoto wake kusimamiwa na ndugu wa upande wa mke ambao wamejimilikisha sehemu ya mali hizo ikiwamo hoteli ya kitalii ya SG Rezot.

Awali mtoto mkubwa wa marehemu, Kelvin Msuya, alimwomba bibi yake kuridhia kesi hiyo kuondolewa na kukaa meza moja na kwamba yupo tayari kwa mazungumzo na upande wa wazazi wa baba yake.

“Nawaomba ndugu zangu hawa wawe na upendo na mama yangu anayesota gerezani kwa kesi ya mauaji kama ambavyo wanavyodai wanaupendo naye,” alisema.

Awali, mjomba wa Kelvin, Mbazi Mrita, aliomba serikali kuingilia kati mgogoro huo na kuondoa kesi hiyo mahakamani kama walivyo shauriwa na Mkuu wa Wilaya.

Alisema kwamba awali mama wa Msuya alikubaliana wamalize mgogoro huo kwa kuwa ukimalizika litakua jambo jema la kuanza mwanzo mzuri wa kusimamia mali za marehemu.

Kesi hiyo imeahirishwa mwishoni mwa wiki katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha na Msajili Msaidizi wa Mahakama John Fransis Nkwabi hadi Desemba 13 mwaka huu, itakaposikilizwa na kujua hatima yake.

# Adai binti wa miaka 14 kuwekwa kinyumba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKAZI wa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Khadija Mtoro, ameiomba serikali mkoani Kilimanjaro kufuatilia taarifa za kupotea kwa binti yake, mwanafunzi wa kidato cha kwanza ambaye anahisiwa kuwekwa kinyumba na mwanaume.

Alisema kuwa binti yake Zaituni Sheshe (14), alikuwa anasoma kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Langoni mjini Moshi na alipotea Septemba mwaka huu hadi sasa hajaonekana.

Alisema binti huyo alikuwa anaishi na bibi yake, lakini amepotea katika mazingira ya kutatanisha na kusababisha kuwe na hisia za kuozeshwa.

Alisema baadhi ya majirani wamemweleza bibi yake huwa ana kawaida ya kuwaozesha mabinti za watu kwa wanaume ili apate fedha.

Aliomba serikali kuingilia kati suala hilo ili mtoto huyo apatikane na kwenda shule.

“Mwanaume anayedaiwa kumuweka kinyumba binti yangu naomba achukuliwe hatua kali za kisheria,” alisema.

“Hivi sasa serikali ya Rais John Magufuli inatoa kipaumbele kwa watoto kupatiwa elimu hivyo naiomba serikali ichukue hatua kwa kuchunguza jambo hili ili kubaini ukweli,” alisema Mtoro.

Alisema japokuwa bibi wa binti alitoa taarifa polisi ya kupotea kwa mtoto huyo, lakini ufuatiliaji ni mdogo hadi kutoa hofu kuwa anahusika kwenye tukio la uozeshaji wa mwanafunzi huyo.

“Mimi sikuwa na taarifa kuwa huyo bibi ana tabia za kuozesha mabinti za watu hadi majirani waliponieleza kuwa wanahisi anahusika ndiyo nikawa na wasiwasi juu ya mtoto wangu ambaye ni mwanafunzi,” alisema Mtoro.

Mume wa Mtoro, Omary Janja, alisema wana masikitiko makubwa juu ya taarifa ya kupotea kwa binti huyo ambaye alikuwa na ndoto za kupata elimu na sasa inahisiwa amewekwa kinyumba.

“Tunaiomba serikali ichukue hatua kwa wahusika wote ili kama amewekwa kinyumba mhusika akamatwe na kufikishwa kituo cha polisi kisha mahakamani,” alisema Janja.

## Wahitimu wapewa vitendea kazi wajiajiri

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAHITIMU wa Chuo cha Ufundi Ghona kilichopo Wilaya ya Moshi, wameaswa kuanzisha viwanda vidogo vidogo kupitia vifaa walivyokabidhiwa ili waanzishe miradi yao ya kiuchumi.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Childreach Tanzania, Martha Lyimo, wakati wa mahafali ya nne chuoni humo.

Aidha, aliwakabidhi wahitimu hao wenye ulemavu wa usikivu vyerehani na vifaa vya useremala kwa ajili ya kuwawezesha kujitegemea.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Miradi ya Childreach Tanzania, Winfrida Kway, alisema watu wenye ulemavu wanakabliwa na changamoto ya ubaguzi miongoni mwa jamii, jambo linalowakatisha tamaa.

"Kutokana na ukosefu wa elimu miongoni mwa jamii zetu tumejikuta wengi wanabaguliwa, kutengwa na kukataliwa kutokana na ulemavu wao, Childreach Tanzania imeona ili kutokomeza vitendo hivyo hasa nyakati za kutafuta ajira imechukua jukumu la kuwapa vitendea kazi ili kuweza kujiajiri," alisema.

Kway alisema shirika limeweza kutekeleza miradi mbalimbali ndani ya chuo hicho kwa kushirikiana na serikali pamoja na wana jamii ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha kufikia malengo endelevu na Sera ya Taifa ya Maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu ya mwaka 2003.

"Mwaka 2017 hadi mwaka 2019 Shirika la Childreach... Tanzania kupitia mradi wake wa mafunzo kwa vitendo limeweza kuwafikia jumla ya wanafunzi 23 kwa kuwawezesha vifaa mbalimbali kama vile vyerehani, vitambaa vya kushonea nguo na vifaa vya useremala, ikiwa ni pamoja na mahitaji mengine yote muhimu," alisema na kuongeza. "Wanafunzi wa fani ya useremala hupewa nyenzo zote muhimu za kuweza kujiajiri pindi wanaporudi majumbani, pamoja na wale wa fani za hupewa vyerehani na vitambaa."

Aidha, alisema Childreach Tanzania pia imeweza kujenga miradi mbalimbali ikiwemo utengenezaji wa darasa kwa ajili ya kusomea na mafunzo ya vitendo, uboreshaji wa vyoo, ili kuwawezesha wanafunzi kuwa na miundombinu mizuri ya kiafya ili kuweza kunguza magonjwa ya mlipuko.

Miradi mingine ni uchimbaji wa kisima cha maji, ili kuwawezesha upatikanaji wa maji shuleni kwa matumizi mbalimbali, mradi wa duka, mradi wa mbuzi, mradi wa ng'ombe wa maziwa na mradi wa ufugaji wa kuku. Kwa upande wake mgeni rasmi katika mahafali hayo, Ofisa Elimu Ufundi Halmashauri ya Moshi, Ladislaus Tilya, alisema endapo wahitimu hao watatumia vyema taaluma na vifaa walivyopewa watajiajiri na kuajiri wengine.

Awali, akitoa taarifa ya maendeleo ya chuo, Mkuu wa Chuo hicho, Aminiel Mwanga, alieleza kuwa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho mwaka 2010 na umoja wa wazazi wenye watoto walemavu Kanda ya Kaskazini (UWAVIKA), wanafunzi hao wamefaidika na mafunzo mbalimbali, ambayo yamekuwa yakitolewa chuoni hapo.

"Lengo la kuanzishwa kwa kituo hiki ni kuwasaidia watoto viziwi ambao wanamaliza elimu ya msingi na hawakupata nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari na waliohitimu elimu ya sekondari na hawakupata mahali pa kujifunza stadi mbalimbali za kiufundi zitakazowasaidia kujitegemea wao wenyewe," alisema.

# Kwieco yawanoa wadau uchaguzi mkuu

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

VUGUVUGU la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (Tapo) limewaleta pamoja wataalamu kutoka asasi zisizo za kiserikali mkoani Kilimanjaro kujadili mchakato wa uchaguzi mkuu na utekelezaji wake.

Viguvugu hilo lenye mtazamo wa ufeministi likiwa na lengo la kuweka sauti za makundi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki kwenye maamuzi na uongozi katika uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Mkakati huo unatekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Kwieco kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania (WFT), chini ya mradi wa ujenzi wa nguvu ya pamoja kutetea wanawake na watoto kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mwezeshaji wa mafunzo ya kuhamasisha uelewa na kujenga uwezo kwa wadau, Asseny Muro, jana alieleza namna ufeministi unavyoingia katika ujenzi wa vuguvugu la ukombozi wa mwanamke kimapinduzi kwenye ngazi ya mtu binafsi kwa mtizamo, imani na itikadi.

"Kwa kuwa ufeministi unabomoa mawazo mgando na unatambua mchango wa wanawake kimapinduzi, ujenzi wa Tapo ni mchakato wa muda mrefu, unahitaji uwekezaji na maeneo ya kuwekeza ni wahusika au wadau wote waelewe ajenda na umiliki," alisema.

Mratibu wa mradi wa Kwieco, Veronika Ullomi, akizungumza kabla ya mafunzo hayo alisema malengo mahusus ya Tapo ni kukuza uelewa na utambuzi wa kada hiyo ya umuhimu wa ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwenye maamuzi na uongozi.

"Nia yetu ni kujenga uelewa wa pamoja wa dhana muhimu za kijinsia zikihusishwa na maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, lakini kuhamasisha jamii na kukuza uelewa wao juu ya dhana na itikadi ya ufeministi kama dhana ya kufikia usawa wa kijinsia," alieleza Ullomi.

Mpaka wadau walioshirikishwa juu ya vuguvugu hilo ni viongozi wa timu za ufeministi ngazi za wilaya, wanawake mashuhuri kila wilaya, viongozi wanawake kwenye taasisi za dini ngazi ya mkoa, wanawake wasaidizi wa kisheria kila wilaya na waandishi wa habari wanawake.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Mchungaji Geneveve Manaseh wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini, alisema faida anayoiona katika vuguvugu hilo ni kuwapo kwa mshikamano wa dhati wa kuleta mabadiliko ya muda mrefu, huku ukijumuisha rasilimali watu na mali.



Mwezeshaji wa mafunzo juu ya ujenzi wa harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi na ushawishi kwa ajili ya kufikia usawa wa kijinsia na haki za binadamu ngazi ya jamii, Asseny Muro, akiwa na wanaharakati wa Mkoa wa Kilimanjaro juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Viongozi S/Mitaa Hai wapewa somo

**Na Mary Mosha,** HAI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kimewataka viongozi wa serikali za vijiji, mitaa na vitongoji kujiepusha na migogoro ikiwamo kupokea rushwa.

Katibu wa CCM wilaya hiyo, Lawrence Kumotola, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye mkutano wa serikali ya kitongoji cha Gezaulole.

Alisema viongozi hao wana umuhimu mkubwa kutokana na kuwa karibu na wananchi wao, hivyo wanapaswa wawe watu makini wenye utu na wasiopenda rushwa.

"Unapokuwa kiongozi lazima utetee maslahi ya wananchi wako na usiwe sehemu ya migogoro, pia unatakiwa kuzitambua changamoto zinazowakabili wananchi wako," alisema na kuongeza:

"Mwenyekiti wa eneo hili unatakiwa kuwa imara katika kusimamia soko la Gezaulole linajengwa vizuri ili wafanyabiashara hawa waweze kufanya biashara zao na wajipatie ridhiki yao bila bughudha."

Mwenyekiti wa Kitogoji cha Gezaulole, Fadhil Ngazi, alisema yupo tayari kushirikiana na wananchi pamoja na viongozi wengine katika kutetea maslai ya Taifa.

Aidha, alibainisha changamoto zilizopo katika kijiji hicho ambazo ni soko, uporwaji wa ardhi, kutokusomewa taarifa za mapato na matumizi pamoja na wananchi kuchangishwa michango bila kupatiwa risiti za EFD.

NIPASHE JUMATATU DESEMBA 2, 2019

Nipashe

# Spotika



WA3 WANAOSUBIRI UPEPO WA KISULISULI JANUARI 2020 UK. 20




# HAIKAMATIKI

Beki Mholanzi wa Liverpool, Virgil van Dijk, akishangilia baada ya kuifungia timu yake mabao yote mawili katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Brighton & Hove Albion iliyochezwa juzi usiku, kwenye Uwanja wa Anfield jijini London. Liverpool ilishinda mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

Straika Zlatan Ibrahimovic ambaye amejiunga na Hammarby akitokea LA Galaxy, rasmi naye amekuwa ni mmoja wa wamiliki wa klabu hiyo kongwe nchini Sweden. Hata hivyo haijathibitishwa kuwa nyota huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Sweden atastaafu kucheza kandanda akiwa na klabu hiyo.



SOKA



# MAKOCHA WA4 WALIOKALIA KUTI KAVU EPL KWA SASA

**LONDON, England**

MSIMU wa Ligi Kuu England unazidi kushika kasi, huku hadi sasa mechi 13 zimechezwa na timu zipo kwenye nafasi zao (kabla ya mechi za juzi Jumamosi na jana Jumapili).

Liverpool na Manchester City walitarajiwa kuwa kwenye mbio moja, lakini tofauti na matarajio ya wengi kikosi cha Jurgen Klopp kimewaacha vijana wa pale Etihad kwa tofauti ya pointi nane, na nafasi ya pili wakiwa Leicester City wanaonolewa na kocha, Brendan Rodgers.

Leicester pamoja na Sheffield United, wamefanya kile kisichotarajiwa na wengi na kujikuta wakiwa na kiwango cha kuvutia zaidi.

Leicester kwa sasa inashika nafasi ya pili kwenye msimamo baada ya mechi 13.

Manchester United na Arsenal, klabu kubwa mbili zilizokuwa na mafanikio chini ya makocha, Sir Alex Ferguson na Arsene Wenger, sasa zimeachwa nje kabisa ya nne bora.

Tottenham Hotspur, nayo imekuwa kwenye wakati mgumu kwa mwanzo mbaya na baadae wakaamua kuachana na kocha, Mauricio Pochettino na nafasi yake ikichukuliwa na Jose Mourinho.

Katika soka, timu ikiwa na matokeo mabaya, kocha ndio mtu wa kwanza kubeba msalaba, sasa wakati tayari makocha kadhaa wameshatimuliwa akiwamo Unai Emery wa Arsenal, hapa tunawaangalia makocha wanne waliokalia kuti kavu kwenye Ligi Kuu England maarufu EPL.

**4. Ralph Hasenhuttl - Southampton**

Tangu alivyochukua mikoa kutoka kwa Mark Hughes, Desemba mwaka jana, Ralph Hasenhuttl, ameshindwa kuiweka Southampton kwenye ramani nzuri. Sasa klabu hiyo imejikuta yenyewe kwenye hatari ya kushuka daraja, ikiwa imepata pointi tisa tu katika mechi 13.

Southampton haijashinda mchezo wowote kati ya mechi tano zilizopita kwenye Ligi Kuu, ikiwamo kichapo cha mabao 9-0 kutoka kwa Leicester City wakiwa nyumbani na sasa kocha huyo raia wa Austria yupo kwenye hatari ya kufukuzwa.

Tangu hapo, kikosi hicho kimepambana na kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Emirates, lakini Hasenhuttl anaweza kuwa kocha anayefuatia kufukuzwa kwenye ligi hiyo, kama matokeo yataendelea kuwa hivyo, huku Southampton wakiwa kwenye hatari ya kushuka daraja.

**3. Manuel Pellegrini - West Ham United**

Ingawa West Ham walianza vizuri msimu na walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Manchester United Oktoba mwaka huu. Tangu hapo kikosi hicho cha kocha, Manuel Pellegrini kimeshindwa kushinda mchezo wowote kwenye Ligi Kuu na kujikuta kikiwa na matokeo mabaya kila wiki.

West Ham iliimarisha kikosi chake kwa kutumia fedha nyingi kuwasajili Pablo Fornals na Sebastien Haller kipindi cha majira ya joto, lakini wameshindwa kufikia kile walichokiacha msimu uliopita na sasa bila shaka nafasi ya Pellegrini klabuni hapo ipo shakani.

Wagonga nyundo hao wa jiji la London kwa sasa wamejikuta wakiwa juu kwa pointi tatu tu kutoka mstari wa kushuka daraja wakiwa nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Pellegrini ni mshindi wa taji la Ligi Kuu England akiwa na Manchester City, lakini West Ham wanaweza kuachana nae ndani ya wiki chache zijazo, kama matokeo ya klabu hiyo hayatabadilika.

**2. Marco Silva - Everton**

Nafasi ya Marco Silva pale Everton ipo shakani hasa katika wiki za hivi karibuni, wakati Toffees hao wakijikuta wenyewe wakiwa nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi baada ya mechi 13. Klabu hiyo ya pale Merseyside ilifanya kazi nzuri kwenye dirisha la usajili ikiwa moja ya timu 6 zilizotumia kiasi cha pauni milioni 100 kwenye usajili, wakiwa kwenye harakati za kufuzu kwenye Ligi ya Europa.

Ni Norwich City na Watford pekee ndio zilizopoteza mechi nyingi zaidi kuliko Everton msimu huu.

Katika wiki za hivi karibuni, mashabiki na wachambuzi wa soka, wamepaza sauti zao kutaka kocha huyo raia wa Ureno kuondoka klabuni hapo. Muda unaonekana kwenda kwa kasi zaidi kwa kocha huyo wa zamani wa Hull City na kama matokeo yataendelea kuwa mabaya, kuna uwezekano mkubwa nafasi ya Silva akapewa mtu mwingine ndani ya siku chache zijazo.

**1 Ole Gunnar Solskjaer - United**


Manchester United imeanza msimu wa Ligi Kuu vibaya zaidi, licha ya kuwa moja ya klabu iliyotumia fedha nyingi kwenye usajili wa kipindi cha majira ya joto na sasa kocha, Ole Gunnar Solskjaer anaoneka wazi kwamba amekalia kuti kavu. Raia huyo wa Norway alionekana kuwa kwenye nafasi nzuri wakati alipochukua mikoba ya Jose Mourinho, lakini tangu alipopewa mkataba wa kudumu, matokeo ya timu hiyo yamekuwa sio ya kuridhisha.

United walikuwa na nafasi nzuri katikati ya wiki iliyopita, wakati walipotoka nyuma ya mabao mawili dhidi ya Sheffield United na kuongoza 3-0 pale kwenye dimba la Bramall Lane. Lakini Blades hao wakafanikiwa kulazimisha sare ya 3-3 wakati Oliver McBurnie alipofunga dakika ya mwisho. Kwa kiasi kikubwa matokeo ya United yamekuwa sio ya kuvutia, huku pia wakitoka kuchapwa mabao 2-1 kwenye Ligi ya Europa Alhamisi iliyopita.

Kocha Mauricio Pochettino kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na mpango wa kuchukua nafasi katika kikosi cha Manchester United na tangu raia huyo wa Argentina afukuzwe pale Tottenham Hotspurs wiki iliyopita, kibarua cha Solskjaer kinaweza kuwa kwenye wakati mgumu zaidi kwa wiki zinazokuja.

Kwa sasa United inashika nafasi ya tisa ikipitwa pointi 9 nyuma ya Chelsea iliyopo nafasi ya nne.

**JE, WAJUA?**



Golikipa wa Liverpool, Alisson ataukosa mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya mahasimu wao, Everton utakaochezwa Jumatano baada ya kuonyeshwa kadi nyekundu juzi usiku. Refa Martin Atkinson alimtoa nje Mbrazil huyo katika mechi waliyoshinda mabao 2-1 dhidi ya Brighton baada ya kudakia mpira nje ya eneo la 18.

# MICHEZO




Mchezaji bora wa michuano ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake, Mwanahamisi Omari 'Gaucho' wa Kilimanjaro Queens, (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa Kenya, wakati wa mechi ya fainali ya michuano hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex. Kenya ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MAKTABA.**

# WACHEZAJI 11 WALIOTISHA CHALENJI WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

MICHUANO ya Kombe la Chalenji kwa Wanawake kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, ilimalizika Jumatatu iliyopita (Novemba 25, mwaka huu), kwenye Uwanja wa Azam Complex Chamazi jijini, Dar es Salaam kwa Kenya kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza.

Kenya ilibuka kidedea baada ya kuwafunga wenyeji Kilimanjaro Queens ya Tanzania Bara, mabao 2-0 katika mechi ya fainali.

Ni michuano iliyokuwa na msisimko wa aina yake, mashabiki wakijazana kwa wingi tangu ilipoanza kutimua vumbi Novemba 16, mwaka huu, mechi zote zikichezwa kwenye uwanja huo huo.

Jumla ya michezo 16 ilichezwa hadi fainali, ikishuhudia magoli 85 yakifungwa hadi kumalizika kwa michuano hiyo.

Hat-trick saba zimepigwa na wachezaji mbalimbali kwenye michuano hiyo, wakati penalti sita zilipatikana.

Mabingwa wapya Kenya, ndiyo timu iliyoondoka bila kufungwa hata goli moja, huku Zanzibar na Djibouti zikiwa zimeondoka kwenye michuano hiyo bila goli lolote.

Baada ya michuano hiyo kumalizika, mwandishi wa makala haya amekusanya majina ya wachezaji 11 bora walioonekana kufanya vizuri kwenye michuano hiyo na kustahili kuunda kombaini ya Afrika Mashariki na Kati (Cecafa).

**1. Annedy Andey-Kenya**

Ndiye kipa bora wa michuano hiyo mwaka huu. Mpaka michuano hiyo inamalizika na kuiwezesha timu yake kutwaa ubingwa hajaruhusu wavu wake kuguswa.

Ni golikipa wa viwango vya juu, kwani ukianzia umbo ni mrefu, ana nguvu mikononi kiasi cha kudaka mashuti makali bila kutema, kitu ambacho kinawashinda makipa wengi wa kike.

**2. Happyness Mwaipaja-Kili Queens**

Ni beki wa kulia wa Kilimanjaro Queens, aliyecheza vema sana kwenye michuano hiyo iliyomalizika na anastahili kuwamo kwenye kikosi hiki, licha ya kasoro ndogo kwenye mechi ya fainali kushindwa kumkaba vema mchezaji hatari wa Kenya, Jentrix Shikangwa na kusababisha magoli yote mawili yaliyotokea upande wake.

**3. Nally Sawe-Kenya**

Beki huyu wa kushoto ameonyesha uwezo wa hali ya juu akiwa mgumu kupitika, mwenye uwezo na nguvu na akili ambazo zimeifanya beki wa Kenya kutopitika ovyo.

**4. Amina Ally- Kili Queens**

Beki wa kati maridadi kabisa anayecheza kwa kutumia akili zaidi kuliko nguvu. Ana "kontroo" ya hali ya juu na uwezo wa kumiliki mpira, kutoa pasi za uhakika kiasi cha mashabiki wengi kumshangilia kila anapochukua mpira.

Wengine wanadai angechezeshwa namba nane kutokana na uwezo alionao.

**5. Dorcus Nixon-Kenya**

Moja ya faida ya wachezaji wa Kenya ni warefu na wana fikizi ya hali ya juu, hasa mabeki.

Dorcus ni mmoja wa mabeki wa kati ya Kenya mrefu na mwenye nguvu, pia ndiye kapteni wa timu hiyo ambaye kwa kiasi kikubwa alichangia kuifanya timu isiyofungika hadi kutwaa ubingwa.

**6. Aquino Corazole-Kenya**

Huyu dada ni mkata umeme kweli. Ni mrefu, mbishi, asiyependa masihara wala mzaha hata kidogo awapo uwanjani, ingawa ndiye aliyekuwa kinara wa kuselebuka muziki baada ya kutwaa kombe. Nguvu alizokuwa nazo, ziliwaweka salama mabeki wake na kipa kwa kupambana na mastraika wa timu pinzani na kuwapunguza nguvu kabla ya kuwafikia ukuta wa timu yake.

**7. Mwanalima Jereko-Kenya**

Huwezi kumtofautisha sana na Mwanahamisi Omari jinsi ya uchezaji wake, wakati mwingine hata wajihi.

Ni mchezaji mwenye ufundi wa hali ya juu mguuni, anayeweza kupiga chenga za kunyanyasa, mbio na kuweza kufanya chochote muda wowote.

Ndiye aliyekuwa chachu ya ushindi wa Kenya, aliweza kuuvusha mpira kutoka nyuma na kuupeleka mbele akicheza kama winga wa kulia, wakati mwingine hata beki wa kulia, lakini akitumika zaidi kushambulia kupitia pembeni.

Naye alifunga hat-trick kwenye mechi ambayo timu yake ya Kenya ilicheza dhidi ya Djibouti.

**8. Juliet Nalukenge- Uganda**

Ni mchezaji tegemeo kwenye ufungaji kikosi cha Uganda na ndiye staa wa timu hiyo ya taifa.

Alifunga hat-trick kwenye mechi ambayo timu yake ilichapa Djibouti mabao 13-0.

Ni mchezaji ambaye anafaa kabisa kuwa kwenye kikosi hiki cha wachezaji 11 bora wa Cecafa, akiungana na wenzake kutoka timu nyingine wanaweza kutengeneza kikosi hatari sana kwenye ukanda huu.

**9. Asha Rashid 'Mwalala' - Kili Queens**

Ni mchezaji kiongozi na mkongwe kwenye kikosi cha Kilimanjaro Queens ambaye ametoa mchango mkubwa hadi timu kufika fainali.

Ana nguvu na uwezo wa kufumua mashuti makali ambayo humfanya awe mfungaji mzuri, mwenye uwezo wa kucheza kama straika wa kati namba tisa, 10 au kiungo mchezeshaji.

**10. Jentrix Shikangwa-Kenya**

Ndiye mshindi wa kiatu cha dhahabu kwenye michuano hiyo, akimaliza akiwa amefunga mabao 10, akipiga hat-trick kwenye mechi dhidi ya Djibouti, Kenya ikishinda mabao 12-0, Jentrix akifunga mabao matano peke yake kwenye mechi hiyo.

Ndiye aliyefunga magoli yote mawili kwenye mechi ya fainali Kenya ikiichapa Kilimanjaro Queens magoli 2-0.

Ni mchezaji hatari na wa kuchungwa kutokana na uwezo wake mkubwa wa kukokota mpira hasa kwenye mguu wake wa kushoto, chenga za maudhi ya kupiga mashuti makali.

Kocha wa Kenya mara nyingi alikuwa akimuingiza kipindi cha pili ambacho mabeki wa timu pinzani wanakuwa wamechoka.

**11. Mwanahamisi Omari-Kili Queens**

Huyu ni Mchezaji Bora kwenye michuano hiyo ambayo mwaka huu imefanyika katika msimu yake watatu. Ni mmoja wa wachezaji waliopiga hat-trick kwenye michuano hiyo.

Alifanya hivyo kwenye mechi dhidi ya Sudan Kusini alipofunga magoli matatu, Kilimanjaro Queens ilishinda mabao 9-0. Alimaliza michuano hiyo akiwa na magoli manne.

Uwezo wake wa kucheza na mpira, kasi, chenga za maudhi zimekuwa kivutio kikubwa kwenye michuano hiyo. Na ndiye mchezaji aliyekuwa akichungwa zaidi na wapinzani waliokuwa wakipambana na timu hiyo ya Tanzania Bara, hasa Kenya ambao walimuwekea ulinzi wa watu watatu waliokuwa wakitembea naye kila anakokwenda.

Mshambuliaji huyo kwa sasa anaichezea Simba Queens ya Dar es Salaam ambayo ilimsajili akitokea kwa mabingwa wa Ligi Kuu Wanawake msimu wa 2017/17, Mlandizi Queens ya mkoani Pwani,

## NJE YA UWANJA

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward, amesema kuwa aliwahi kuzuia usajili wa wachezaji wawili au mmoja wapya aliowataka aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Jose Mourinho.

Bosi huyo alisema kuwa alifikia uamuzi huo baada ya kuona tayari klabu ilishatumia kiasi kikubwa cha fedha, lakini ikiendelea kufanya vibaya katika Ligi Kuu England.



# SITA WANAOTAJWA KUMRITHI EMERY

**LONDON, England**

MIEZI 18 baada ya kumtea Unai Emery kuwa kocha wake, klabu ya Arsenal imeamua kuachana na mwalimu huyo, baada ya kupata matokeo mabaya dimbani.

Kibarua cha Emery kilifikia tamati Ijumaa baada ya Washika Bunduki hao kucheza mechi nyingi zaidi bila ushindi tangu mwaka 1992, huku kichapo kutoka kwa Eintracht Frankfurt cha 2-1 katika mchezo wa Ligi ya Europa kikifikisha mechi saba bila ushindi katika mashindano yote.

Baada ya kutimuliwa, nafasi yake amepewa mchezaji wa zamani wa klabu hiyo, Freddie Ljungberg ambaye atakuwa kocha wa muda.

Makala hii inakuchambulia makocha sita wanaopewa nafasi ya kuchukua mikoba ya Unai pale kwenye dimba la Emirates.

**Carlo Ancelotti**

Kwa sasa Arsenal hawataweza tena kufanya haraka katika kutafuta kocha wa kikosi hicho, ili aweze kurudisha makali yao kwenye Ligi Kuu England.

Katika umri wake wa miaka 60, Ancelotti anaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kupewa mikoba hiyo hasa kutokana na ukweli kwamba, nyuma yake ana mafanikio makubwa.

Aliweka historia pale Chelsea huku sasa akiiongoza vizuri zaidi Napoli, ana nafasi kubwa ya kuchukua jukumu hilo.

**Mauricio Pochettino**

Licha ya kuwa na mafanikio makubwa pale Tottenham, Pochettino alitimuliwa baada ya timu hiyo kuwa na mwanzo mbaya zaidi wa Ligi Kuu.

Aliifanya Tottenham kuwa moja ya timu iliyoleta ushindani mkubwa zaidi kwenye Ligi Kuu England na pia kuifikisha fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kwa sasa Pochettino ni mmoja wa makocha bora zaidi Ulaya na kuna uwezekano mkubwa Arsenal wakaamua kutupa ndoano yao kumchukua. Lakini kushinda kwake kuipa taji lolote Spurs kwa kipindi cha miaka mitano aliyokaa pale, kunaweza kuwa changamoto kubwa kwake.

**Freddie Ljungberg**

Raia huyu wa Sweden amepewa nafasi ya kuwa kocha wa muda, lakini kama atakuwa na matokeo mazuri kwenye mechi zinazokuja, anaweza kupewa mkataba wa kuinoa timu hiyo angalau hadi mwishoni mwa msimu huu.

Licha ya kwamba hana uzoefu wa kutosha, akitoka kuifundisha timu ya Arsenal chini ya umri wa miaka 23, na baadaye kupandishwa kwenye timu ya wakubwa kumsaidia Emery, anaweza kuliongoza jahazi hilo vizuri.

Kama ataweza kuiweka kwenye nafasi nzuri katika kipindi chake hiki cha muda, Ljungberg anaweza kupewa mkataba wa kudumu wa kuinoa timu hiyo.

**Nuno Espirito Santo**

Kocha huyo wa Wolves, Santo amekuwa akihusishwa kwa muda mrefu na kupewa nafasi ya kuinoa Arsenal hata kabla Emery hajatimuliwa.

Ni rahisi kujua kwanini. Kuitoa Wolves toka daraja la chini na baadaye kusumbua kwenye Ligi Kuu na kufuzu Ligi ya Europa kwenye msimu wake wa kwanza, ni mafanikio makubwa kwake.

Katika umri wake wa miaka 45 anaweza kuwa chaguo sahihi kwa Arsenal katika harakati zake za kutaka kurudisha ubora wao.

**Massimiliano Allegri**

Huyu ni kocha wa daraja la juu kabisa duniani. Rekodi ya kushinda mataji mengi pale Juventus ni moja ya sifa kubwa aliyonayo kocha huyu, huku akipendelea zaidi timu yake kuwa na safu imara ya ulinzi.

Alifanya kazi nzuri akiwa AC Milan na baadaye Juventus, hivyo jina lake linapewa nafasi kubwa zaidi ya kuchukua mikoba ya kuwanoa The Gunners hao.

**Mikel Arteta**

Huyu ni kocha msaidizi wa Manchester City na amekuwa nahodha wa Arsenal wakati akicheza pale. Kabla ya Emery kuteuliwa kuwa kocha, Arteta ndiye alikuwa akipewa nafasi kubwa zaidi ya kuchukua mkoba ya kuinoa Arsenal.

Akiwa ametumia miaka mitatu akifanya kazi chini ya Pep Guardiola, hali hiyo inamfanya Arteta kuwa na uzoefu wa kutosha.

Pamoja na wasifu wake Arteta ndiye anayetajwa zaidi kupewa nafasi ya kuwa kocha wa Arsenal ili kuchukua mikoba ya Mhispania mwenzake, Emery.



Mauricio Pochettino

## Nukuu

"Nataka kucheza kwa ajili ya England, na ninataka kucheza katika moja ya klabu kubwa Ulaya," **nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho (19), ambaye anawindwa na klabu saba, alisema maneno hayo baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona uliochezwa kwenye Uwanja wa Nou Camp Jumatano iliyopita.**




"Siwezi kumzungumzia Griezmann (Antoinne), kwa sababu ni mchezaji anayeichezea timu nyingine. Kila siku huwa naweza kumzungumzia na kumfikiria mtu ambaye tuko timu moja, siwezi kuweka kwenye mipango yangu, kitu kinachozungumziwa na watu," **Diego Simeone, Kocha wa Atletico Madrid alisema alipoulizwa kama anampango wowote wa kumrejesha Mfaransa huyo katika kikosi chake.**



"Mimi niko huru (kwa sababu), ninafurahi sana kufanya kazi katika klabu hii, itagemea pia na matokeo, ninataka kuona klabu, ninataka kuona wachezaji namna tunavyoendelea kufanya kazi pamoja, hili ndilo jambo muhimu sana kwangu, baada ya kukaa pamoja kwa miaka mitano," **alisema Pep Guardiola, Kocha wa Manchester City ambaye mkataba wake wa miaka mitano unatarajia kumalizika mwaka 2021.**



## Michezo



# SABABU 5 ZA KIUFUNDI AUSSEMS KUTEMWA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE klabu ya Simba imetangaza kuachana rasmi na kocha wake mkuu, Patrick Aussems, raia wa Ubelgiji.

Jumamosi iliyopita, klabu hiyo ilitangaza kuachana naye baada ya tetesi za muda mrefu ikiwa ni pamoja na kumsimamisha.

Katika taarifa ya klabu hiyo iliyotolewa na Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mbatha Mazingiza, ilisema kuwa wameachana na Aussems kwa sababu ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa viwango na malengo aliyokubaliana na klabu katika mkataba wake wa ajira ikiwamo kufika hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Pamoja na jitihada za dhati za bodi kumpa ushirikiano Patrick Winand J. Aussems hata baada ya kutolewa kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, bado ameendelea kuisimamia bila kujali malengo ya Simba, kujenga timu yenye ari na mafanikio, nidhamu na ushindani kwenye mashindano ya ndani na nje ya nchi," ilisema sehemu ya taarifa ya Mazingiza.

Uamuzi huo wa bodi unakuja siku tano tu baada ya Aussems kusimamishwa kwa sababu za utovu wa nidhamu na utetezi wake alioutoa kwenye kikao cha Kamati ya Nidhamu juzi haukuwa na mashiko baada ya kuondoka kwenye kituo cha kazi bila ruhusa.

Mazingiza amesema kwamba Aussems alikataa kuiambia Kamati ya Nidhamu alipokwenda na sababu za kwenda bila ruhusa.

Aussems alijiunga na Simba Julai 19 mwaka jana akitokea katika Timu ya Taifa ya Nepal, akichukua nafasi ya Mfaransa, Pierre Lechantre, aliyeondoka Mei mwaka jana.

Katika kipindi miezi 16 ya klabu, Aussems ameiongoza Simba kucheza mechi 91, ikishinda 61, ikifungwa 13 na kupata sare 17, ndani yake akiipa mataji matatu, ubingwa wa Ligi Kuu na Ngao ya Jamii mara mbili pamoja na kufikisha hatua ya Robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu uliopita.

Hadi anaondolewa, Simba SC inaongoza Ligi Kuu ikiwa na pointi 25 baada ya kucheza mechi 10, ikifuatiwa na Kagera Sugar yenye pointi 24, lakini ikicheza mechi 13.

Pamoja na sababu zote hizo mwandishi wa makala haya anakuletea sababu nyingine tano za kiufundi ambazo ziliwafanya viongozi wa Simba wafikie uamuzi wa kumwonyesha mlango wa kutokea.

**1. Timu kutokuwa na kiwango kizuri msimu huu**

Simba haijawa na kiwango kizuri msimu huu kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Ikumbukwe kuwa wanachama na mashabiki wa Simba wana sifa kwanza ya kutaka timu yao icheze soka la kuvutia na baadaye ushindi. Hilo lilionekana msimu uliopita, lakini msimu huu limeshindwa kuonekana.

Mechi ambazo angalau Simba ilionyesha kuwa ilicheza soka safi zilikuwa mbili tu msimu huu, nayo dhidi ya Power Dynamos ya Zambia siku ya Simba Day ikashinda mabao 3-1, pia kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC, ikashinda magoli 4-2.

Katika mechi za Ligi ya Mabingwa msimu huu, pamoja na Ligi Kuu, soka la timu hiyo chini ya Aussems halijawaridhisha mashabiki na viongozi wa timu hiyo.

**2. Baadhi ya wachezaji kushuka viwango**

Tofauti na msimu uliopita, baadhi ya wachezaji tegemeo msimu huu wameonekana kushuka viwango chini yake.

Mchezaji kama, Jonas Mkude na Claotus Chama wameonekana kushuka viwango kwa kiasi kikubwa na kuonekana kama vile hakuna juhudi yoyote inayofanywa ili kuwarejesha kwenye mstari.

Hata mchezaji mpya aliyesajiliwa msimu huu, Sharaf Eldin Shoboub, kiwango chake cha sasa ni tofauti na alipokuja, hasa alichokionyesha kwenye mechi za awali kabisa dhidi ya Azam FC, Ngao ya Jamii. Kwa sasa kila mechi zinavyozidi kusonga mbele, kiwango chake kinaonekana kupungua kiasi cha mashabiki kuomba asianzishwe, bali aingie kipindi cha pili.

**3. Wachezaji kuchoka mapema**

Msimu uliopita, timu yoyote iliyokuwa ikicheza na Simba kama haikufungwa goli mpaka dakika ya 65, basi kuanzia hapo dakika yoyote goli litapatikana tu.

Na kama tayari timu imeshafungwa bao moja, basi yataongezeka. Kuanzia dakika ya 65 kwenda mbele ndizo dakika za Simba kufunga magoli kwa kiasi kikubwa kwenye Ligi ya Mabingwa na Ligi Kuu kutokana na kuwa na pumzi za kutosha na kuonekana kana kwamba wanaanza mechi, huku wapinzani wao wakiwa wamekata pumzi.

Msimu huu kama Simba haikupata bao mpaka dakika 45 za kwanza, mechi inaweza kuisha kwa sare kwa sababu wanakata pumzi mapema na kuonekana kama hawana mazoezi ya kutosha.

**4. Stamina nayo tatizo**

Ukiiangalia Simba inavyocheza msimu huu, utagundua kuwa wachezaji wake wana tatizo la kutokuwa na stamina, yaani utimamu wa mwili.

Wachezaji wengi wa timu hiyo wawawezi kugombea mpira wa mchezaji wa timu pinzani wakaweza kunyang'anya.

Angalau wachezaji kama Meddie Kagere, Paschal Wawa, Hassan Dilunga, Miraji Athumani, Fraga Viera na Mzamiru Yassin wanaweza kufanya hivyo. Waliobaki ni tatizo.

Ndiyo maana imekuwa ikishambuliwa sana kwa sababu wengi hawakabi kwa kutokuwa na stamina ya kutosha.

Aussems hakwepi lawama kwani pamoja na kuwa na makocha wawili wa viungo, lakini ameshindwa kusimamisha hilo. Haiwezekani wachezaji wa Simba wenye walimu wa viungo wakashindwa kunyang'anyana mpira na wachezaji wa timu za mikoani ambao hawana walimu maalum wa viungo.


**5. Nidhamu mbovu ya wachezaji**

Kikubwa ni Aussems ameshindwa kusimamisha nidhamu, kwanza kabisa kutokana na wachezaji wa Simba kutokaa kambini kwa muda mrefu.

Wachezaji wa Kiafrika, hususan wa Kibongo unapowapa nafasi kubwa ya kukaa majumbani na kambini siku moja au mbili kabla ya mechi ni tatizo kubwa kwa sababu hawajitunzi, hivyo kufanya mambo mengine kinyume na maadili ya soka.

Na inawezekana kabisa matatizo yote haya yanaanzia hapa. Inasemekana kuwa baadhi ya viongozi walimtahadharisha kuhusu tabia hiyo, lakini kutokana na kuwa na "urafiki wa kupitiliza" na wachezaji wake wengi, alikuwa akiwapa ruhusa ya kuwa majumbani kwa muda mrefu kuliko kambini.

**NAJUA WAJUA**



Mshambuliaji Thierry Henry, ndiye nyota wa Timu ya Taifa ya Ufaransa ambaye mechi yake ya kwanza ya kimataifa alicheza Mei 21, mwaka 1904 dhidi ya Ubelgiji jijini Brussels na kutoka sare ya mabao 3–3, ndiye anashikilia rekodi ya kufunga magoli mengi.



# KWA NINI NI MSIMU WA MADRID LA LIGA

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid ndio mabingwa wenye rekodi katika Ligi Kuu Hispania, wakiwa wamelitwaa taji hilo mara 33. Hata hivyo, mafanikio yao kwenye ligi hiyo katika miaka ya hivi karibuni yamekuwa sio mazuri, hasa baada ya kutawaliwa na Barcelona.

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, Madrid imeshinda taji la La Liga mara sita, huku miamba wa pale Katalunya wakishinda mara 10, ikiwamo kushinda mara nne katika misimu mitano iliyopita.

Madrid ilianza msimu huu kwa ushindi wa 3-1 dhidi ya Celta Vigo ambapo ushindi huo ukaifanya klabu hiyo ya pale Bernabeu kukaa kileleni mwa La Liga.

Baada ya mechi 13, Madrid inaburuzwa na Barcelona kileleni kwa tofauti ya pointi nne (kabla ya mechi za jana).

Hapa tunaangalia sababu 3 kwa nini Madrid wanaweza kushinda taji la La Liga msimu huu, likiwa la kwanza kwa kipindi cha miaka mitatu.

**1. Zinedine Zidane**

Makocha wengi walitoa dukuduku lao wakati Zinedine Zidane akiwa hana uzoefu wa kuinoa timu ya wakubwa alipopewa nafasi ya kuinoa Real Madrid Januari 2016. Lakini Mfaransa huyo akafanya maajabu kwa kuwawezesha Real Madrid kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu. Hakuna klabu yoyote ilifanya hivyo tangu msimu wa 1992-93.

**2. Safu imara ya ulinzi**

Real Madrid ilianza msimu mpya wa La Liga kwa ushindi na sare nyumbani na ugenini kabla ya kucheza mchezo bila kuruhusu bao wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Sevilla, ambao mara zote huwa wanawasumbua.

Mabingwa hao mara 33 wa La Liga sasa wamecheza mechi tatu bila kuruhusu bao baada ya kuifunga Osasuna mabao 2-0 na baadaye sare ya bila kufungana na Atletico.

Madrid msimu uliopita ilicheza mechi 12 bila kuruhusu bao, lakini tayari msimu huu ina mechi sita ilizocheza bila kuruhusu bao katika mechi 13. Nahodha Sergio Ramos na Raphael Varane wamekuwa na "upatna" mzuri zaidi kwenye safu ya ulinzi ya Madrid wakionyesha kiwango kizuri cha kuzuia mashambulizi ya timu pinzani.

Golikipa wa kimataifa wa Ubelgiji, Thibaut Courtois pia amekuwa na msimu mzuri baada ya kuanza vibaya msimu wa 2018-19, akiwa amecheza mechi tano za La Liga bila kuruhusu bao. Ni makipa wanne tu kwenye La Liga ambao wamecheza mechi nyingi zaidi bila kuruhusu bao msimu huu.

Kwa mwanzo huu wa Ligi Madrid wanaonekana wana nafasi nzuri zaidi wa kulitwaa taji hilo, huku Courtois akionesha ubora wake kama alivyokuwa kwenye Ligi Kuu England na klabu ya Chelsea.

**3. Mabao ya Karim Benzema**


Karim Benzema kwa sasa anaonekana kama amezaliwa upya msimu huu. Baada ya kuwa na msimu mbaya wa 2018-19, Mfaransa huyo amerudi kwenye ubora wake, akiongoza kwenye chati ya ufungaji mabao na kwa sasa ametikisa nyavu mara 10 katika mechi 13 za LaLiga.

Benzema pia amenufaika na mabao kutoka kila pande ya uwanja. Wachezaji wengine 12 wa Madrid wamechangia mabao 18 kwenye la Liga msimu huu, kitu ambacho kinapunguza presha kwa mshambuliaji huyo. Kwa sasa Mfaransa huyo ana funga mabao kwa urahisi zaidi huku akisaidiwa na wachezaji wenzake na hivyo yeye kutokuwa na mzigo mkubwa.

Msimu uliopita, licha ya kuifungia klabu yake mabao 21 kwenye La Liga, Benzema alionekana kama vile hayupo kwenye ubora wake, hasa baada ya kuondoka kwa mfungaji aliyeweka rekodi klabuni hapo, Cristiano Ronaldo.

Baada ya mechi 13 msimu wa 2018-19, Madrid ilifunga mabao 20. Lakini hadi sasa msimu huu Los Blancos hao wamefunga mabao 28.

NDANI YA 18



ARSENAL imemtimua aliyekuwa Kocha Mkuu, Unai Emery baada ya kushindwa kupata ushindi katika mechi saba, matokeo hayo yametajwa kuwa mabaya zaidi kutokea kwenye timu hiyo tangu mwaka 1992.

Nipashe
Spotika



MIEZI 18 baada ya kumtea Unai Emery kuwa kocha wake, klabu ya Arsenal imeamua kuachana na mwalimu huyo, baada ya kupata matokeo mabaya dimbani. Kibarua cha Emery kilifikia tamati Ijumaa baada ya Washika Bunduki...

Uk. 16-17

# WA3 WANAOSUBIRI UPEPO WA KISULISULI JANUARI 2020



**LONDON, England**

USAJILI wa dirisha dogo la Januari ni muhimu kama lile la majira ya joto. Mara kwa mara timu zinatumia dirisha hili kwa ajili ya kusahihisha makosa yao kwa kile walichoshindwa kukikamilisha kipindi cha majira ya joto.

Dirisha la Januari linawapa wachezaji nafasi ya kujiimarisha zaidi kwa ajili ya kumalizia msimu.

Hapa tunawaangalia wachezaji watatu ambao wanasubiri dirisha hilo la Januari ili kuweza kukamilisha usajili wao katika klabu nyingine.

**3. Gareth Bale**

Sio jambo la kushangaza kwamba Gareth Bale ni mshindi mara nne wa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini bado mashabiki wa Real Madrid wanataka auzwe.

Bahati mbaya kwa Bale ni kwamba ameshindwa kujitengeneza kuwa kama Cristiano Ronaldo kwa mashabiki wa Madrid na hapo ndio kila kitu kilipokwenda mrama.

Wakati Ronaldo mshindi mara tano wa Ballon d'Or akiondoka na kutua Juventus, Bale alikuwa ndiye anatarajiwa kuchukua nafasi yake, badala yake mambo yamekwenda tofauti kabisa. Juu ya hilo, uvumi umeenea kwamba, klabu hiyo inataka kumuuza.

Kipindi cha majira ya joto kilichopita, Bale alikaribia kwenda kwenye Ligi Kuu China baada ya kushindwa kuelewana na kocha, Zinedine Zidane, lakini dili hilo lilishindikana dakika za mwisho. Raia huyo wa Wales mwenye umri wa miaka 30 kwa sasa ni wazi kwamba, safari yake inakaribia na kuna uwezekano mkubwa akaondoka wakati wa dirisha dogo la Januari.

**2. Nemanja Matik**

Alinunuliwa na kocha, Jose Mourinho, lakini Nemanja Matik ameshindwa kuwa na nafasi katika kikosi cha Manchester United kilichoko chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer. Wakati akiwa pale kwenye dimba la Stamford Bridge, raia huyo wa Serbia alikuwa mmoja wa viungo bora zaidi duniani kwa kiwango chake bora kabisa.

Mati mara kwa mara alikuwa akionekana kama kiungo mkabaji bora zaidi, lakini tangu atue pale Old Trafford mambo yamekwenda tofauti kabisa.

Msimu huu kiungo huyo mwenye umri wa miaka 31 amecheza mechi tatu tu za Ligi Kuu. Kocha Ole ni kama anamuona hafiti kuvaa jezi ya United.

Juu ya hilo uvumi umekuwa ukienea kwamba, mchezaji huyo anataka kuondoka na kwa namna yoyote ana nafasi kubwa ya kuachiwa wakati wa dirisha dogo la Januari, huku Tottenham ikipewa nafasi kubwa ya kupata saini yake ili akaungane na kocha wake wa zamani, Jose Mourinho.

**1. Granit Xhaka**

Kutoka kuwa nahodha wa Arsenal hadi kuwa katikati ya mgogoro na mashabiki wake. Granit Xhaka kwa sasa hana nafasi kubwa pale Arsenal na kuna uwezekano mkubwa akaondoka wakati wa dirisha la Januari.

Alibwatukiana na mashabiki wakati Arsenal ikitoka sare na Crystal Palace na hivyo mchezaji huyo raia wa Uswisi akajikuta akivuliwa kitambaa cha unahodha na hajawa kwenye kikosi tangu hapo.

Xhaka sasa anaonekana kwamba maisha yake pale Arsenal yanafikia mwisho na katika umri wake wa miaka 27 ana nafasi kubwa ya kuondoka wakati wa dirisha dogo la usajili.

Katika kipindi chake cha miaka mitatu aliyokaa na klabu hiyo Xhaka alionekana kama mchezaji ambaye hastahili kuvaa jezi ya klabu hiyo. Uvumi umeenea kwamba, klabu ya AC Milan imekuwa ikiwania saini yake.

Hivyo kuna uwezekano mkubwa akaondoka pale kwenye dimba la Emirates kipindi cha dirisha dogola usajili la Januari, hasa ikizingatia kwamba, uhusiano wake na mashabiki wa klabu hiyo umeshaingia doa.

**USILOLIJUA**



TIMU ya Taifa ya Brazil ilicheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa mwaka 1914 na katika mchezo huo, ikiwa mwenyeji ilipokea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa Argentina. Brazil ilicheza pia mechi yake ya kwanza ya Kombe la Dunia mwaka 1930.



# Polisi yasaka waliomjeruhi mwenyekiti CCM

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

JESHI la Polisi limefanya msako mkali wa nyumba kwa nyumba katika Kijiji cha Gooye Kata ya Ndato wilayani Rungwe kwa lengo la kukibaini kikundi cha watu wanaovuruga amani katika kijiji hicho, kwa kuwashambulia wananchi, huku mashambulizi hayo yakihusishwa na siasa.

Msako huo ulianza mwishoni mwa wiki baada ya kikundi cha watu wanaodaiwa kuwa zaidi ya 10 kumvamia Mwenyekiti wa Kijiji cha Ndaga kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), George Mwasoni, na mkewe na kuwajeruhi sehemu mbalimbali za miili.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mtu mmoja ambaye anajulikana kwa jina moja la Joseph, anashikiliwa kutokana na tukio hilo na wengine 13 wanatafutwa.

"Ni tukio baya sana kutokea katika kijiji hiki, huyu bwana Geoge ni mwenyekiti wa CCM tawi la Ndato na ni miongoni mwa wenyeviti waliopita bila kupingwa kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, hivyo hili tukio linahisiwa kuhusika na masuala ya siasa," alisema Kamanda Matei.

Alisema pamoja na mtu huyo mmoja kukamatwa, lakini jeshi hilo lina majina zaidi ya 13 ya washukiwa wa tukio hilo, na kwamba watahakikisha wote wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Akizungumza na wananchi hao kwenye mkutano wa hadhara Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema matukio ya wananchi hao kushambuliana yalianza mwanzoni mwa vuguvugu la uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema tangu wakati huo wamekuwa wakipokea taarifa za matukio mbalimbali ya wananchi hao kuviziana na kushambuliana hasa nyakati za usiku na kwamba sasa wameamua kupeleka Jeshi la Polisi ili kurejesha amani katika kijiji hicho.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kuendelea kupiga kambi katika kijiji hicho mpaka wahusika wa uhalifu wanakamatwa na kuchukuliwa hatua na kwamba wananchi wote ambao wamekimbia makazi yao wanatakiwa warejee.

Chalya aliwataka wananchi waendelee kuwafichua wahusika wa matukio hayo ili wachukuliwe hatua na kukomesha matukio hayo na waendelee kuishi kwa amani.

"Hatuwezi sisi kama serikali tukaacha kikundi cha wahuni kianze kudhuru raia halafu tunyamaze haiwezekani, hivyo tunaomba ushirikiano wenu ili wahusika wakamatwe na tunapenda sana muishi kwa amani," alisema Chalya.

Aliwataka wanasiasa wanaoeneza chuki katika wilaya hiyo kuacha mara moja tabia hiyo na akawataka watu hao waache siasa kwa maelezo kuwa chuki sio tafsiri sahihi ya siasa.

Baadhi ya wananchi walisema kutokana na msako huo wa Jeshi la Polisi baadhi ya wananchi wametelekeza familia zao na kutokomea kusikojulikana hali ambayo ni hatari kwa maisha ya watoto wao.

Mwenyekiti wa CCM Kata ya Ndato, Emmanuel Kajuni, alisema baadhi ya watoto waliachwa bila chakula na wazazi wao, huku akisisitiza kuwa wamekuwa wakiishi kwa hofu katika kata hiyo.

Aliiomba serikali kujenga kituo cha polisi katika eneo hilo ili kudhibiti matukio hayo ya uhalifu unaofanywa na vikundi vya watu ambao baadhi wanafahamika.




Abiria wa mabasi ya kutoka Mkwajuni Songwe kuelekea katika Mji wa Mbalizi mkoani Mbeya, wakisukuma gari iliyobeba shenena ya mbolea ya kupandia tumbaku kupeleka katika Wilaya ya Songwe iliyokuwa imekwama juzi katika eneo la Ndiwi Kata ya Mshewe, kufuatia barabara hiyo kuharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha hali iliyosababisha magari mengine kushindwa kupita. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# TFS yautaja msitu wa Kambikatoto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, umeomba ukabidhiwe msitu wa Kambikatoto wilayani Chunya ili uhifadhiwe kisheria, kwa lengo la kuokoa mapitio ya wanyamapori pamoja na vyanzo vya maji.

Akizungumza kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mbeya (RCC), Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, alisema eneo hilo lina ukubwa wa hekta 179,078 na lina vyanzo vingi vya maji ambavyo vinapeleka maji Mto Ruaha na Ziwa Rukwa.

Alisema mbali na msitu huo kuwa na vyanzo vingi vya maji, pia ni mapitio ya wanyama pori kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Pori la akiba la Lukwati.

Alisema msitu huo ni wenye miti ya asili ambayo imekuwa ikiteketezwa na baadhi ya wananchi ambao wanaikata na kuitumia kwa shughuli mbalimbali na kwamba endapo hautahifadhiwa kisheria kuna hatari ya kutoweka.

"Lakini pia msitu huo ni muhimu kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo ni tishio kwa mstakabali wa maendeleo ya jamii, pia ni msitu wenye uoto unaowezesha ufugaji wa nyuki na una bioanuai muhimu za miti na wanyama," alisema Lupembe.

Alisema msitu huo unapakana na vijiji vinne ambavyo ni Kambikatoto, Mafyeko, Bitimanyanya na Lualaje na kwamba unapakana pia na Hifadhi za misitu ya Kipembawe, hifadhi ya msitu wa kipembawe pamoja na Pori la Akiba la Lukwati.

Alisema wakala huo umeshafuata taratibu zote zinazohitajika wakati wa kuhifadhi msitu mipya kama sheria ya misitu namba 14 ya mwaka 2002 inavyoelekeza ikiwamo kulitambua eneo linalohitaji kuhifadhiwa, uchunguzi wa mipaka pamoja na makubaliano na wananchi.

Mbunge wa Lupa, Victor Mwambalaswa, aliiomba kamati kuridhia msitu huo kuhifadhiwa kwa maelezo kuwa una umuhimu mkubwa katika uhifadhi wa mazingira.

Alisema msitu huo pamoja na misitu mingine wilayani huo ina umuhimu mkubwa ikiwemo kusaidia kuwapo kwa mvua ya kutosha katika Mkoa wa Mbeya na mikoa jirani.

Mwambalaswa alisema Wilaya ya Chunya ndio yenye misitu mingi iliyohifadhiwa ikilinganishwa na wilaya zote za Mkoa wa Mbeya na kwamba faida yake inaonekana.

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema hawawezi kuridhia kienyeji wakati hawajaliona eneo lenyewe, hivyo alishauri aende kwanza akaangalie na kuzungumza na wananchi kabla ya kupitisha uamuzi huo.

Alisema kwa sasa serikali imepunguza baadhi ya mapori na misitu iliyohifadhiwa ili kupunguza migogoro ya ardhi, hivyo haitakuwa vizuri wakakubali kuhifadhi msitu ambao pengine unaweza ukasababisha migogoro na wananchi.

## Maofisa wa Ruwasa wachongewa urasimu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Francis Mtega, amewachongea maofisa wa Mamlaka ya Maji Mijini na Vijijini (Ruwasa) wa wilaya hiyo kwa mabosi wao, akidai wana urasimu kwenye utendaji kazi hali ambayo inakwamisha miradi.

Aliwashtaki watumishi hao kwenye kikao cha wakuu wa wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, wakurugenzi, makatibu tawala wa wilaya, watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Mbeya-WSSA pamoja na watendaji wa Ruwasa.

Alisema watumishi hao walisababisha baadhi ya wafadhili waliokuwa na nia ya kusambaza maji katika Kata ya Chimala wilayani humo kutaka kuhamisha mradi huo na kuupeleka mahali pengine baada ya kuona wanapigwa chenga.

"Waliwaandikia wafadhili wetu barua wakiwa wameorodhesha gharama zao kwenda katika eneo hilo ambazo zilikuwa zinafikia zaidi ya 2,000,000 sasa wafadhili wakaniambia ni bora wapeleke mradi huo mahali pengine, kitu ambacho kilitusikitisha sana," alisema Mtega.

Aliuomba uongozi wa Ruwasa ngazi ya Mkoa kuwaonya watumishi hao ili wasiharibu miradi ambayo ni ya kuwanufaisha wananchi wa kawaida kwa kutaka kupata vitu vidogo vidogo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwatahadharisha watumishi wote wa umma mkoani humo kuacha urasimu kwenye miradi inayoletwa na wawekezaji.

Alisema yeyote atakayebainika, atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria, na kwamba yeye ndiye aliyekabidhiwa Mkoa wa Mbeya ausimamie na atahakikisha anapambana na matukio ya aina hiyo.

Alisisitiza kuwa vitendo vya urasimu vinaambatana na rushwa kwa madai kuwa huwa wanakuwa na urasimu ili kushawishi wapate kitu kidogo kutoka kwa wawekezaji.



# Ataka mitaala ya viwanda, kilimo, kodi vyuoni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKUU wa Chuo cha Mipango na Maendeleo ya Vijijini, Prof. Hozen Mayaya, amesema ipo haja ya kuingiza kwenye mitaala ya vyuo masuala ya viwanda, kilimo na kodi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Prof. Mayaya alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika kongamano la chuo lililokuwa likijadili jinsi viwanda vilivyo na uhusiano wa karibu na kilimo na kodi.

Alisema kutokana na serikali kufanya jitihada za kuhakikisha inajenga uwezo wa kujitegemea kupitia mapato ya ndani ni vyema vitu hivyo vikaingizwa kwenye mitaala ili kusaidia kutoa elimu kwa wahitimu wenye utaalamu mbalimbali.

Mkuu huyo alisema ili kuhakikisha juhudi hizo zinafanyika kwa haraka zaidi, ni lazima elimu ya viwanda, kilimo pamoja na kodi iingizwe kwenye mitaala.

"Mitaala ya vyuo ndiyo inaweza kusaidia serikali katika masuala haya, lakini pia vyuo vya elimu na taasisi viendelee kutoa elimu kwa wanachuo na wananchi kuhusu ulipaji wa kodi ili kujiletea maendeleo," alisema.

"Tunaweza kuiweka kwenye mitaala yetu tusisubirie chuo cha kodi ndio kitoe elimu ya kodi, kuna masomo kama ya maendeleo 'development studies' tunaweza kuhakikisha masuala ya kodi yanahusishwa."

Naye Kamishna Msaidizi wa Bajeti kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Mwamwaja Charles, alisema ili kilimo kitosheleze viwanda ni lazima kiwe cha kisasa.

Alisema viwanda vinahitaji malighafi za uhakika kila siku. Hata hivyo, alisema kuna uwezekano wa kujenga mazingira mazuri kwa Watanzania kulipa kodi bila kushurutishwa kwa kutoa elimu kwa manufaa ya taifa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi anayehusika na masuala ya uratibu wa sera, Ofisi ya Rais, Tamisemi, Dk. Andrew Komba, alisema ipo haja ya serikali pamoja na sekta binafsi kujikita zaidi katika masuala ya uwekezaji na kukuza uchumi wa kila mwananchi.

Komba alisema kunahitajika kuwekeza kwenye kilimo na kukifanya kiwe na tija.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. John Jingu, akizungumza mwishoni mwa wiki wakati alipokuwa akifunga Mkutano wa Mtandao wa Mashirika ya Wazee Tanzania uliofanyika jijini Dodoma. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Sheria ndogo kudhibiti uharibifu mazingira

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, imetakiwa kutunga sheria ndogo itakayosimamia mazingira na kulinda miti inayopandwa.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, alipokuwa akizindua mradi wa kuifanya Dodoma kuwa ya kijani unaofadhiliwa na Shirika la Kuhifadhi Mazingira la Kimataifa (WWF) kwa kushirikiana na Vodacom Foundation na TFS.

Alisema sheria hiyo itasimamia suala la mazingira ikiwamo utunzaji miti inaopandwa.

Aliagiza Wakala wa Misitu nchini (TFS), Kanda ya Kati, kutoa miche ya miti 37,000 kwa vyuo na shule za jiji la Dodoma ili kutekeleza agizo la serikali ya awamu ya tano ya kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Aliainisha kuwa miche 20,000 itapelekwa vyuo vya elimu ya juu, 10,000 kwa vyuo vya kawaida, 5,000 sekondari na shule za msingi miche 2000 ili ipandwe kwenye maeneo mbalimbali.

Katambi alisema taasisi zote za serikali zinapaswa kupelekewa miti ili kuhakikisha inapandwa na kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

"Naomba maagizo haya yatekelezwe haraka iwezekenavyo lengo ni kuona mazingira ya Dodoma yanaboreshwa na kuifanya inakuwa ya kijani," alisema.

Mkurugenzi wa WWF, Dk. Amani Ngusaru, alisema shirika hilo limejipanga kuhakikisha Dodoma inakuwa ya kijani kutokana na upandaji miti katika maeneo mbalimbali.

"WWF inaunga mkono jitihada za Ofisi ya Makamu wa Rais na Rais John Magufuli ya kutunza mazingira ndio maana tuko Dodoma kwa ajili ya kutekeleza agizo hilo," alisema Dk. Ngusaru.

Alisema wao kwa kushirikiana na TFS, Vodacom Foundation na wadau wengine watahakikisha miti hiyo inastawi na kubadilisha mazingira ya Jiji la Dodoma kuwa ya kijani.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa TFS, Yohana Sanga, alisema wameandaa miche zaidi ya milioni moja kwa ajili ya kuisambaza sehemu mbalimbali na kubadilisha mazingira ya jiji hilo.

# Waitara atamani sheria kuadhibu wasiotunza wazazi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, ameshauri kutungwa kwa sheria ya kuwalazimisha watoto kuwatunza wazazi wao wanapokuwa wazee.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa mtandao wa mashirika ya wazee Tanzania uliofanyika jijini hapa.

Alisema kuna baadhi ya watoto wanaokwepa kuwatunza wazazi wao na kusababisha wazee kuishi kwenye mazingira magumu.

"Ninatamani iwepo sheria ya kuwalazimisha watoto kuwatunza wazazi wao kutokana na baadhi ya vijana kuponda maisha ya starehe mjini na vijijini huku wazazi wao wakitaabika kwa ugumu wa maisha wakati wazazi hao walihangaika na kujinyima kwa kuwasomesha," alisema.

Waitara alisema wazee hao wamewahangaikia watoto wao na kuwatengenezea msingi mzuri wa maisha, lakini wanawatelekeza na kuishi maisha magumu.

"Mimi natoka Mkoa wa Mara Wilaya ya Tarime, kuna mwenzetu mmoja sitamtaja jina aliwahi kufiwa na mzazi wake mkoani Dar es Salaam na alikuwa tajiri, ilimbidi aweke msiba kwa siku kadhaa ili kukamilisha ujenzi nyumbani huko Tarime, kwanini asingejenga nyumba hiyo mapema ili wazazi hao waishi kabla ya kufa," alihoji.

Alisema watoto wanatakiwa kuwawekea maisha bora wazazi wao wakiwa hai na si kusubiri kuwavisha suti wakati wakifariki.

Hata hivyo, Naibu Waziri huyo alisema maadili yameporomoka kutokana na vijana wengi kutowajali wazee hasa kwenye vyombo ya usafiri.

"Utakuta kijana amekaa kwenye siti ya gari huku mzee akiwa amesimama," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mtandao huo, Sebastian Bulegi, alisema mtandao huo ni muungano wa mashirika 39 ya wazee na umekuwa ukitetea haki za wazee wote nchini.

Pia alisema unasimamia kazi na kuratibu kazi zote za kila siku za mashirika hayo.

Aliomba kutungwa kwa sheria ya kuwahudumia wazee nchini ili kutambuliwa na kuhudumiwa mahitaji muhimu ya maisha.

Alishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuwatambua wazee na kuwasaidia ruzuku kila mwezi kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

Kadhalika, aliomba serikali kuwateua wazee katika nafasi mbalimbali za uamuzi katika jamii kwa kuwa bado wana uwezo wa kufanya kazi.



# Bashiru akemea siasa za kibaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amekemea siasa za ubaguzi ambazo amesema madhara yake ni makubwa katika ustawi wa maendeleo ya nchi.

Amesema ubaguzi hauwezi kujenga umoja wa kitaifa na kwamba CCM ni chama kinachoongoza dola kinatakiwa kuvikumbusha vyama vingine vya siasa nchini kuepuka dhambi hiyo kwa kuwa madhara yake ni makubwa.

Aliyasema hayo, wakati akizungumza na viongozi na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Mjini Unguja.

Vile vile, Dk. Bashiru alikemea siasa za ubaguzi na kutaka kupingwa na vyama vyote vya siasa kwa kuwa zinaharibu sifa ya nchi na kusababisha mipasuko isiyokuwa ya lazima kwa wananchi.

Alisema CCM sio chama cha wakati wa uchaguzi bali ni cha uongozi kinachoongoza wananchi wote, hivyo hakiwezi kushindwa kukemea masuala mbalimbali yanayolenga kuhatarisha amani na utulivu wa nchi.

"Siasa za ubaguzi haziwezi kujenga umoja wa kitaifa hivyo tukiwa ni chama kinachoongoza dola ni lazima tuwakumbushe vyama vingine vya siasa nchini waepuke dhambi hiyo kwa kuwa madhara yake ni makubwa juu ya ustawi wa maendeleo ya nchi," alisema Dk. Bashiru.

Kupitia Kikao hicho alihimiza wanachama kuendeleza utamaduni wa kuwa na uhusiano wa kijamii baina ya wanachama na wanachama pamoja na wananchi wengine.

Alisema uhusiano huo ndiyo msingi wa umoja na mshikamano wa CCM unaowafanya watu wawe wamoja.

Pia, aliwataka viongozi na watendaji wa CCM visiwani Zanzibar kuendelea kubuni miradi itakayoongeza mapato ndani ya chama.

Alisema kuwa miradi itasaidia chama kujitegemea kiuchumi, rasilimali za vyanzo vya mapato zinazomilikiwa na CCM katika maeneo mbalimbali nchini zikitumiwa vizuri, zitasaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa fedha nchini.

"Chama chetu kimejaaliwa kuwa na rasilimali nyingi zikiwamo majengo, ardhi na vitu mbalimbali vilivyoasisiwa na wazee wetu wa ASP na TANU, wajibu wetu kuvitunza na kuongeza vingine ili na sisi tuache alama za uongozi kama walivyofanya viongozi waliopita," alisema.

"Nasi tunaendelea kudhibiti rasilimali hizo zisihujumiwe na watu wachache kwa kuwa zipo kwa manufaa ya wanachama wote."

Akizungumza kwa wakati tofauti wakati akipandisha bendera za chama katika mashina mbalimbali ya CCM, aliwataka watendaji wa ngazi za wilaya kuhakikisha mabalozi wote wanapatiwa vitambulisho vitakavyowasaidia kuingiza katika ofisi za umma kuwasilisha changamoto za wananchi ili zitatuliwe.

Akikagua kazi za vikundi vya ujasiriamali katika Chuo Cha Ujasiriamali cha UWT Wilaya ya Mjini Kilichopo Miembeni, Dk. Bashiru aliwapongeza viongozi wa CCM na kuwataka bidhaa zinazozalishwa katika chuo hicho zitafutiwe soko la uhakika.



Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohammed Khamis Mussa, akiongea na baadhi ya wanachama wa Saccos ya Meli Nne wakati wa semina kuhusiana na kutambua dalili za ugonjwa wa saratani ya matiti iliyoandaliwa na Saccos hiyo na kufanyika mjini Zanzibar jana, (kulia) ni ofisa kitengo cha maradhi yasioambukiza kutoka Wizara ya Afya Zanzibar, Zuhura Saleh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaume watakiwa kufichua wadhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Zanzibar, Katerina Peter Nao, amewataka kinababa kuwa tayari kuwafichua wanaume wanaofanya vitendo vya udhalilishaji kwa watoto.

Aliyasema hayo katika hafla ya sherehe za wazazi wa Shule ya Maandalizi ya Mwangaza iliyopo Munduli Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema kumekuwapo na vitendo vya udhalilishaji kwa watoto hasa ubakaji ambao unasababishwa na baadhi ya wanaume wasiokuwa na utu na kwamba umefika wakati sasa kinababa wakashirikiana na kinamama wakati linapotokea tukio.

Alisema hatua ya kushirikiana itasaidia kuondoa au kupunguza vitendo hivyo.

Alisema ni jambo la kawaida kuwaona kinamama pekee wakifatilia matendo hayo, sasa juhudi za pamoja zinahitajika ili kuhakikisha wabakaji wote wanatiwa hatiani.

Kadhalika alisema Rais ametia saini Sheria ya Makosa ya Jinai ambayo imezuia dhamana kwa wabakaji, lakini bado wanakwama kutokana na watu kutokwenda kutoa ushahidi.

Alisema ushahidi ni muhimu katika kuthibitisha makosa na kuwataka wahakikishe wanaripoti matukio hayo pamoja na kwenda kutoa ushahidi yanapofika mahakamani.

"Rais katia saini sheria, lakini inakwama kutokana na watu kushindwa kwenda kutoa ushahidi mahakamani," alisema Nao.

Akisoma risala ya wanafunzi wa shule hiyo, Yusra Salum, alisema watoto wana wakati mgumu kutokana na kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema hivi sasa watoto hawako katika usalama jambo linalowanyima raha wanapotembea.

# Z'bar yajikita matumizi Tehama

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imejielekeza zaidi katika matumizi ya Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano kwenye maeneo yote yenye vivutio vya utalii kama mkakati wake kabambe wa kuiinua sekta hiyo muhimu pamoja uchumi wa kisiwa hicho.

Utalii unachangia takribani asilimia 25 ya Pato la Zanzibar (GDP) na asilimia 80 ya pesa za kigeni, ajenda ya serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha matumizi ya teknolojia yanaimarishwa maeneo yote wanayotembelea watalii wengi ikiwamo mji Mkongwe.

Akizungumza na waandishi wa habari waliokwenda kujifunza na kuona maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) visiwani hapa mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa Mawasiliano katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi, Dk. Mzee Suleiman Mndewa, alisema mbali ya utalii, Tehama imekuwa kichocheo kwenye sekta zingine za uchumi.

"Kutoka na umuhimu huu ndiyo maana tumeweka kamera za usalama katika eneo zima la mji Mkongwe na lengo likiwa kuhakikisha kuwa mtu yeyote anayetembelea eneo hilo anakuwa salama mpaka anaporudi kwake," alisema Dk. Mndewa.

Dk. Mndewa ambaye ni mbobezi pia katika masuala ya Tehama alisema serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo kampuni kubwa ya kichina ya mawasiliano ya ZTE Corporation, imechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya Tehama ambayo ni chachu kwa maendeleo ya uchumi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano Zanzibar, Mhandisi Shukuru Awadhi Suleiman, kuelewa umuhimu wa utalii kwa maendeleo ya uchumi wa Zanzibar ni vizuri kwa uongozi wa Rais Dk. Ali Mohammed Shein, umeimarisha huduma ya mawasiliano maeneo yote ya utalii Kaskazini, Kusini na Zanzibar mjini.

"Tumefanikiwa sana kwa msaada au kuungwa mkono na kampuni zote simu na tuone kitovu cha Tehama na hivyo kurahisisha huduma kwa watalii," alisema na kuongeza kuwa wanaoendesha shughuli za utalii wananufaika na Mkongo wa Taifa.

Pia alisema Mkongo wa Taifa umesaidia kuwapunguzia gharama wanaoendesha au kujihusisha na shughuli za utalii visiwani hapo kwa kuwa hawahitaji kutumia 'microwaves' kwa ajili ya mawasiliano kama ilivyokuwa awali. Kwa mujibu wa Mhandisi Suleiman, 'microwaves' ni gharama kubwa ndiyo maana serikali ilikuja na ajenda ya Mkongo wa Taifa ili kuimarisha mawasiliano kwa watalii na wakazi wa Zanzibar.

"Teknolojia ya 'Microwave' hupitisha kiwango kidogo cha data ukilinganisha na Mkongo wa Taifa na pia uendeshaji wake unatumia gharama kubwa sana na unahitaji pia umeme au jenereta," alisema.

# FCC, TET zaandaa mtaala kulinda mlaji

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WAKATI serikali ikijikita katika uchumi wa viwanda, Tume ya Ushindani (FCC) kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu (TET), zipo katika hatua ya kuandaa mtaala ya kulinda mlaji kwa shule za msingi na sekondari ili bidhaa zitakazozalishwa kupitia viwanda ziweze kukidhi ubora na kuleta ushindani katika masoko ya ndani na nje.

Ofisa Mwandamizi wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma wa Tume hiyo, Frank Mdimi, alisema lengo la mtaala huo ni wanafunzi waanze kufundishwa mapema na kueneza elimu hiyo katika jamii kuhusu umuhimu wa kuzitambua bidhaa zenye ubora na zisizo na ubora hatua ambayo itasaidia kuleta ushindani katika soko na kumlinda mlaji.

Mdimi alisema kuwapo mitaala ya elimu ya kulinda mlaji shule za msingi na sekondari itakapofanikiwa ni hatua muhimu hasa kwa uchumi wa viwanda kwa vile bidhaa hizo zitakapokwenda sokoni zitakuwa bora zaidi unaokubalika kitaifa na kimataifa, hivyo kuvifanya viwanda kuwa na uhakika na masoko.

Alifafanua kuwa bidhaa zisizokuwa na ubora walaji hawatakubali kuzipokea sokoni na kutokana na baadhi ya wazalishaji wake wakati mwingine kushindwa kuandika maelezo ya matumizi yasiyojitosheleza.

Alisema FCC jukumu lake ni kutoa elimu kwa ujumla, lakini waliamua kwenda mbali zaidi kwenye shule za msingi na kuanzisha vilabu za wanafunzi na kutoa elimu ya ulewa wa kumlinda mlaji ili visaidie kuelimisha jamii wanapokuwa nyumbani.

Alisema FCC imeshatoa elimu ya kumlinda mlaji katika vilabu vya shule tano za Manispaa ya Morogoro ambazo ni Mzimbu A, Mazimbu B, Kihonda, Mzinga, Kemo na Mafiga B.

Mmoja ya walimu katika Shule ya Msingi Mazimbu A, Ezra Lukwale, alisema kama itatungwa mitaala hiyo kwa shule za msingi na sekondari, kutasaidia siku za usoni kujenga jamii yenye uelewa kwa kuanzia na ngazi ya chini ya familia mpaka ngazi ya juu kielimu, hivyo kuvisaidia baadhi ya viwanda vinavyozalisha bidhaa kiujanjaujanja kubadilika na kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokubalika.

Mwanafunzi wa shule hiyo wa darasa la sita, Debora Philemon, alisema kupitia klabu hiyo amejifunza mambo muhimu yakiwamo ya kukagua uhalisia wa bidhaa ikiwamo ufungashaji wa bidhaa, uandishi wa jina la bidhaa au nembo.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mhandisi Dk. Samuel Gwamaka (kushoto), akimwelekeza jambo Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhandisi Joseph Malongo katika ziara ya kukagua uharibifu wa mazingira katika Mto Nyakasangwa ulipo Boko jijini Dar es Salaam na kupiga marufuku uchimbaji mchanga na utupaji takataka katika maeneo ya mito nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakunwa mbolea kuongeza vitunguu

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

UZALISHAJI wa zao la vitunguu na mahindi umeongeza mavuno kutokana na matumizi ya mbolea katika eneo la Mbuyuni, Wilaya ya Karatu, huku baadhi ya wakulima wadogo wakieleza kufurahishwa.

Waliwaeleza wanahabari ambao wamo katika ziara ya mikoa ya kaskazini kujionea shughuli za kilimo na kusikia mawazo yao juu uzalishaji wa mazao wanayolima na iwapo kilimo chao kinawapa matumaini ya kuboresha maisha yao kulingana na shabaha ya serikali ya kuifanya Tanzania kuwa taifa la uchumi wa kati ifikapo 2025.

Wakulima walio wengi wamesifu elimu inayotolewa na maofisa ugani wa Kampuni ya Yara na kusema kwamba elimu hiyo imesaidia kuongeza uzalishaji mazao wanayolima.

"Uzalishaji ulikuwa mdogo sana kabla ya ujio wa mbolea hizi za Yara, lakini sasa tunazalisha zaidi ya mara tatu au nne ukilinganisha na huko tulikotoka, tunawashukuru kwa namna pekee jamaa hawa kwa jinsi walivyotukomboa sisi wakulima wadogo," alisema Emmanuel Ole Mollel, bila kutoa takwimu.

Mollel, ambaye ni mkulima wa vitunguu, alisema mbolea na pembejeo vinavyosambazwa na Yara vimewapa matumaini makubwa kwamba kilimo kitawatoa katika lindi la umaskini.

"Yara wametupa matumaini makubwa ya kuinua kilimo chetu cha vitunguu, kwa sababu wingi wa vitunguu na kupatikana kwa sokoo vimefanya kipato chetu kiwe kizuri," alisema.

Licha ya kuipongeza Yara, Mollel pia aliishukuru serikali kwa namna inavyoshirikiana na wadau wa kilimo katika sekta binafsi katika kuwakwamua wakulima.

"Jitihada hizi za Yara zinatokana na msukumo wa serikali yetu katika jitihada yake ya kutimiza azma ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati. Hivyo naipongeza sana serikali kwa namna inavyoshirikiana na wadau katika sekta ya kilimo ili kumwinua mkulima wa kawaida," alieleza.

Gwandu John, mkulima wa mahindi katika eneo hilo, alieleza kuwa elimu inayotolewa na maofisa ugani wa Yara ina thamani sana, kwani imewafanya wakulima watambue namna bora ya matumizi ya mbolea na udongo. "Maofisa ugani wa YARA wametuweka pazuri kwani miaka ya nyuma hatukujua matumizi sahihi ya mbolea na wala hatukujua kwamba tulikuwa tunafanya makosa. Hali hiyo ilichangia kupata mavuno kidogo. Lakini tangu tumeanza kutumia huduma zao, uzalishaji umeongezeka sana," alisema John.

Kwa mujibu wa John, uongezekaji wa zao la mahindi umewajengea heshima wakulima.

"Sasa tunasimama mbele za watu na kujivunia mageuzi haya ya kilimo katika zao la mahindi, tumelima kwa miaka mingi lakini sasa tupo mahali pazuri . Mafanikio yanatusaidia katika maisha ya kila siku," alisema John.

# Mtaalamu kuchunguza magonjwa ya saratani

**Na Joseph Mwendapole**

DAKTARI bingwa wa magonjwa ya saratani kutoka India, Dk. Plis Sridhar, anatarajiwa kuendesha kambi ya uchunguzi wa magonjwa hayo na kutoa ushauri wa namna ya kukabiliana na maradhi hayo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Hospitali ya Regency, uchunguzi huo utaanza Jumanne katika tawi la hospitali hiyo lililopo Upanga, Dar es Salaam.

Ilisema kambi hiyo ni muhimu kwa ajili ya Watanzania kuwaona wataalamu waliobobea kwenye maradhi hayo badala ya kwenda nje ya nchi kwa ajili ya tiba hiyo.

"Watu wengi wamekuwa wakienda nje ya nchi kutafuta tiba kama hii, lakini wataalamu hawa waliobobea watakaoendesha kambi hii wanafanya kile ambacho mtu angekipata nje ya nchi hivyo kupunguza gharama za nauli na maisha ya nje ya nchi," ilisema taarifa hiyo.

Ilisema kwa watu ambao walishawahi kufanya vipimo mbalimbali wanapaswa kwenda navyo kwaajili ya kuwaonyesha wataalamu hao wakati watakapokuwa wanaendelea na vipimo vingine vipya.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), maradhi ya saratani yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka na kwa miaka ya karibuni watu milioni 8.2 walikufa kwa saratani duniani wakati robo tatu ya vifo hivyo vilitokea kwenye nchi zinazondelea.

WHO inasema saratani inayoongoza kwa kuua watu wengi ni ya kizazi, saratani ya matiti na ya tezi dume na kwamba ongezeko la ugonjwa huo linatokana na tabia hatarishi kama kula vyakula visivyozingatia mlo kamili, kutofanya mazoezi, matumizi makubwa ya pombe na sigara.

WHO inasema tatizo la saratani linaweza kupunguzwa kwa kutoa elimu kwa umma kwenda kupima wanapoona dalili za saratani na watu kuachana na mtindo wa maisha ambao ni hatarishi kwa afya zao.

## HABARI KIMATAIFA

## Mamia Hong Kong kupinga mabomu ya machozi

**HONGKONG, China**

MAMIA ya waandamanaji mjini Hong Kong waliojumuisha familia na watoto, wamefanya maandamano kulalamikia matumizi ya gesi ya machozi inayotumiwa na polisi, huku eneo hilo likijiandaa kwa maandamano zaidi ya kuipinga serikali baada ya wiki ya utulivu.

Wakibeba mabofu ya manjano na kupeperusha mabango yaliosoma, '' Hakuna gesi za machozi, okoa watoto wetu'', waandamanaji hao walimiminika katika eneo la kati la mji huo kuelekea katika makao makuu ya serikali katika kisiwa hicho kikuu cha Hong Kong.

Maandamano matatu yamepangiwa leo na yote yameidhinishwa na idara husika. Jana wanafunzi wa shule za upili na watu waliostaafu walishirikiana kuandamana dhidi ya kile walichokitaja kuwa ukatili wa polisi na kukamatwa kiholela.

Wanaharakati wameahidi kudumisha kasi ya maandamano hayo ambayo yamelikumba jimbo hilo linalotawaliwa na China kwa takriban miezi sita.

**DW**

## Atangazwa mshindi wa urais Namibia

**WINDHOEK, Namibia**

TUME ya Uchaguzi ya Namibia imetangaza kuwa Rais Hage Geingob, ameshinda uchaguzi wa nchi hiyo kwa kupata asilimia 56.3 ya kura.

Panduleni Itula ambaye ni mwanachama mwenzake wa chama cha SWAPO aliyeshiriki kama mgombea binafsi, alimaliza katika nafasi ya pili akiwa na asilimia 29.4.

Kiongozi wa chama cha upinzani, McHenry Venaani alikuwa wa tatu kwa asilimia 5.3. Rais Geingob aliwashuruku Wanamibia kupitia ukurasa wake wa Twitter, kwa kumchagua tena kuwa rais wao, akiahidi kuyaboresha zaidi maisha ya raia wa nchi hiyo.

Matokeo hayo yalionyesha kupungua pakubwa uungwaji mkono wa Geingob kutoka asilimia 87 katika uchaguzi wa awali mwaka wa 2014, na wapinzani wake katika uchaguzi wanadai kutokea dosari katika shughuli ya mwaka huu. Chama cha SWAPO kimeiongoza Namibia tangu uhuru kutoka Afrika Kusini mwaka 1990.

**DW**

# Maandamano yapamba moto Iraq

**BAGDAD, Iraq**

RAIA nchini Iraq, wameendelea na maandamano kwenye mji mkuu Baghdad na eneo la kusini mwa nchi hiyo ikiwa ni ishara ya kutoridhishwa na mipango ya kujiuzulu waziri mkuu na kusisitiza wanasiasa wote laghai kuondoka.

Waziri Mkuu, Adel Abdul Mahdi, alitangaza azma ya kujuzulu siku ya Ijumaa baada ya wito uliotolewa na kiongozi wa juu wa madhehebu ya

Washia wa kuitaka serikali kuachia madaraka ili kuhitimisha wiki kadha za machafuko.

Waandamanaji wamechoma matairi na kukizingira kituo cha polisi katika mji wa Nassiriya ulioko kusini mwa Iraq, wakishinikiza zaidi juu ya madai yao ya kufanyika mageuzi licha ya waziri mkuu kuahidi kujiuzulu.

Waandamanaji pia wamewasha moto kwenye madaraja matatu muhimu yanayokatisha Mto Euphrates, huku mamia ya watu wakikusanyika kwenye kambi ya maandamano iliyopo katikati ya mji.

Vikosi vya usalama vilitumia risasi za moja kwa moja, mabomu ya gesi na maguruneti dhidi ya waandamanaji kwa karibu miezi miwili na kuwaua zaidi ya watu 400 ikiwamo waliouawa siku za karibuni hususan katika mji wa Nassiriya.

Mikusanyiko imerejea tena licha ya ukandamizaji uliofanywa na vikosi vya usalama ambao ulisababisha vifo vya zaidi ya waandamanaji 40 siku mbili zilizopita.

Mji huo umeshuhudia ghasia mbaya zilizoikumba nchi hiyo tangu maandamano ya kuipinga serikali yalipoanza mjini Baghdad. Kuchomwa kwa ubalozi mdogo wa Iran katika Mji Mtakatifu wa Najaf ulioko kusini,

kulichochea ghasia zaidi na kusababisha Waziri Mkuu Abdul Mahdi kutangaza nia ya kujiuzulu.

Bunge la nchi hiyo lilitarajiwa kukutana jana kwa ajili ya kupigakura ya kutokuwa na imani na waziri mkuu. Hata hivyo ahadi ya Abdul Mahdi ya kujuzulu haijawaridhisha waandamanaji, ambao wanataka mfumo mzima wa kisiasa kufumuliwa wakidai kuwa umejaa ufisadi na kuwafanya maskini na bila fursa zozote.

Wairaq wengi wana hofu kwamba ghasia hizo zitaendelea kwa sababu familia nyingi zinaomboleza kwa kuwapoteza ndugu zao huku serikali ikichukua hatua kidogo kufanya mageuzi. Mkwamo wa kisiasa unatarajiwa kuendelea kabla ya mrithi wa Abdul Mahdi kuchaguliwa na serikali mpya kupatikana.

Tume ndogo ya haki za binadamu ya Iraq imesema siku ya Jumamosi katika taarifa yake kwamba wote waliohusika katika mauaji ya waandamanaji lazima washtakiwe na kwamba itakusanya ushahidi kwa ajili ya uchunguzi.

***DW***



Waandamanaji nchini Iraq wakishinikiza mabadiliko zaidi baada ya kufanikiwa kumng'oa Waziri Mkuu Mahdi. **PICHA: DW**

# Japan yaishukia Korea Kaskazini

**TOKYO, Japan**

WAZIRI Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, ameikemea Korea Kaskazini kwa vitendo vyake vya kurusha makombora mara kwa mara baada ya makombora mawili siku ya Alhamisi kuonekana katika anga la nchi hiyo.

Korea Kaskazini imepigwa marufuku kufyatua makombora marufuku hiyo imekuja chini ya makubaliano ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa wakati ambapo nchi hiyo inakabiliwa na vikwazo kwa sababu ya mpango wake wa nyuklia.

Kuondosha vikwazo imekuwa ni kusudio kubwa kwa Korea Kaskazini kuwa katika mazungumzo na Marekanimshirika wa Japan, lakini mazungumzo yamesimama tangu baada ya mkutano kati ya kiongozi wa nchi hiyo, Kim Jong-un na Rais Donald Trump ulipovunjika Februari.

Korea Kaskazini ilifyatua kile kinachoelezwa na waangalizi wa Korea Kusini kuwa ''makombora mawili'' kutoka Jimbo lake la Kusini la Hamgyong kuelekea bahari ya Japan siku ya Alhamisi.

Waziri Mkuu Abe alisema kitendo cha Korea Kaskazini kufytua makombora ni uasi kwa jumuiya ya kimataifa na hivyo hakipaswi kufumbiwa macho.

Chombo cha habari cha serikali ya Korea Kaskazini kilimkosoa vikali kiongozi huyo kwa madai kuwa ameshindwa kutofautisha kombora na mfumo wa kurusha roketi alipoitazama picha na ripoti.

Mazungumzo yaliyoanza tangu Oktoba mwaka huu kati ya Korea Kaskazini na Marekani yamesimama tangu kuvunjika kwa mkutanowa mwezi Februari mjini Hanoi. Trump na Kim walikutana tena katika eneo linalozigawanya nchi za Korea mwezi Juni na kukubaliana kuanza tena jitihada za kuanzisha tena mazungumzo.

Mei, Waziri Abe alisema kuwa yuko tayari kukutana na Kim bila masharti, hatua iliyotoa matumaini ya kuanza upya kwa mazungumzo

kuhusu masuala ya nyuklia pia kuhusu mgogoro wa muda mrefu kuhusu Korea Kaskazini kuwateka raia wa Japan.

Raia wa Japan walichukuliwa Korea Kaskazini miongo kadhaa iliyopita kusaidia kuwafunza majasusi wake. Japan inaamini raia wake 17 walitekwa, watano pekee kati yao wamerejeshwa.

***BBC***

# Jaji mstaafu akumbushia hukumu kesi ya ubakaji

**Na Elizabeth Zaya**

MWANAMKE wa kwanza kuteuliwa kuwa Jaji katika Mahakama ya Rufani, Eusebia Mnuo, amesimulia namna alivyoshughulikia kesi ya kwanza ya ubakaji baada ya kuingia katika nafasi yake hiyo.

Akizungumza katika mahojiano na televisheni moja inayoendesha shughuli zake kwa njia ya mtandao, Jaji Mnuo alisema miaka ya nyuma wanaume walikuwa wakiwabaka wanawake kinguvu na walipofikishwa mahakamani walijitetea kufanya hivyo kwa nia ya kuwaoa kama mbinu ya kukwepa kulipa mahali.

Jaji huyo ambaye ni mstaafu kwa sasa, alisema kupitia utetezi wa namna hiyo wanaume wote waliokuwa wakifanya vitendo hivyo walikuwa wakiachiwa.

"Mara ya kwanza kabisa wakati ndio naingia katika kazi hii jambo nililoanza kushughulikia ni sheria ya ubakaji ambayo imekuwa kwenye kanuni ya adhabu kwa muda mrefu, na kwa mara nyingi wabakaji wengi walikuwa wanaachwa huru kwa urahisi sana," alisema Jaji Mnuo.

"Kwa mfano kwa mara ya kwanza kabisa nilipoingia Mahakama Kuu, iliketwa kesi ya kijana mmoja ambaye alishirikiana na marafiki zake kumkamata binti kumpeleka nyumbani kwake na kumbaka, jambo ambalo wazazi wa binti waliamua kumshtaki," alibainisha na kuongeza:

"Lakini katika utetezi wa kijana, alisema kwamba yeye hakuwa na nia ya kumbaka, isipokuwa alifanya hivyo kwa sababu alikuwa anampenda na lengo lake lilikuwa ni kumuoa na kwamba alimkamata na kumpeleka kwake na kumbaka kwa sababu hakuwa na uwezo wa kulipa mahali."

"Kisheria, hakuna mapenzi ya kutumia nguvu, mtu anasema anampenda binti halafu anatumia marafiki zake wanamkamata na kumbaka, hapo hakuna upendo tena, kwa hiyo kipindi kile mabinti walikuwa wanaumizwa kwa mtindo huo, ilibidi nizitazame sheria za nchi zinasemaje, sheria za kimila na za kimataifa na ikabainika kwamba yule kijana alifanya makosa na nikaidhinisha afungwe miaka 30 jela," alisisitiza Jaji mstaafu Munuo.

Alisema jambo jingine analojivunia kwamba alilifanya kwa maadili na limesaidia watu wengi ni suala la wajane kunyimwa mirathi na kufukuzwa nyumbani walipokuwa wakifiwa na wenza wao.

"Hili nalo limesumbua wajane, wengi wao walikuwa wanafukuzwa na ndugu za mume bila kujali wameishi nao kwa kipindi kirefu au kifupi na wameshirikiana kutafuta mali, na hali hii ilichangia watoto wengi kuharibikiwa, kwa kweli kesi za namna hii ziliponifikia nilihakikisha kwamba wajane wanatoka na furaha," alisema Jaji Mnuo.

Jaji Mnuo alisema kadri idadi ya wanawake inavyozidi kuongezeka katika vyombo vya sheria, ndivyo na haki zinavyozidi kupatikana kwa wanawake na hata kupunguza vitendo vya unyanyasaji walivyokuwa wakifanyiwa kipindi cha nyuma.

"Sisemi kwamba wanaume hawatendi haki, lakini inahitaji moyo wa ziada unapokuwa katika nafasi ya kutenda haki, wanawake wako katika nafasi nzuri zaidi ya kutenda haki kwa sababu kwanza hayo mambo wamekuwa wakikumbana nayo moja kwa moja kwa hiyo ni rahisi hata kuyaelewa kwa haraka wanapofikishiwa kuliko ilivyo kwa majaji wa kiume," alisema Jaji Mnuo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni inayozalisha biskuti ya Bakers, Frildire Iviekerk (kushoto), akigawa biskuti kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Kinyerezi JICA, wakati wa hafla ya kutoa zawadi kwa shule 30 zilizoshiriki shindano la Kusanya Ushinde na Bakers iliyofanyika katika shule hiyo mwishoni mwa wiki. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# Ufaransa, Ubelgiji kutatua ukatili kwa wasichana

**Na Beatrice Shayo**

UBALOZI wa Ufaransa na Ubelgiji zimeungana kutatua changamoto zinazowakabili wasichana wenye umri mdogo ikiwamo kufanyiwa ukatili.

Wakizungumza hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Balozi wa Ubelgiji na Ufaransa katika kuunga mkono juhudi hizo waliandaa muziki wa kucheza 'Jasiri' ambao utafanywa kwa shule zote nchini ikiwa ni sehemu ya Siku 16 za Harakati za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Walisisitiza umuhimu wa kuwawezesha wanawake na kukuza usawa wa kijinsia ili kuhakikisha athari zisiongezeke.

Balozi wa Ubelgiji nchini Tanzania, Peter Van Acker, alisema kwa sasa wanafadhili mradi wa Tapala unaotekelezwa na asasi isiyo ya kiserikali TRIAS kwa jamii ya Wamaasai katika sehemu ya Kaskazini mwa nchi.

"Mradi wa Tapala unakusudia kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika vijiji vikuu vya Wamasai kwa kuongeza uhamasishaji na kuchukua hatua za kinga shuleni," alisema.

Alisema haki za wanawake na watoto zimekuwa kipaumbele cha sera nchini Ubelgiji.

Vile vile, alisema Ubelgiji iliandaa mkutano wa She Decides huko Brussels na nchi zaidi ya 50 na mashirika ziliahidi fedha kuboresha maisha ya wanawake na wasichana.

Alisema nchi inaleta fedha zinazotolewa kwa wanawake na wasichana kupitia ufadhili wa kimsingi kwa mashirika maalum kama Unicef, Unfpa na UN Women.

Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier alisema lengo la nchi hiyo ni kuongeza misaada ya maendeleo ya umma kwenye miradi inayohusiana na jinsia kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

Balozi Clavier alisema wakati huo, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, limejipanga kutatua tatizo la ukatili nchini.

Mwanzilishi na Mkurugenzi wa Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, alisema ubakaji bado ni shida kubwa nchini na moja ya uhalifu ulioripotiwa.

Gyumi alisema matokeo ya utafiti ya Unicef ya 2011 yanaonyesha kuwa nchini Tanzania, kati ya kila wasichana watano, wawili wamepitia unyanyasaji wa kijinsia.

"Ipo haja ya kuungana kwa pamoja kupinga ukatili wa kijinsia na tatizo la mimba za utotoni," alisema.

Msichana Initiative pia iliwezesha watoto wa shule 800 kutoka Dar es Salaam kutazama uchezaji wa muziki wa 'Jasiri' kwenye jumba la kumbukumbu la kitaifa.

# Mbaroni madai ya kukutwa na bangi bandarini

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, linamshikilia Khamis Hamad Sakaza (23) mkazi wa Mitiulaya Wete kwa tuhuma za kupatikana na vifurushi 30 vya dawa za kulevya aina ya bangi katika Bandari ya Wete.

Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Mohamed Shehan Mohamed, alisema tukio hilo lilitokea juzi jioni.

Alisema walimkamata mtuhumiwa huyo katika Bandari ya Wete akiwa na dawa hizo zinazosadikiwa kuwa ni bangi wakati akitokea mkoani Tanga.

"Tulimkamata mtuhumiwa wakati akitokea Tanga kuingia kwenye Mkoa wetu wa Kaskazini, jambo ambalo ni kosa kisheria," alisema.

Kamanda huyo alisema wanaendelea kufanya upelelezi wa kesi hiyo na atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

"Bangi tumeihifadhi na tunaendelea kumuhoji mtuhumiwa, huku tukiendelea kufanya uchunguzi wa shauri hilo, ambapo tutamfikisha mahakamani mara tutakapokamilisha upelelezi," alisema.

Kamanda Shehan aliwataka vijana kufanya kazi za halali ambazo zitawapatia fedha za kujikwamua kimaisha na sio kufanya kazi za haramu zitakazowaingia kwenye matatizo.

"Zipo kazi nyingi za halali tuzifanye na tusifanye kazi za haramu ambazo matokeo yake ni kuishia chuo cha mafunzo, hapo itakuwa hujajisaidia bado," alieleza.

Alisema mikakati yao ni kufanya operesheni mbalimbali katika mkoa huo katika kuhakikisha wanadhibiti uingizaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

"Tuna operesheni mbalimbali katika Mkoa wetu kuwasaka wahalifu wanaojishirikisha na uingizaji pamoja uuzaji wa dawa za kulevya, lengo ni kudhibiti," aliongeza.

Aidha, kamanda huyo aliwataka masheha kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha dawa za kulevya hazuingii katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**"Zipo kazi nyingi za halali tuzifanye na tusifanye kazi za haramu ambazo matokeo yake ni kuishia chuo cha mafunzo, hapo itakuwa hujajisaidia bado," alieleza.**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**MATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana wako tufuatilie msingi wake wa hisabati hadi pale shida ilipoanzia na kuanza kuujenga tena upya. Wahusika ni kuanzia darasa la tano hadi kidato cha sita.Tuitions za majumbani zinapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho Dsm. Simu 0655.0754 617987

### KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:......20....**
**Mdai: HELLEN MNDEME**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: SHANAM ABRAHAM**

Kwa:
SHANAM ABRAHAM

Ombi la Mdai:
HELLEN MNDEME

Madai ya: PESA SHILINGI 1,200,000/=
Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 03 mwezi 12 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 11 mwaka 2019.

115539802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo: MIKESE

Usimamizi wa mirathi No; 6/2019

Ombi la **ATHUMAN ALLY MUHINA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JUMA SAID MGONGOLA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 27/11/2019.

115539702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo - MWANJELWA**
**Wilaya ya...MBEYA**
**MADAI NAMBARI...95...YA...2019**

**Mdai...** **SAULI SOLOMONI MWALABHILA**
**Mdaiwa...** **EMMANUEL KESSY**

**POPOTE ULIPO**
Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza hapa chini)
**NI JUU YA MADAI YALIYOPO MAHAKAMANI**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumatano tarehe 04/12/2019 saa 2.30 asubuhi kwa kujibu madai haya na kwa kuwa hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta Mshauri wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalizo: Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 19/11/2019.

215539502

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.193/2019**
**JENIPHER HATSON MSONGOLE....................MDAIWA WA KWANZA**
**TUNDUMA TOWN COUNCIL...........................MDAIWA WA PILI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: 1) JAMAL M.AHMED**
**2) TUNDUMA TOWN COUNCIL**

Fahamu kwamba shauri limefunguliwa dhidi yakokatika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 05/12/2019 saa 2:30 asubuhi,mbele ya Mhe.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya Mjini.

Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahili ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 19/11/2019.

215539502

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

LAKE OIL LIMITED anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 943 CMJ TOYOTA VITZ. Chassis namba SCP100371641. Engine namba 1SZ4992104.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: KBA/RB/6902/2019.

115539602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya mwanzo DODOMA MJINI**
**wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 249/2019**
**MDAI..................................................HAMPHREY SANGU**
**MDAIWA.........................................BONIFACE MAKANGE**

**KWA: BONIFACE MAKANGE**
**DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba

**MADAI YA TSH.5,000,000/=**
Hivyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Jumanne tarehe 10/12/2019 saa 08.30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Na kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa Amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 29/11/2019

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ARUSHA MJINI**
**WILAYA YA ARUSHA**

**SHAURI LA MADAI TALAKA 97/2019-PETER EALIAKIM**
**DHIDI YA JACKLINE NKYA**
**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)**

**Kwa JACKILINE NKYA**
Kwa kuwa imelazimika uhudhurie mahakamani na kujibu madai yani shahidi kama ifuatavyo:
TALAKA NA 97/2019

UNAAMRISHWA NA JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama siku ya JUMATATU tarehe 16.12.2019 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa.

**USIKOSE KUHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/F Na 114A,sura 16KA hivyo mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria .

**Hati hii imetolewa kwa ombi la PETER ELIAKIM.**


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# KIPIGO

## CHAMKERA KOCHA BAYERN MUNICH



**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Hansi Flick, aliachwa "amekasirika" baada ya kushuhudia kikosi chake kikipoteza nafasi na kukumbana na kichapo cha mabao 2-1 nyumbani kutoka kwa Bayer Leverkusen.

Leon Bailey alifunga kwa mara ya kwanza mabao mawili katika mchezo wa Bundesliga wa juzi Jumamosi kwenye dimba la Allianz na kuwaacha mabingwa hao watetezi kwenye wakati mgumu chini ya kocha wa muda, Flick.

Bayern iligonga mwamba wa goli mara tatu na kupiga mashuti langoni mwa timu pinzani mara 11, lakini hawakuweza kuongeza bao baada ya lile la Thomas Muller alilofunga kipindi cha kwanza, licha ya Jonathan Tah kutolewa nje kwa kadi nyekundu dakika tisa kabla ya mchezo kumalizika kwa kumchezea vibaya Philippe Coutinho, aliyetokea benchi.

"Kwa uhakika kabisa nawalaumu wachezaji wangu kwa kiwango cha leo (juzi)," alisema Flick katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Walicheza vizuri na kujaribu kushinda mchezo. Inatia hasira kushindwa kupata pointi katika mchezo kama ule.

"Hatukucheza kwa umakini katika kipindi cha kwanza na tuliruhusu kwa urahisi mabao yao mawili.

"Siwezi kuilaumu sana timu kwa namna walivyocheza, lakini kiukweli hatukuwa makini licha ya kuanza kuongoza kwa bao moja."

## KLOPP AMSIFIA KIPA WA AKIBA KUIBEBA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp amesifia mchango wa golikipa Adrian aliyetoka benchi kwa kuchangia "ushindi mzuri" baada ya Liverpool kuifunga Brighton and Hove Albion mabao 2-1, licha ya kutolewa kwa Alisson kwa kadi nyekundu.

Mabao mawili ya kichwa ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Virgil van Dijk yaliwaweka vinara hao wa Ligi Kuu kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuendelea kuongoza msimamo, lakini Liverpool walimaliza mchezo pale kwenye dimba la Anfield kwa kumkosa Alisson aliyetolewa nje dakika ya 76.

Adrian aliokoa shuti la adhabu ndogo ya Lewis Dunk, huku kipa huyu akionekana kuwa kwenye kiwango bora cha kuupanga ukuta wake vizuri.

Hata hivyo, Liverpool waliweza kuondoka na pointi zote tatu na kuendeleza rekodi ya kutofungwa kwenye Ligi Kuu, huku Adrian akiokoa pia shuti la Aaron Mooy.

"Kwa uhakika kabisa mabao mawili ya Virgil bila shaka yanamfanya kuwa nyota wa mchezo, lakini kwangu mimi Adrian ndiye alikuwa nyota wa mchezo," alisema kocha huyo wa Wekundu hao, Klopp.

"Kwa sababu kuingia kwenye mchezo kama ule na kuokoa hatari za wazi mbili, sio jambo rahisi.

"Moja ilikuwa hatari zaidi. Na kipa alicheza kwa ustadi mkubwa zaidi, ni ngumu kwa mtu mwingine kuona kwa karibu kile alichokifanya, lakini ukweli ni kwamba alicheza vizuri kabisa.

"Pengine tungefanya tofauti, lakini hatukujiandaa kwa hili, nina uhakika tulicheza kwa kutafuta ushindi na tulifanikiwa kuupata, kwa uhakika kabisa nina furaha kubwa."



## LAMPARD AFUNGUKA KUMKOSA ABRAHAM

**LONDON, England**

FRANK Lampard anataka kuona "hali ya kupambana" wakati timu yake ikitakiwa kusahau kichapo cha bao 1-0 walichokipata nyumbani kutoka kwa West Ham, huku akikataa kulaumu kukosekana kwa Tammy Abraham aliye majeruhi ndio sababu ya matokeo hayo.

Abraham aliukosa mchezo huo kwa sababu ya mejeruhi aliyoyapata wakati Chelsea ikitoka sare ya 2-2 na Valencia kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Jumatano na Olivier Giroud alichukua nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya West Ham, juzi Jumamosi.

Lampard pia alimuacha benchi N'Golo Kante na alishuhudia West Ham wakitawala eneo la kiungo na wakapata ushindi wao wa kwanza katika mechi nane za Ligi Kuu England.

Chelsea watacheza na Aston Villa kwenye dimba la Stamford Bridge katikati ya wiki hii kabla ya kusafiri kwenda pale Goodison Park kucheza na Everton Jumamosi ijayo, na Lampard atafanya mabadiliko baada ya kikosi chake kushuhudia kikipoteza mchezo wa pili wa ligi nyumbani.

"Haiwezi kuwa sababu ya mchezaji mmoja," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari baada ya kuulizwa kuhusu umuhimu wa Abraham ambaye ni majeruhi.

"Tulichelewa kuwasili kutoka Valencia na nililazimika kufikiria kuhusu mchezo unaokuja. Hatuwezi kwenda msimu mzima kwa kuwategemea wachezaji 10 au 11.

"Nafikiri timu ina ubora wa kutosha kuweza kushinda mechi. Ni mara chache sana nasema kwamba kuna siku tulicheza kwa kiwango cha chini. Leo (juzi) ilikuwa moja ya siku hiyo."



# VIEIRA
## AKATAA UKOCHA ARSENAL

**NICE, Ufaransa**

PATRICK Vieira amekataa uwezekano wa yeye kuchukua mikoba ya ukocha pale Arsenal wakati kocha huyo wa Nice akisema kwamba "ni kazi ngumu".

Unai Emery alifukuzwa kama kocha mkuu wa Arsenal Ijumaa iliyopita baada ya kuiongoza timu hiyo kwenye mechi saba bila ushindi kwenye Ligi Kuu England.

Vieira - mchezaji wa zamani wa Arsenal amekuwa akitajwa kuwa na nafasi kubwa ya kupewa mikoba ya ukocha katika timu hiyo inayotumia Uwanja wa Emirates, lakini kocha huyo wa Nice amepuuzia ripoti hiyo.

"Kuna vitu ambavyo siwezi kuvizuia, watu wanazungumza mambo mengi, mengi ni ya kweli na mengine ni uongo," alisema akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo wa Nice kushinda mabao 3-1 dhidi ya Angers kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa, juzi Jumamosi.

"Sijasema chochote, sijazungumza kuhusu hilo. Mimi ni kama nyinyi, naona, nasoma na nasikia kila kitu na huo ndio ukweli."

Vieira, ambaye kikosi chake cha Nice kipo nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, amesema nafasi iliyopo Arsenal itakuwa kazi ngumu kwa mrithi wa Emery.

"Ni kazi ngumu, nakubali hilo," alisema. "Namsapoti Emery, mara zote ni huzuni kuona kocha akipoteza kazi.

"Leo ni yeye, kesho inaweza kuwa kwangu mimi, lakini haraka unavyoamua kuanza kazi, unatakiwa kukubali pia kufukuzwa kazi muda ukifika."

Vieira alitumia misimu nane pale Arsenal akiwa mchezaji, akishinda mataji mawili ya Ligi Kuu na matatu ya Kombe la FA.

Mchezaji mwenzake wa zamani, Freddie Ljungberg, kwa sasa ndiye amepewa jukumu la kuwa kocha wa muda wa Arsenal.

# Martinez: Hazard atang'ara zaidi Madrid




**MADRID, Hispania**

MUDA wa Eden Hazard pale Real Madrid utamsaidia kuimarisha "kitu maalumu", kwa mujibu wa kocha wa timu ya taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez.

Hazard amekuwa na wakati mgumu wa kurudisha kiwango chake pale Madrid kabla ya kuumia kifundo cha mguu kwenye mchezo wa sare wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain, Jumanne iliyopita.

Mchezaji huyo wa zamani wa Chelsea ana bao moja na pasi za mwisho mbili katika mechi 13 alizocheza msimu huu, lakini Martinez anaamini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji atakuwa nyota wa Madrid.

"Nilimuona Eden pale (Santiago) Bernabeu akicheza dhidi ya PSG na naweza kusema kwamba tuliona muda wa kuvutia zaidi," alisema Martinez juzi Jumamosi.

"Alitufundisha namna gani msimu wake na Real Madrid utakavyokuwa na ukweli ni kwamba, unakufanya umwangalie mara mbilimbili.

"Mbaya ni kwamba alilazimika kutoka nje kwa sababu ya majeruhi, lakini tuliona kwamba, Eden Hazard atakwenda kuchangia zaidi, na wachezaji wenzake wanamjua vizuri.

"Na ukweli ni kwamba, Eden muda wake pale Real Madrid utakuwa na kitu fulani kizuri zaidi."

# Messi ni bora, mpeni Ballon d'Or – Valverde

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ernesto Valverde anaamini upigaji wa kura ya kumchagua mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or utakuwa rahisi, akisema Lionel Messi anastahili tuzo hiyo.


Messi mwenye umri wa miaka 32, anapewa nafasi ya kuweka rekodi ya kushinda tuzo hiyo ya Ballon d'Or kwa mara ya sita, wakati itakapofanyika leo Jumatatu jijini Paris nchini Ufaransa.

Valverde, ambaye jana Jumapili timu yake ilikwenda kucheza na Atletico Madrid katika mchezo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, amesema upigaji wa kura hautakiwi kuwa na tatizo kwa sababu Messi ndiye mchezaji bora duniani.


"Sifuatiliagi sherehe za tuzo hizi kwa sababu mchakato ni mrefu. Kura yangu nafikiri itakuwa sawa na wengine wote," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nitapiga kura kwa mchezaji bora. Kila mwaka unapigana kura kuangalia namna msimu ulivyokwenda kwa wachezaji.

"Kama unatakiwa kutoa tuzo ya mchezaji bora, ni suala la kumpatia tu Messi na wala hakuna tatizo katika hilo."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AKUBALI AMEPEPESUKA EPL

Kocha huyo asema kwa sasa hawezi kufikiria kuhusu mbio za kuwania taji hilo…

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesisitiza Manchester City haiwezi kufikiria kuhusu taji la Ligi Kuu England baada ya timu yake kuzidi kupoteza kwenye mbio za ubingwa huo dhidi ya Liverpool, wakati akishuhudia ikitoka sare ya 2-2 na Newcastle.

Kwa matokeo hayo, City iko nyuma kwa pointi 11 na vijana wale wa Jurgen Klopp ambao waliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion, juzi Jumamosi.

City waliongoza mara mbili kwenye mchezo huo uliopigwa kwenye dimba la St James' Park kupitia kwa mabao ya Raheem Sterling aliyefikisha magoli 15 msimu huu kwa klabu hiyo, lile la Kevin De Bruyne.

Lakini Jetro Willems na Jonjo Shelvey wakaisawazishia Newcastle United katika mchezo huo.

Guardiola alishuhudia timu yake ikishindwa kupata pointi zote tatu ili kuweza kuendelea kuifukuza Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa ligi hiyo.

Baada ya hapo, anaona ni ngumu kwa timu yake kufikiria kuhusu ubingwa.

"Sio muda wake. Tuna wapinzani wengine mbele yetu," alisema akijibu swali la waandishi wa habari alipoulizwa kuhusu City kama bado ipo kwenye mbio za kulitwaa taji hilo kwa mara ya tatu mfululizo.

"Kwa sasa tunajaribu kushinda michezo, kushinda mechi zote na kuangalia nini kitatokea.

"Sio jambo nzuri kwa sasa kufikiria kuhusu taji la Ligi Kuu England kwa kuwa na pointi nyingi kiasi gani. Tunatakiwa kushinda mechi. Kama hatushindi, itakuwa ngumu zaidi kwetu.

"Msimu uliopita dhidi ya (Newcastle) tulicheza vibaya. Leo (juzi) tulijaribu kila njia kushinda mchezo, na huo ndio ukweli.

"Tulicheza kwa kiwango kizuri kabisa, tulizuia, tulitengeneza nafasi na kila kitu. Tulitawanya mipira mbele kwa uzuri kabisa, tulitafuta nafasi na tulifika golini kwao mara nyingi tu.

"Bahati mbaya, hatukuweza kufunga na hilo ndilo lilikuwa jambo muhimu zaidi kwetu."

Wakiwa wameongoza mara mbili na baadaye mabao yote kusawazisha inaonyesha kikosi cha City kina kazi kubwa ya kufanya ili kurudisha ubora wake kwa wiki za hivi karibuni, lakini Guardiola hakusita kuwasifia Newcastle.

"Ni bora kufunga moja, chukua muda na funga la pili. Lakini walicheza vizuri," alisema.

"Katika hali moja, walilinda vizuri na kujaribu kusukumiza mbele mashambulizi na Shelvey aliirudisha timu yake mchezoni."

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL, SPURS VITANI**

LIVERPOOL na Tottenham ziko tayari kupambana vita kuwania saini ya kiungo wa Lyon na Timu ya Taifa ya Holland, Memphis Depay, ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Sunday Express)***

**PSG KUMFUNGA MBAPPE**

MABOSI wa Paris St-Germain wako tayari kumpa ofa ya kusaini mkataba mpya mshambuliaji wake Mfaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 20. ***(Le10Sport - in French)***

**FLORES KUFUKUZWA WATFORD**

MABOSI wa klabu ya Watford walitarajia kukutana jana ili kujadili uamuzi wa kumfukuza kazi kwa mara ya pili, kocha wake, Quique Sanchez Flores. ***(The Athletic - subscription required)***

**POCHETTINO KUKAMULIWA**

ALIYEKUWA Kocha wa Tottenham, Mauricio Pochettino, ambaye anahusishwa na tetesi za kutakiwa na Manchester United pamoja na Arsenal, atalazimika kulipishwa kiasi cha pauni milioni 12.5, endapo atajiunga na timu nyingine ya Ligi Kuu England msimu huu. ***(Sunday Express)***

**RODGERS AIWAZA ARSENAL**

ARSENAL inatarajia kusubiri hadi katika kipindi cha majira ya joto mwakani ili kumkabidhi mikoba ya timu kocha mpya, wakati mmoja wa makocha mwenye nafasi ya kutua klabuni hapo, Brendan Rodgers, anaeleza kwamba kupata nafasi ya kuiongoza Gunners ni moja ya ndoto zake. ***(Star on Sunday)***

**ARTETA APIGIWA DEBE**

INAELEZWA kuwa Kocha Msaidizi wa Manchester City, Mikel Arteta, ndiye mtu sahihi anayefaa kurithi mikoba ya Mhispania Unai Emery katika kikosi cha Arsenal. Emery alitimuliwa kuiongoza timu hiyo Ijumaa iliyopita. ***(Sunday Mirror)***

**LJUNGBERG ATAKIWA WEST**

KLABU ya West Ham imeanza mchakato wa kumwinda Kaimu Kocha Mkuu wa Arsenal, Freddie Ljungberg, kwa ajili ya kutua kwenye kikosi chake kurithi mikoba ya Manuel Pellegrini. ***(Star on Sunday)***

**MOURINHO AITOSA MADRID**

JOSE Mourinho alipewa ofa ya kulipwa pauni milioni 12 na Real Madrid kwa lengo la kukataa kujiunga na klabu nyingine na kusubiri uongozi wa vigogo hao wa Hispania wamfukuze kazi Zinedine Zidane, kabla ya kufanya uamuzi wa kutua Tottenham. ***(Sun on Sunday)***

**HOWE ATAJWA EVERTON**

EVERTON imeweka wazi nia yake ya kumwajiri Kocha wa Bournemouth, Eddie Howe, ambaye ni shabiki wa klabu hiyo maarufu Toffees tangu akiwa mtoto, ili kuchukua nafasi ya Marco Silva, ambaye amekalia kuti kavu. ***(Sunday Mirror)***

**AUBAMEYANG ANUKIA MADRID**

REAL Madrid inapanga kutuma ofa ya pauni milioni 70 kwa Arsenal ili kumsajili straika wa Timu ya Taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang (30), huku pia ikimtoa kiungo wake kutoka Colombia, James Rodriguez (28), kama sehemu ya kufanikisha usajili wake. ***(Eldesmarque, via Star)***

**CHELSEA YAMTAJA SANCHO**

CHELSEA imewaweka kwenye orodha ya nyota inaowahitaji, Zaha na winga wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho (19), kama sehemu ya kuimarisha safu yake ya mawinga. ***(Sunday Express)***

**COSTA ATAKIWA FLAMENGO**

STRAIKA Mhispania, Diego Costa (31), ambaye alijiunga na Atletico Madrid akitokea Chelsea mwaka 2018, anatarajia kusajiliwa na Flamengo kwa dau la pauni milioni 25. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# MWAKYEMBE AWALILIA MASHABIKI WA MWAKINYO

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigela, kufuatia vifo vya mashabiki wawili waliofariki wakiwa njiani kurejea jijini humo baada ya kutoka kumshangilia bondia wa ngumi za kulipwa nchini, Hassan Mwakinyo.

Bondia hiyo aliibuka mshindi kwa pointi katika pambano la kuwania uzito wa Super dhidi ya mpinzani wake kutoka Ufilipino, Arnel Tinampay, ambalo lilifanyika juzi kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Mashabiki waliofariki baada ya gari walilopanda kupata ajali usiku wa kuamkia jana, ni pamoja na Hussein Mkubwe na Ibrahim Omari.

"Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya vifo vya ndugu zetu wawili ambao walikuja Dar es Salaam, kumuunga mkono kijana wetu, Hassan Mwakinyo, wakati analiwakilisha Taifa kwenye pambano la kimataifa dhidi ya bondia Arnel Tinampay kutoka Ufilipino," alisema Dk. Mwakyembe katika taarifa yake.

Kiongozi huyo ametoa pole pia kwa familia, ndugu, jamaa na mashabiki wa mchezo wa masumbwi kwa kuondokewa na wapendwa wao na pia anawaombea majeruhi wapate nafuu haraka.

Akizungumza na gazeti hili jana, kiongozi wa msafara huo ambao ulikuwa na mabasi madogo aina ya Coster kutoka Tanga, Nasser Makau, alisema kuwa ajali iliyowaua mashabiki hao ilitokea katika eneo la Bunju, Dar es Salaam baada ya kugongana na lori la kubeba mizigo ambalo lilikuwa linatokea Tanga.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, ametoa pole kwa familia za wafiwa, mashabiki wote wa ngumi jijini humo, huku pia akiwaombea majeruhi wapone haraka.

Shigela alisema kuwa serikali ipo pamoja na majeruhi hao pamoja na familia ambazo zimepoteza wapendwa wao katika kipindi hiki kigumu.

Kwa upande wake, Mbunge wa Jimbo la Muheza, Tanga Balozi, Adadi Rajabu, alisema kuwa kifo cha mashabiki hao kimewashtua sana kwa kuwa walikwenda salama kumshangilia Mwakinyo na anawaomba wanafamilia kuwa watulivu.

"Tumepata pigo kubwa sana juu ya vifo vya mashabiki hawa wawili," alisema kwa kifupi, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Henry Shekifu.



Mchezaji wa tenisi chipukizi, Isando John, akipiga mpira kuurudisha kwa mpinzani wake hayupo (pichani), katika mashindano ya BQ, yaliyofanyika kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kikosi Zanzibar Heroes kamili

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WACHEZAJI 12 wa Timu ya Soka ya Zanzibar (Zanzibar Heroes), wanaocheza katika klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara wameripoti katika kambi ya timu hiyo inayojiandaa na mashindano ya Kombe la Chalenji yatakayofanyika kuanzia Jumamosi jijini Kampala, Uganda, imeelezwa.

Nyota hao waliungana na wachezaji wenzao wanaocheza katika Ligi Kuu Zanzibar ili kujiandaa na michuano hiyo inayotarajiwa kushirikisha timu 12 za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

Kocha Mkuu wa Zanzibar Heroes, Hemed Morocco, aliwataja nyota hao kuwa ni pamoja na Feisal Salum "Fei Toto", Mohamed Issa Banka, Ali li na Abdul-Azizi Makame kutoka Yanga, Abdallah Sebo (Azam), Othman Mmanga (Polisi Tanzania), Hassan Nassor Abal, Ibrahim Makame (Coastal Union), Mohamed Mwali (Polisi Tanzania), Mohamed Mussa (Mbeya City) na Mohamed Wawesha wa JKT Tanzania.

Morocco aliwataja wachezaji ambao bado hawajafika katika kikosi hicho ni Aggrey Moris, Mudathir Yahya, Kassim Suleiman kutoka Azam na Awesu Awesu na Abdul-Swamad Kassim wa Kagera Sugar.

"Kikosi cha awali kilikuwa na wachezaji 47, nimeshafanya mchujo wa awali, sasa wamebakia nyota 34, na mchujo wa mwisho utabakisha wachezaji 21, ambao ndio nitakwenda nao kwenye mashindano," alisema Morocco.

Aliwataja nyota hao aliowaacha ni Abdullatif Said kutoka Jamhuri, Ally Haji (Mwenge), Ally Juma Maarifa "Mabata" (Malindi), Mustapha Muhsin "Park" (Zimamoto), Juma Kukuti (Polisi Tanzania), Said Salum "Etoo" (Kipanga), Khalid Shaaban (Rich Boys) na Mohamed Abdalla wa Mlandege.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Hamasa ya timu hiyo, ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema kamati hiyo itaendelea kutoa hamasa kwa jamii ili kuhakikisha Zanzibar Heroes inafanya vizuri katika michuano hiyo ya mwaka huu.

Mahmoud alisema kuwa wachezaji wao wanaendelea vema na mazoezi na amewataka Wazanzibar kuendelea kuichangia timu yao ili wakamilishe maandalizi yote muhimu yanayohitajika.

## BMT yaendelea kukumbusha usajili

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limepiga marufuku vyama vya michezo ambavyo bado havijakamilisha usajili kuendelea kushiriki katika michezo mbalimbali mpaka pale itakapokamilisha taratibu za kisheria.

Ofisa Maendeleo ya Michezo wa Manispaa ya Singida, Samweli Mwaikenda, alisema kuwa vyama vitakavyoendelea kukaidi taratibu na sheria zilizowekwa hapa nchini, vitafungiwa mara moja.

Mwaikenda alisema kuwa bado vyama vingi havijatekeleza agizo hilo la serikali, licha ya kupewa maelekezo na mwongozo wa kukamilisha mchakato wa usajili.

"Tutalazimika kuchukua hatua kwa vyama ambavyo vinakaidi agizo hili, utafika wakati tutawazuia kufanya shughuli za michezo mpaka watakapokuwa wamekamilisha usajili," alisema Mwaikenda.

Alivitaja vyama vinne vya michezo ya riadha, mpira wa kikapu, mpira wa wavu na netiboli, ambavyo huendesha mashindano mbalimbali hapa nchini, kukamilisha mchakato huo wa usajili kabla "rungu" la kufungiwa halijawakuta.

Meneja wa timu ya soka ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Dodoma, George Mzuri, alikiri klabu yake kupokea barua ya kukumbushwa kufanya usajili na kuelezwa kwamba timu isiyosajiliwa haitaweza kushiriki mashindano yoyote.

## Viongozi Mbeya City waamshwa

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, ameutaka uongozi wa timu hiyo kujipanga upya kwa ajili ya kukukisuka upya kikosi ili kukabiliana na ushindani uliopo, kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.


Mwambusi aliamua kujiuzulu kuifundisha timu hiyo na uongozi wa Mbeya City, umemtangaza Kocha Msaidizi, Mohammed Kijuso, kukaimu nafasi hiyo.

Mwambusi aliliambia gazeti hili kuwa uongozi wa Mbeya City wanatakiwa kuwekeza zaidi katika timu hiyo ili ifanye vizuri kwenye Ligi Kuu Bara na kutatua changamoto zinazoikabili klabu yao.

"Mimi naomba viongozi wa Mbeya City washirikiane na watafakari kwa pamoja ili kuondoa changamoto zilizopo, kufahamu chanzo kinachosababisha timu ifanye vibaya," alisema Mwambusi.

Kocha huyo aliamua kujiweka pembeni baada ya kuona "jahazi" la Mbeya City linazidi kuzama kutokana na kushindwa kasi iliyopo kwenye ligi hiyo inayoshirikisha klabu 20.

Michezo
Jumatatu Desemba 2, 2019
Nipashe



Guardiola akubali amepepesuka EPL
HABARI UK 30



Mshambuliaji wa Liverpool, Sadio Mane (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Brighton & Hove Albion, Davy Propper, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield juzi usiku. Liverpool ilishinda mabao 2-1. **PICHA: TOUCHLINE**

# YANGA, KMC FC KIBARUANI BARA

●●●Ni katika mchezo wa kiporo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo...

**Na Somoe Ng'itu**

HAKUNA kulala! Ndio maneno ya Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa kuelekea mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC inayotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Yanga itashuka katika mchezo wa leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1, walioupata dhidi ya Alliance FC ya Mwanza, wakati KMC FC, ambayo nayo inafundishwa na Kaimu Kocha Mkuu, Ahmady Ally, ilichapwa magoli 2-0 na Mbao FC.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkwasa, alisema kuwa wachezaji wake wamejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo na wamejipanga kupambana ili malengo yao ya kuchukua pointi tatu muhimu yatimie.

Mkwasa alisema amewaandaa wachezaji wake kukutana na ushindani na kuwakumbusha kila mechi kwao ni sawa na fainali, hivyo hawatakiwi kudharau timu yoyote inayoshiriki ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Wachezaji wangu wako katika hali nzuri, tumejiandaa kupambana kwa sababu tunajua ligi ni ngumu, kila timu imejipanga kuhakikisha inapata matokeo mazuri ili isishuke daraja, kila siku wachezaji wanaimarika na ushindani unaongezeka, kila timu inataka kukaa kwenye nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi," alisema Mkwasa.

Nahodha wa timu hiyo, Papy Tshishimbi, aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo na wanataka kuona hawapotezi mchezo huo.

"Tunahitaji ushindi, na ili tupate ushindi ni lazima tujitume, tutaingia uwanjani kucheza kwa nguvu, hayo ndiyo malengo yetu kwa ajili ya mechi ya kesho (leo), na nyingine zitakazofuata," alisema Tshishimbi.

Naye Ahmad Ally, anasema kuwa wanaiheshimu Yanga na wataingia katika mchezo huo kwa lengo la kusaka matokeo mazuri na si kitu kingine.

"Tunaamini tulichokiandaa, tunaamini tutaweza kufanya kile tunachotarajia, mpaka sasa kila mtu anapointi moja, tunachofanya ni kwenda kupambana kusaka pointi mbili, tunaiheshimu timu tunayokwenda kukutana nayo, lakini na sisi tuna mipango yetu kwa ajili ya mechi hii," alisema kocha huyo.

Ofisa Habari wa KMC, Anwary Bhinde, alisema kuwa bado kikosi chao kinapitia wakati mgumu kutokana na mabadiliko ya benchi la ufundi, lakini Yanga wasitarajie mteremko katika mchezo huo.

"Timu yetu inaendelea na maandalizi ya mechi dhidi ya Yanga, wachezaji wako katika hali nzuri, na wameahidi kurekebisha makosa yaliyotokea Mwanza, tunapitia wakati mgumu, lakini tunasema kuteleza sio kuanguka," alisema kiongozi huyo.

Baada ya mechi ya leo, Ligi Kuu inatarajia kusimama ili kupisha maandalizi ya Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars), inayotarajiwa kwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji yatakayofanyika kuanzia Jumamosi jijini Kampala, Uganda.

## Ronaldo kundi gumu Euro 2020

**BUCHAREST, Romania**

MABINGWA wa Ulaya, Timu ya Taifa ya Ureno wamepangwa katika Kundi F pamoja na vigogo, washindi wa Kombe la Dunia, Ujerumani na Ufaransa katika mashindano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Euro 2020.

Ratiba hiyo iliyotolewa usiku wa kuamkia jana inaonyesha kuwa, Ujerumani itacheza mechi ya ufunguzi dhidi ya Ufaransa katika mashindano hayo yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Juni 12 hadi Julai 12, mwakani.

**Katika kinyang'anyiro hicho, Kundi A linaundwa na Italia, Uswisi, Uturuki na Wales wakati Ubelgiji, Urusi, Denmark, Finland wanaunda Kundi B huku Ukraine, Uholanzi, Austria na timu nyingine, zimepangwa kwenye Kundi C.**

England, Croatia, Jamhuri ya Czech na nyingine itakayojulikana baadaye kati ya Scotland, Israel, Norway au Serbia zenyewe ziko katika Kundi D.

England yenye itaanza kampeni zake kwa kuwavaa Croatia, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Wembley, huku kwa mara nyingine tena ikipangwa dhidi ya timu ya Jamhuri ya Czech.

Kikosi hicho kinachonolewa na Gareth Southgate, mwaka jana kilitolewa na Croatia katika hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Dunia.

Mashindano hayo yamepangwa kuchezwa katika mataifa 12 za Ulaya, mfumo ambao umewekwa maalumu kusherehekea miaka 60 ya kuanzishwa kwa michuano hiyo ya Ulaya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >